

Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Saba - Tarehe 12 Novemba, 2003

(Mkutano Ulianiza Saa Tatru Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Posta Tanzania kwa Mwaka 2002 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Postal Bank for the Year 2002*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 87

Umaskini Mkao wa Shinyanga

MHE. PAUL N. MAKOLO aliuliza:-

Kwa kuwa Shinyanga ni mionganini mwa Mikoa iliyoye nyuma sana kimaendeleo na inayokabiliwa na umaskini uliokithiri ingawa kijiografia una raslimali ya kuweza kuondoa umaskini huo:-

(a) Je, umaskini katika Mkao huo unasababishwa na nini?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa umaskini katika Mkao huo unasababishwa na mipango mibaya ya maendeleo kati ya baadhi ya Mikoa nchini?

(c) Kwa kuwa ili kuondoa umaskini ni muhimu kuongeza ajira, pato na lishe bora na kuboresha huduma za afya na kuimarisha huduma za maji, je, jambo hili limeteklezwaje katika Mkao wa Shinyanga?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Umaskini Mkoani Shinyanga kama ilivyo katika Mikoa mingine unachangiwa na miundombinu duni katika uzalishaji, wananchi wengi bado wanategemea jembe la mkono, elimu duni katika kutumia raslimali zilizopo na kukosekana kwa masoko ya mazao yazalishwayo hapo Mkoani. Kushuka kwa bei ya zao la Pamba ambalo ni zao kuu la biashara Shinyanga, kumechangia umaskini kwa kiwango kikubwa. Aidha, hali ya ukame katika maeneo mengi pamoja na kuanguka kwa Vyama vya Msingi vya Ushirika kumechangia pia umaskini.

Pia wananchi wengi bado wanaamini kwamba kuwa na idadi kubwa ya mifugo ndiyo utajiri badala ya kutumia mifugo hiyo ili kujiweka katika hali nzuri zaidi ya maisha. Kama inavyoeleweka wananchi wengi wa Shinyanga ni wafugaji, ni muhimu kuboresha na kupanua ufugaji ili kupata mifugo mingi na bora kwa ajili ya kuvutia soko. Pia fedha zipatikanazo kutokana na mifugo hiyo zitumike kwa shughuli za maendeleo ya Kaya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba umaskini katika Mkoa wa Shinyanga umesababishwa na mipango mibaya ya maendeleo kati ya baadhi ya Mikoa nchini. Mipango mizuri ikiwepo ile ya utekelezaji imekuwa na mapungufu kwa maana ya upungufu wa fedha, maarifa na ujuzi katika utekelezaji na kutowajibika vya kutosha. Mipango iliyopo imelenga utekelezaji Dira ya Taifa ya Maendeleo na Mkakati wa Kupunguza Umaskini ambao kila Mkoa na Wilaya imeyaainisha katika mipango yao ya maendeleo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoeleweka Mkakati wa Kupunguza Umaskini umebainisha maeneo ya kipaumbele likiwemo suala la maji safi na salama, miundombinu, elimu, afya, kilimo, utawala bora na kadhalika. Pamoja na mipango mbalimbali ya maendeleo ambayo imekuwepo siku nyingi katika Mikoa yote, kumekuwa na ongezeko la fedha katika sekta za kipaumbele zinazotumwa moja kwa moja katika Wilaya zote kutoka Wizara ya Fedha ili kuboresha huduma mbalimbali za jamii ambazo zimeangaliwa kama sekta za kipaumbele katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini.

Ushirikishwaji wa jamii unasisitizwa hasa katika kuchangia nguvu, kumiliki na kutunza vyanzo vya maji na kutunza miradi ya maendeleo iliyopo kwenye maeneo yanayowazunguka. Aidha, ningependa kutoa ushauri kwa uongozi wa Mkoa wa Shinyanga wahakikishe kwamba umaskini unapunguzwa kwa kasi zaidi.

Ili wafanye hivyo ni lazima wawahamashe wananchi kuwekeza katika elimu ya msingi, elimu ya watu wazima, elimu ya sekondari na kuboresha makazi ya watu ili kuimarisha usambazaji wa huduma za maji safi na salama, kuboresha afya, barabara, miradi ya kuongeza pato na kujitosheleza kwa chakula. Maeneo mengine muhimu ni

kuimarisha sekta binafsi na kuvutia wawekezaji ili kusaidia ongezeko la ajira na mapato ya wananchi na kuimarisha kilimo na kukifanya cha kisasa na cha kibiashara zaidi ili kiweze kuboresha maisha ya wananchi.

MHE. PAUL N. MAKOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Mkoa huu wa Shinyanga huchimbwa madini kama vile almasi na dhahabu, Serikali kwa utaratibu ulionao ni kwamba madini haya yanapochimbwa huchukuliwa katika Mfuko wa Taifa bila kuacha *percent* fulani kwa ajili ya kusaidia maendeleo katika Mkoa huo, je, Serikali ina mpango gani wa kuacha *percent* fulani ili iweze kusaidia shughuli za maendeleo katika Mkoa huo na vile vile kuondoa suala la umaskini? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambaye nimekaa naye pale, ameniambia ya kwamba bwana hili swali la umaskini ni la madini, madini hivi, kwa hiyo, jiandae utaulizwa swali la nyongeza linalohusiana na madini. Nakupongea kwa kubashiri hivyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo niseme tu kwamba juzi tulikuwa na semina hapa ya madini na tumezungumza na nina uhakika Wizara husika ya Nishati na Madini, imechukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge ya kuona namna ya kuboresha maisha ya wananchi wanaozunguka migodi. Lakini zaidi ya hayo niseme pia ya kwamba Mheshimiwa Paul Makolo, anaelewa kwamba katika Wilaya zile ambazo zinazungukwa na migodi, upo utaratibu wa kuwataka wale wenye migodi kujihusisha na miradi ya kuiendeleza jamii inayozunguka migodi hiyo. Mheshimiwa Paul Makolo ni Mjumbe katika Bodi ya *Mwadui Diamonds*, nina hakika mawazo yake yatatumika kuboresha hili alilolisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda nimalizie kwa kusema kwamba, bado Serikali pamoja na kwamba mapato yanayotokana na madini yanatumika Kitaifa ikiwa ni pamoja na maeneo yale ambayo madini yanapatikana, tutaendelea na mjadala kuona ni jinsi gani wananchi wataboresha zaidi maisha yao kwa kutumia madini.

Na. 88

Uwezeshaji Wazee

MHE. ISSA MOHAMED SALIM (k.n.y MHE. JOB Y. NDUGAI) aliuliza:-

Kwa kuwa zipo sera na mipango mingi ya kuwawezesha kiuchumi wanawake na vijana; na kwa kuwa hadi sasa bado hakuna sera wala mipango ya wazi ya kuwawezesha wazee kiuchumi:-

Je, Serikali imeandaa fursa zipi za kuwawezesha wazee kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Wazee ni moja kati ya makundi yaliyoainishwa katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Mwanadamu anahesabika kuwa mzee anapofikisha umri wa miaka 60 na kuendelea. Katika umri huu wengi hushindwa kujipatia mahitaji yao ya lazima kutokana na kupungukiwa nguvu ya kufanya kazi. Hali hii humpunguzia mzee uwezo wa kupambana na umaskini, kwa hiyo, anakuwa mwepesi wa kuathirika na umaskini kuliko ilivyokuwa awali.

Pamoja na hali ya kupungukiwa na nguvu ya kufanya kazi, mchango wa wazee katika maendeleo ya Taifa ni kubwa kwani busara, hekima na uzoefu uliokomaa huonekana zaidi wakati wa izeeni. Serikali inatambua hilo na kuona umuhimu wa kuwa na mipango maalum ya kiuchumi ya kusaidia wazee kama ilivyo katika makundi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutekeleza hilo, Serikali imeandaa Sera ya Taifa ya Wazee kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wazee wakiwa wadau wakuu. Sera hii imechapishwa na imezinduliwa mwezi Oktoba, 2003 wakati wa Wiki ya Sera ya Kuondoa Umaskini.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mpango wa utekelezaji wa sera hiyo ambao upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Ni matarajio yetu kuwa mpango huo utakamilika mapema. Mikakati ya utekelezaji wa sera hiyo ya wazee imewekwa bayana jinsi ya kushughulikia kero za wazee katika suala zima la kuondoa umaskini. Serikali imeweka mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Uboreshaji huduma za afya kwa wazee, matunzo ya wazee, ushirikishwaji wa wadau katika kutoa huduma kwa wazee, kuunda Mfuko wa wazee kuchangia uzalishaji mali, hifadhi ya jamii, kuangalia mahitaji ya msingi ya maisha ya izeeni, uhamasishaji na uelimishaji, wanawake wazee na mila potofu ambazo zinadumaza mikakati ya wazee kujiondoa kwenye umaskini, wanawake wazee wenye ulemavu pia wameangaliwa katika sera hiyo. Sheria zisizolinda na kuendeleza wazee zimetazamwa, malezi na maandalizi ya vijana kuelekea izeeni na vyama vya kuhudumia wazee kama help age vinavyoshughulika na sera za wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi zinazokusudiwa kufanywa, Serikali imekuwa ikitekeleza sera mbalimbali ambazo zinalenga kuwasaidia wazee, mfano, ni Sera ya Afya ambayo imeeleza wazi kuwa matibabu kwa wazee ni bure. Pia

kila inapowezekana Serikali huboresha maslahi ya wastaafu kama vile pensheni na huduma nyinginezo. (*Makofi*)

MHE. ISSA MOHAMED SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri napenda kuuliza kwamba katika sera mojawapo ya kunyanyua uchumi wa wanawake na vijana ni mapato yanayochangishwa na Halmashauri kuchangia asilimia fulani ya makusanyo; na Halmashauri nyingi hazitoi mchango huo ipasavyo, je, Serikali inasema nini juu ya suala hilo? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Mkakati wa Kuondoa Umaskini Halmashauri za Wilaya ni sehemu muhimu sana katika kuchangia utekelezaji wa mkakati huo ambao unasisitiza zaidi katika kuondoa umaskini wa mapato, umaskini wa Mfukoni, lazima wananchi wenyewe waanze kuuchukia umaskini huo na ndipo Halmashauri, Mifuko ya kutoa mikopo na Mabenki itachangia juhud zao za kujiondolea umaskini.

Kwa hiyo, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, Halmashauri zimeelekezwa kutoa *percent* kumi ya mapato yao kwa ajili ya kuboresha na kutunisha Mfuko kwa kuondoa umaskini kwa upande wa vijana pamoja na akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitoe wito kwa Serikali za Mitaa kuzingatia maelekezo hayo na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni sehemu ya Halmashauri kwa maana ya kwamba ni Wajumbe wa *full council* wanapokutana, nawashauri Waheshimiwa Wabunge mhakikishe ya kwamba mnatoa *percent* hiyo kwenye vikao vyenu vinavyohusika kwenye Halmashauri zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka napenda nimalizie kwa kusema kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atakuwa anazingatia kwa maana ya kufuatilia maelekezo haya yanatekelezwa ipasavyo. (*Makofi*)

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wazee wetu ni muhimu sana; na kwa sababu ndio waliotuzaa na pia wako wengi wenyewe utaalami mzuri na uzoefu katika shughuli za kiuchumi na kimaendeleo, lakini wengi wanauawa kwa kudhaniwa ya kwamba ni wachawi kwa sababu eti wana macho mekundu; je, Serikali itakomesha lini mauaji hayo ili kuwafanya wazee wetu waishi kwa furaha? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kwa kuwa mstari wa mbele katika kutetea haki za wazee.

Kwenye majibu yangu nimesema wazee ni dawa, wazee ndio chimbuko la busara na pia wazee wasipokuwepo mambo hayaendi vizuri. Ndiyo maana katika wiki ya kutafakari masuala ya umaskini tuliyofanya hivi karibuni, tuliwashirikisha Chama cha Wazee kikiongozwa na Mwenyekiti wake, Brigedia Mstaafu, Mzee Mbena, ndiye anayeongoza harakati za kutetea shughuli za wazee na tunawatambua hivyo. Pia tuisahau kwamba wazee sio tu kwamba wanatumika kwa masuala mbalimbali lakini tuisahau nyumba ndogo nyingi ni za wazee kwa hiyo, wanatumika pia katika kuendeleza Taifa mpaka siku za mbele kabisa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kusema kwamba vitendo vya kuwaona wazee hawafai lazima vikemewe, hasa ile ya kusema ya kwamba wakiwa na macho mekundu kwamba wao ni wachawi, hapana, kuwa na macho mekundu ni sehemu tu ya kuzeeka, unapokuwa mzee, *nerves* zinatoa macho mekundu. Kwa hiyo, mimi napenda kukemea matendo hayo hasa yanayotokea katika maeneo ya Usukumani, mwache tabia hiyo!! (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na pia ameieleza sera ambayo tunaitegemea inakuja, sisi wazee wa miaka 60 tunategemea tutafanya vizuri kazi; je, Serikali ina mkakati gani kwa sasa kuhakikisha kuwa mzee anaendelea kupata haki yake ya heshima katika nchi hii, heshima imekufa pamoja na kuwa hata mnapogombea viti vya aina yoyote iwe ni Ubunge au Udiwani mzee anatengwa pembeni, Serikali inaingiliaje katika suala hili ili kumsaidia? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO): Mheshimiwa Naibu Spika, sera za Serikali zinazingatia umuhimu wa wazee. Nimesema wazee kwa mtazamo wetu sisi tunaanzia miaka 60 na ndiyo maana Mzee George Kahama, yuko humu na siyo Mbunge tu wa kuchaguliwa lakini ameteuliwa pia na Mheshimiwa Rais kwenye Baraza la Mawaziri.

Mkitazama humu kwa sehemu kubwa kwa kweli ninyi ni wazee humu ndani, tunawatambua hata Bunge linawatambua hata wananchi wanatambua umuhimu wa kuwachagua wazee ili watumie uzoefu wao kuja hapa Bungeni. Kwa hiyo, tutazingatia hilo na Serikali kama nilivyosema kwa sababu imepitisha Sera ya Wazee, ina mfumo mzuri kabisa wa uwakilishi wa wazee katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, tutazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuwaenzi wazee na ili kusudi tutumie busara zao. Pale kuna Mzee Chifu Abdallah Fundikira, ananitazama, wewe unafikiri angeingia humu bila kutambuliwa umuhimu wake? Kwa hiyo, wazee tutawaenzi kama Taifa linavyotutaka. (*Makofi*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI aliuliza:-

Kwa kuwa matumizi ya umeme yameonyesha uwezo mkubwa wa kupunguza matumizi mabaya ya Nishati Mbadala ya kuni na mkaa na kuokoa sehemu kubwa ya uharibifu wa mazingira:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliondoa tatizo hilo hapa nchini?
- (b) Sambamba na hilo, je, ni nchi gani wahisani na fedha kiasi gani kimeandaliwa na Serikali kupeleka umeme Namanyere, Nkasi pamoja na Vijiji vilivyoahidiwa vya Ntendo, Nkundi, Kipande, Kasu, Chala, Ntatumbia na kadhalika?
- (c) Je, ni kweli kuwa umeme utakuwa umefikishwa Wilayani Nkasi kabla au ifikapo mwaka 2005 kama Serikali ilivyoahidi Bungeni mwaka 2002?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ili kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na kukata miti kwa ajili ya matumizi ya kuni, Serikali ilianzisha na inatekeleza Sera ya kupeleka umeme Vijijini. Sera hiyo inalenga kwanza kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ambazo bado hazijapata umeme na baadaye yatafuata Majimbo/Miji midogo, Makao Makuu ya Tarafa na kadhalika.

(b) Mradi wa kupeleka umeme Wilayani Nkasi bado unatafutiwa fedha na Serikali kutoka kwa Wahisani mbalimbali.

(c) Ni lengo la Serikali kupeleka umeme Wilayani Nkasi ifikapo mwaka 2005. Hata hivyo, lengo hili litatimia tu kama fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mradi huu zitapatikana. Hivi sasa inakadirwa kuwa gharama za kupeleka umeme Wilayani Nkasi ni zaidi ya shilingi bilioni 2.6.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mzuri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi hapa nchini kuna Wilaya 16 ambazo hazina umeme ikiwa ni pamoja na Wilaya hiyo ya Nkasi ambayo iliahidiwa mwaka 2002 kwamba ifikapo mwaka 2005 itakuwa imekwishapata umeme; na kwa kuwa Sera ya CCM imetamka wazi kwamba ifikapo mwaka 2005 Wilaya zote ambazo hazina umeme zitakuwa zimekwishapata umeme; je, hili linawezekana wakati imebakia miaka miwili kuitekeleza sera yetu hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa kama alivyokiri kwamba kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira ipo Vijijini pamoja na maeneo mengine ya Miji mikubwa ambayo haina umeme; na hasa inasababishwa kwa kukata kuni kama alivyosema pamoja na mkaa; je, kwa nini Serikali isingekuwa imeweka kipaumbele kabisa wakati

inapopambana na suala hili la uharibifu wa mazingira, kuhakikisha ya kwamba umeme unapewa kipaumbele kwa wananchi wote ili mazingira yawefeze kuboreka kama vile nchi nyingi zilivyoboreka za Ulaya, Marekani na Asia ambazo zina umeme na wametunza mazingira yao vizuri? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko makini kabisa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi hususan katika eneo la upelekaji umeme Vijijini au kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Nilijibu hapa juzi tu kwamba katika Wilaya 16 ambazo hazina umeme, nne tayari mwaka huu zinapelekewa umeme. Nilisema pia kwamba hizi ambazo zimebaki, Serikali imetengeneza utaratibu wa kushughulikia maombi haya kwa ujumla na nilisema kwamba tutatoa taarifa ya maendeleo ya utaratibu huu kwenye Kamati ya Bunge husika.

Kwa hiyo, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali iko makini katika utekelezaji wa sera. Lakini kama ambavyo inafahamika, utekelezaji huu unategemea upatikanaji wa fedha ambazo ni nyingi katika suala la usambazaji wa umeme na nyingi katika hizo zinategemea ufadhili kutoka kwa wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, Serikali inaweka kipaumbele sana kama ambavyo nimeeleza awali juu ya upelekaji umeme Vijijini, tulikwishatangaza juu ya mradi kamambe wa utafiti wa kupeleka umeme Vijijini na pia tulikwishatangaza juu ya Mfuko maalum ambapo juzi wakati najibu swali Bungeni nilisema ya kwamba unatarajiwu kuanzishwa ifikapo mwishoni mwa mwaka kesho yaani Mfuko wa kupeleka umeme Vijijini na Taasisi maalum itakayoshughulikia kupeleka umeme Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo tumekuwa tukisema hapa Bungeni kwamba ni muhimu sana pia tutazame njia nyingine ambazo ni mbadala za kushughulikia nishati Vijijini ili kuondokana na tatizo la kukata kata miti ovyo na hususan *biogas*. Nimekuwa nikisema hapa mfano mzuri wa maeneo ambayo tayari *biogas* inatumika na Taasisi kama *CAMATEC* ambayo inashughulikia masuala ya usambazaji wa *biogas* na pia nikasema juu ya umuhimu wa Mikoa ambayo ina ng'ombe wengi kuhakikisha kwamba wanatumia nyenzo hii muhimu ya *biogas* katika kupata umeme ili kutunza mazingira. (*Makofî*)

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niulize swali la nyongeza. Kwa sababu suala hili la kupeleka umeme Vijijini ni suala muhimu kwa nchi nzima; na kwa sababu katika Mkoa wetu hasa tumepata umeme kutoka nchi ya jirani ya Zambia na umeme ule umepita katika Jimbo la Kalambo kuelekea Sumbawanga; na kuna Kijiji kimoja cha Matai ambapo inaweza kuwa ni *distribution centre* nzuri ya kusambaza umeme katika Jimbo la Kalambo, Jimbo la Kwela na Jimbo la Nkasi; je, Serikali inasema nini ili iweze kupeleka umeme Vijijini ikiwa ni pamoja na kuupeleka umeme huo katika Wilaya ya Nkasi kwa kupitia Kijiji cha Matai? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu imeunganishwa na nchi ya Zambia ki-umeme,

ni moja ya jitihada za kuunganisha nchi zote za *SADC* katika *grid* ya umeme ya pamoja kama ambavyo tunavyofanya na nchi za Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali, tunafahamu umuhimu wa kufikisha umeme kwenye Vijiji. Lakini upelekaji umeme huu ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge, unategemea sana upatikanaji wa fedha.

Mimi napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ambaye amekuwa wakati hadi wakati akifuatilia masuala haya Wilayani kwake, kwamba pale ambapo fedha zitapatikana *TANESCO* itatazama njia ambayo ni nyepesi zaidi ya kufikisha umeme kwenye maeneo ambayo ameyataja kama ikiwa hili alilolitaja la Matai ndiyo ambalo ni nafuu au kwa njia nyingine yoyote ili umeme ufile katika maeneo yale ambayo yanahitajika wafike.

Na. 90

Kupeleka Umeme Vijiji Vinavyozunguka Machimbo ya Dhahabu

MHE. KABUZI F. RWILOMBA aliuliza:-

Kwa kuwa umeme ni muhimu kwa wachimbaji wa madini kama dhahabu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Vijiji vya Nyakagwe, Ngula, Bukoli, Nyarugusu, Buziba, Rwamugasa na Katoro ili kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo na kuongeza kipato chao na cha Taifa kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upelekaji umeme maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, ameyataja unategemea mpango wa kupeleka umeme Ushirombo yaani Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe. Kwa kuwa maeneo ya Nyakagwe, Ngula, Bukoli, Nyarugusu, Buziba, Rwamugasa na Katoro yako jirani na Ushirombo, Mji Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, ni matarajio ya Serikali kuwa maeneo haya yatapelekewa umeme mara baada ya Mji wa Ushirombo kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kupeleka umeme Wilayani Bukombe pamoja na maeneo yote ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge ni karibu shilingi bilioni 14.

Serikali inatambua dhahiri umuhimu wa kusambaza umeme katika maeneo ya uzalishaji kama kwenye migodi ya dhahabu ili kuchochea maendeleo, lakini kikwazo kikubwa kama ambavyo nimesema awali ni ukosefu wa fedha za kugharamia miradi

hiyo. Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kusambaza umeme na itatekelezwa kwa awamu kulingana na uwezo wa upatikanaji wa fedha.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri maeneo hayo niliyoyataja yamezungukwa na migodi mikubwa miwili ya dhahabu ya Bulyanhulu na Geita; na migodi hiyo inachangia fedha nyingi sana katika kipato cha Serikali na Serikali imekwishatangaza kwamba migodi inaingiza fedha; je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba wananchi wanashangaa kuona kwamba wako jirani na fedha hizo lakini hawaoni faida yake?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wasishangae, migodi hii ambayo iko katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja kama ambavyo Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, amesema hapa inachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa na katika huduma za jamii. Lakini kwenye suala la kupeleka umeme, mgodi wa Kahama ndio ambao tunautegemea katika kuchangia suala zima la kupeleka umeme Ushirombo Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe baada ya wao kugharamia suala zima la kujenga kituo cha kupoozea umeme na kupeleka umeme kwenye maeneo yao ya wafanyakazi ya Bugarama na Ilogi.

Hivi karibuni tu Mgodi wa Kahama umefikia makubaliano na *TANESCO* katika kuhakikisha kwamba awamu hii ya kwanza ya kupeleka umeme hadi Ushirombo inatekelezwa kwa maana ya Kahama kutengeneza sehemu yao na *TANESCO* pia wamepewa kazi hiyo ya kujenga, Kahama watanunua vifaa na *TANESCO* watajenga mradi huu wa umeme hadi pale ili ukitoka pale basi iwezekane sasa kupeleka umeme katika awamu ya pili hadi Ushirombo na kumnufaisha Mheshimiwa Mbunge katika maeneo ambayo ameyataja.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, umeme ni kitu muhimu sana kwa kila mmoja na kwa sababu hivi karibuni Bwana Mrema wa *TLP* alisema kwamba amegundua umeme rahisi ambao unaweza kufika kwenye kila kijiji, je, si wakati muafaka kwa Serikali kutoa ufanuzi ili wananchi waelewe?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kama ilivytangazwa kwenye vyombo vya habari kwamba kuna mradi wa umeme kutoka kampuni inayoitwa *Ian* ya Marekani na mapendekezo ya mradi huu yaliletwa Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mapendekezo ya mradi huu hayako bayana kwamba ni chanzo kipi kitakachotumika kuzalisha umeme na jinsi ilivyoandikwa ni kama vile mtu anaandika kitabu au anataka kutoa *lecture* darasani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mapendekezo yale hayazingatii hali halisi ya Tanzania kwa sababu umeme wake utatumia *Direct Current*. Kwa uzoefu wa Tanzania na vifaa ambavyo tunavitumia sisi ambavyo vinaitwa *AlterNet Current (AC)* hii inaathari vifaa ambavyo vitatumia umeme huo kwa mfano redio, televisheni na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, bado hawajaweza kusema umeme huo haswa ni wa bei gani kwa mtumiaji. Uzoefu unaonyesha kwamba nyumba ya vyumba vitatu yenye *TV*, redio na kadhalika katika miradi ya upelekaji umeme vijijiini ambayo Serikali imekuwa ikiifanya uchambuzi inagharimu karibu shilingi milioni mbili na ndio maana hii imekuwa ni changamoto kubwa kwa Serikali kuona ni namna gani tunaweza kupunguza gharama hizi ili mwananchi wa kawaida aweze kufaidika na umeme huu wa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, hajaweza kutueleza huu mradi wenyewe ni wa mkopo au ni msaada tu. Hii ni muhimu kwa sababu usiposema hivyo itakuwa na athari katika bei ya umeme wenyewe kwa mtumiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kadri tunavyofahamu sisi hii kampuni ambayo Mheshimiwa Mrema ameileta inashughulika sana na uuzaaji wa vifaa, hawana uzoefu wa kutengeneza umeme. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, lazima niseme kwamba kwa kweli hakuna jipy a lililoletwa. Suala la usambazaji umeme hapa nchini kuititia mionzi ya jua na njia nyiningine ni masuala ambayo yanafahamika na Serikali, yanafanyiwa kazi na zipo taasisi mbalimbali hapa nchini ambazo zinafanya kazi hii ya kusambaza umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na nia nzuri ya mradi huu ulioletwa bado changamoto iko kwa aliyeleta mradi huu kuonyesha ni kwa kiasi gani mradi huu kwanza ni *viable* yaani unajitosheleza na kweli una manufaa kwa Taifa. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kutoa majibu ya nyongeza kwa maelezo mazuri sana aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kuhusu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalid Suru linalohusu yule Mmarekani waliywewita Mtaalam aliyekuja kuhusiana na suala hili la umeme unaoitwa Umeme Poa wa Mrema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja kati ya wale ambao nilikutana na huyu Linch. Alikuja Ofisini kwetu katika Ofisi ya Makamu wa Rais na tulimpokea kwa sababu Umoja wa Mataifa umezungumzia suala la kuendeleza teknolojia ya vyanzo vyia umeme mbadala.

Katika mazungumzo, la kwanza ni kwamba ingawa imetangazwa kuwa ni mtaalam, lakini ile kadi yake ya kujitambulisha (*business card*) yeche ni Afisa Uhustiano wa Kisiasa na Kimataifa katika Kampuni yao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maongezi baada ya kueleza kwamba lengo kuu linashabihiana na uamuzi wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu kutafuta teknolojia ya umeme mbadala alichokisema pale ofisini kwangu ni kwamba baada ya kuelewa hilo anaondoka kurudi Marekani aende Benki ya Dunia na vyombo vingine vya fedha ili kampuni yake ipate mkopo wa kutekeleza mradi wanaoufikiria. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishahusisha mkopo kutoka Benki ya Dunia na vyombo vingine vya fedha vya Kimataifa, sitarajii hata kidogo kwamba umeme huo unaweza kupatikana kwa kile kinachoitwa bei poa, hata kidogo. (*Makofii*)

Na. 91

Mtambo wa Simu za Kisasa Kyela

MHE. JOHN L. MWAKIPESILE aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ni msingi wa maendeleo ya uchumi, siasa na jamii mahali popote na kwa kuwa kwa kuzingatia msingi huo wananchi wa Kyela wanaishukuru Serikali kwa kujenga mtambo wa simu wa kisasa mjini Kyela:-

(a) Je, mtambo huo una uwezo wa kuhudumia wateja wangapi kwa wakati mmoja na ni wateja wangapi wameshafungiwa simu Kyela?

(b) Je, ni njia ngapi za simu za mtambo huo zimehifadhiwa na kufungwa katika mji midogo ya Kasumulu - Boda na Ipinda?

(c) Je, ni lini simu zitafungwa katika Kituo cha *Matema Beach* ili wananchi, watalii na Hospitali ya Matema waweze kupata huduma hiyo muhimu?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa John Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mtambo wa kisasa wa Kyela aina ya *GX 5000* una uwezo wa kuwashudumia jumla ya wateja 700. Mpaka mwishoni mwa mwezi Septemba, 2003 jumla ya wateja 523 walikuwa wanafaidika na huduma ya mtambo huo na bado wateja 177 wanahitajika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo huo pia una uwezo wa kuhudumia wateja wa mbali (*Out of Area*) na mpaka sasa ni mteja mmoja wa Ipinda anahudumiwa na mtambo wa Kyela lakini hakuna mteja wa kutoka Kasumulu - Boda aliyeomba. Kwa vile Kasumulu - Boda iko mbali na mtambo wa Kyela, wateja wa eneo hilo wanahudumiwa vizuri kwa simu za mkononi za *Celtel*. Kwa sasa kama yupo mteja anayetaka kutumia simu za *land line* kwa utaratibu wa *Out of Area* anashauriwa kupeleka maombi kwa Meneja Biashara wa *TTCL* Mkoa wa Mbeya.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa uboreshaji wa mawasiliano ya simu vijijini, kijiji cha Matema kimepangiwa kupatiwa simu za vibandani ifikapo mwishoni mwa mwaka 2004. Kama kituo cha *Matema Beach* kitahitaji huduma haraka, basi tunawaomba wawasiliane na Meneja wa Mkoa anayehusika na biashara ili uwezekano wa kupatiwa huduma ya mbali kutoka mtambo wa Kyela ichunguzwe na ikiwezekana wapatiwe huduma hiyo.

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mipango mikubwa kabisa ya kueneza mtandao wa simu katika nchi nzima je, Wilaya ya Mafia ni lini itaweza kupata simu za uhakika za mtambo wa *digital* au kuona uwezekano Wilaya yetu ya Mafia kupatiwa simu za mkononi za *Celtel* au shirika lolote lile la simu za mkononi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, swali ni jipya lakini kama una jibu unaweza kujibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoahidiana na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kwamba Mafia itapatiwa mtambo wa *digital*. Napenda nimkumbushe tena kwamba bado ahadi yetu ipo na itatekelezwa.

Na. 92

Mashua Iliyozama Baharini Januari, 2003

MHE. NJELU E.M. KASAKA aliuliza:-

Kwa kuwa imetangazwa kwenye vyombo vyetu vya habari kwamba ipo mashua iliyozama Baharini kati ya Tanga na Kisiwa cha Pemba mwanzoni mwa mwezi Januari, 2003; na kwa kuwa mashua hiyo ilikuwa imebeba abiria wapatao 40 lakini hazikusikika hatua zozote za Serikali zilizochukuliwa ili kuokoa watu hao:-

(a) Je, Serikali inaweza kuueleza umma wa Tanzania kwamba ilichukua hatua gani za uokoaji?

(b) Kwa kuwa ajali za vyombo vya usafiri majini hutokea mara kwa mara katika Pwani ya Bahari ya Hindi na katika Ziwa Victoria; je, Serikali ina utaratibu gani wa kudumu wa uokoaji?

(c) Je, Serikali inacho kikosi cha Walinzi wa Mwambao yaani *Coast Guard*?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ajali ya mashua iitwayo Tunashukuru ilitokea siku ya tarehe 31 Desemba, 2002 kati ya Bahari ya Tanga na Pemba karibu na Mwambao wa Tanga. Mashua hiyo ilikuwa ikitokea Bandari ya Tanga kuelekea Gando Pemba. Inasemekana ilikuwa imebeba magunia themanini ya mbatata pamoja na abiria 38. Raia wawili tu waliokolewa na mzigo wote kupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hicho hakikuwahi kufanyiwa ukaguzi kwa sababu hakikuwa na usajili wowote, kilikuwa kikitumia Bandari zisizo rasmi za Pemba. Aidha, chombo hicho hakikuwa na kifaa chochote cha mawasiliano wala cha uokoaji kwani hakikuwa chombo cha abiria.

Serikali haikuwahi kuchukua hatua yoyote ya uokoaji kwa sababu kama nilivyokwishaeleza hapo awali hakukuwa na mawasiliano ya aina yoyote kati ya chombo hicho na Bandari zinazotambulika kama zile za Mkoani, Wete, Wesha na Tanga.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ziwa Victoria utaratibu ufuatao hutumika:-

Kampuni ya Huduma za Meli kuititia Ofisi yake ya Mawasiliano (*Control Room*) huwa hewani saa 24 kwa siku zote yaani Jumatatu hadi Jumapili pamoja na siku za sikuu. Moja ya shughuli zake ni kuwasiliana na vyombo vyote vinavyosafiri majini ambavyo vina mitambo ya mawasiliano ya *radio*. Mara taarifa zinapowafikia *Controllers* kuhusu kutokea kwa ajali taarifa husambazwa kwa wahusika wote pamoja na *mobilization* ya meli kwenda kwenye eneo la ajali ili kusaidia uokoaji.

Mara zote meli ndogo (*tugs*) huwa *standby* kwa ajili ya tatizo lolote likitokea. Lakini ni wenye meli au vyombo vyenye mawasiliano tu ambao wanaweza kutuma habari mara moja kwa kutaja walipo na msaada wanaouhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunayo Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia masuala ya uokoaji ikiwashirikisha wafuatao:-

Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi, *Disaster Management Department, Tanzania Civil Aviation Authority, Tanzania Harbours Authority, Tanzania Railway Corporation, Marine Services* na Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Pia makubaliano ya kuanzisha *Search and Rescue* kwa ushirikiano kati ya Tanzania, Kenya na *Syckelles* yamekamilika; na mkataba unafanyiwa uchambuzi wa kitaalam na kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuititia Kitengo chake cha Usafiri wa Majini kinaendelea kufanya ukaguzi wa vyombo vidogo vidogo vyta usafiri majini na kuwaelimisha wamiliki umuhimu wa kuwa na vyombo imara, namna ya kujiokoa na umuhimu wa mawasiliano katika vyombo vyao. Aidha, elimu kwa *TV* inatolewa kwenye meli za *Marine Services Company Limited* na namna ya kujiokoa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina *Coast Guard* lakini ina *Police Marine* na Jeshi la Majini. Mojawapo ya majukumu yao ni kufanya doria mwambao wa Tanzania.

MHE. NJELU E.M. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa mara nyingi vyombo vyaa majini vinapozama inasemekana ni kutokana na kujaza abiria wengi sana, hivi hakuna utaratibu kwenye Bandari zetu wa kuvidhibiti vyombo hivyo ili visijaze kupita kiasi?

(ii) Aliposema kwamba ile mashua haikuwa imeandikiswa iliingia tu Baharini na ilikuwa na idadi kubwa ya abiria, hivi ndio kusema Serikali inaweza kuruhusu chombo chochote kikawa kinafanya kazi ya kubeba watu katika Bahari bila idhini ya Serikali na walijuaje idadi ya watu kama chombo hicho kilikuwa hakijulikani?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuhakiki abiria wote wanaoingia katika meli upo na umewekwa katika Bandari zetu na napenda niwakumbushe wanaohusika kwamba utaratibu ule wanapaswa kuufuata. Kama Bandari ya Dar es Salaam kila wiki sisi tunayo ripoti kamili ya wanaopakiwa katika meli, idadi na uwezo wa meli. Nasisitiza wenzangu walioko Mwanza na sehemu nyingine waendelee kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliokolewa watu wawili na taarifa tulizipata kutoka kwao ambaa walibahatika kuokolewa.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Suala la msingi linabaki pale pale kwamba hali ya ulinzi hajakaa sawasawa. Sasa hivi kufuatana na shughuli za uvuvi, usafiri majini umepanuka sana na hali hii ya hatari inaonekana na hatujaona patrol au ulinzi kwenye maji kwa ajili ya kusaidia wasafiri majini, inaonekana Serikali iko nyuma. Je, katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa Serikali inafanya nini kuokoa na kusaidia watu katika suala zima la usafiri majini?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Kazi kwamba ni juu yetu sisi Waheshimiwa Wabunge kuwakumbusha wenzetu ambaa wanatumia huduma za Baharini waache kutumia vyombo visivyohusika katika kubeba abiria. Ukitizama ajali nyingi zinazotokea ni zile ambazo mitumwi ya kuvulia inafanya ndio vyombo vyaa kusafirishia abiria kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, havina usalama wowote, havina vifaa vyaa kuokolea havina hata maboya. Naomba nisisitize kwamba wakati Serikali ikifanya juhudhi zake kwa upande mwingine na sisi wananchi tutimize wajibu wetu.

Matumizi ya Magari ya Viongozi Wakuu

MHE. LEKULE M. LAIZER (k.n.y. MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN) aliliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi maskini ambayo sehemu kubwa ya Bajeti yake hutegemea misaada na mikopo kutoka nje; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imejitahidi sana kukusanya madeni na kusimamia matumizi kiasi cha kurudisha hadhi ya Serikali kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma:-

(a) Je, kuna sababu gani ya kila Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkoo, Wakurugenzi na kadhalika kuwa na gari la Serikali aina ya *Toyota Land Cruiser VX* na *GX* wakati ambapo sehemu kubwa ya kazi zao za kila siku ziko mijini ambako kuna barabara za lami?

(b) Je, isingekuwa busara na unafuu kutumia magari ya aina hiyo yaani *Toyota Land Cruiser VX* na *GX* kwa safari tu za vijijini ambako barabara ni mbaya na badala yake kuwe na magari mengine madogo ya gharama ndogo yatakayotumika kwa matumizi ya kawaida ya kwenda na kurudi ofisini kwa sababu barabara za mijini ni nzuri?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mathew Taki Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zinazofanya kila Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkoo kuwa na gari la Serikali aina ya *Four Wheel Drive Station Wagon* ni kama ifuatavyo:-

(i) Magari hayo hununuliwa kulingana na mahitaji ya Wizara husika kama kukagua miradi na kadhalika na Bajeti ya ununuzi wa magari hayo hupitishwa na Bunge.

(ii) Magari hayo hutumika mijini pamoja na safari za vijijini.

(iii) Magari hayo yana uwezo wa kuhimili barabara zetu pamoja na kusafiri muda mrefu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuwapatia viongozi hao magari madogo na ya gharama ndogo kwa matumizi ya kawaida mijini penye barabara safi za lami, kutaongeza gharama kwa Serikali kwa kuwa itabidi kila mmoja awe na magari mawili ili kurahisisha mpangilio wa kazi zao gari moja la kutumia katika barabara nzuri za lami na gari la pili kutumia katika sehemu mbaya ambazo huhitaji gari la *Four Wheel Drive*.

Aidha, si miji yote Tanzania yenyewe barabara nzuri za lami na hata zinapopatikana ni kilometra chache na hivyo zitawafanya viongozi wetu kutotembelea maeneo mengine ambayo yana barabara mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali imeona ni busara kununua gari aina moja ambalo ni imara linaloweza kutumika mijini pamoja na safari za vijijini ili kupunguza gharama.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, fedha walizotumia kununua magari haya aliyoyataja ni fedha za wafadhili au ni fedha zinazotokana na kodi za wananchi?

(ii) Kwa kuwa magari haya ya viongozi Mawaziri, Naibu Waziri, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu, ma-*DC* na wengine je, isingefaa na maeneo ya vijijini kama vile Vituo vya Polisi, Vituo vya Afya ambavyo havina magari wanunuliwe magari ili wananchi waweze kuhudumiwa vizuri kwa mfano sehemu za mipakani kama Loliondo na Longido?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotumika kununulia magari haya ni za aina mbili zipo fedha za wafadhili kwa miradi inayofadhiliwa kwa mfano miradi ya afya na kadhalika lakini zipo pia fedha ambazo zimenunu magari haya kutokana na bajeti tunayoipitisha katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, amesema Vituo vya Polisi, Vituo vya Afya navyo vina haki ya kupata magari hayo, hili nakubaliana nalo na ndio maana katika Vituo vingi vya Polisi vina magari aina ya *Four Wheel Drive* ambayo ni *Land Rover* na Vituo vingi vya Afya chini ya ufadhili wa *DANIDA* vimeweza kupata magari ya *Four Wheel Drive* ambayo ni *Hardtop Land Cruiser* na haya yote yanalingana na yanaendana na uwezo wa Serikali katika kuhakikisha yanafanyika.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa sio tu viongozi wa Tanzania bali na wananchi wengi tu wa kawaida wana matumizi makubwa sana ya magari ya *Four Wheel Drive* ambayo kawaida yanajulikana kama *SUVs* na kwa kuwa uchakavu wa magari haya unasababishwa tu na jambo la kawaida tunalolijua ambalo ni ubaya wa barabara katika nchi hii, je, Waziri atanihakikishia kwamba ni lini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itajenga kwa kiwango cha lami barabara inayotoka Minjingu - Babati - Singida - Tabora na ile inayotoka Singinda - Mtinko - Hospitali ya Haidom?

NAIBU SPIKA: Ni swali jipya, lakini Mheshimiwa Waziri majibu. (*Kicheko*)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba matumizi ya *Four Wheel Drive* yanaendana na hali halisi ya barabara zetu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwamba Serikali ina mipango mingi tu ya kutengeneza barabara nchini kama zilivyoainishwa kwenye bajeti ya mwaka 2003/2004 ambayo bahati nzuri Mheshimiwa Nyalandu ameipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Minjingu - Babati - Dodoma - Iringa - Tabora - Kigoma na barabara nyingine ambazo amezitaja, kwa barabara ya Minjingu - Iringa katika mukutano wa wiki iliyopita ambapo ulihusisha nchi 10 za *NEPAD* uliofanyika Nairobi barabara hii imewekwa kwenye *priority* namba moja ya kutengenezwa katika kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika bajeti ya barabara za *East Africa Cooperation* vile vile imewekwa na Serikali bado inaendelea na mipango yake ya kuhakikisha kwamba fedha zitakazopatikana za ndani pamoja na za wafadhili ziweze kutengeneza barabara hizi kwa kiwango cha lami na hivyo kupunguza gharama kubwa za matumizi ya magari ya *Four Wheel Drive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwamba Serikali ina mipango mingi ya kutengeneza barabara zote kwa kiwango cha lami na hasa zile kilomita 35,000 ambazo zina-cover nchi nzima yenye ukubwa wa kilomita 945,000. Kwa hiyo, Serikali italizingatia hili katika kupunguza matumizi yake.

Na. 94

Kampeni za Usalama Barabarani

MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y. MHE. DR. JAMES A. MSEKELA
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina desturi nzuri ya kuendesha kampeni za usalama barabarani kuitia Juma la Usalama Barabarani kila mwaka ambapo walengwa huwa ni wote watumiao barabara wakiwemo waenda kwa miguu, wapanda balskeli, abiria umadhubuti na usalama wa vyombo vyenyewe (Magari, pikipiki, matingatinga, vivuko na kadhalika); na kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa msisitizo wa kampeni hizo aghalabu huwa ni kwa magari tu hususani ukaguzi wa appearance tu za magari na wala si umadhubuti na usalama wake:-

- (a) Je, hali hii ya kampeni zisizo kamili itaendelea hivyo hadi lini?
- (b) Kwa kuwa utaratibu wa kampeni hizo hautoshi hata kwa ukaguzi tu wa magari na vyombo vingine vya barabarani nchini, je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza zoezi hilo la ukaguzi wa vyombo vyote ili vitumiapo barabara viwe na stahili (cheti) ambacho kwa urahisi wa ufuutiliaji wa *Traffic Police* kitabandikwa kwenye kibao cha usajili kwa kipindi maalum kama miezi 12?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kuwa kampeni za usalama barabarani zinazofanyika kila mwaka kupitia maadhisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani zinahusu magari pekee hususani ukaguzi wa *appearance* tu za magari na wala si umadhubuti na usalama wake kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Ukweli ni kwamba kampeni hizo ni kamili na huelimisha watumiaji wote wa barabara ikiwa ni pamoja na madreva, watembea kwa miguu, wasukuma mikokoteni, wapanda balskeli, wapanda pikipiki na abiria ambao huelimishwa kutii na kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani na hivyo kuepusha ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutohana na Serikali kuelewa umuhimu wa maadhisho haya, uzinduzi wake Kitaifa hufanywa na viongozi wa ngazi ya juu Serikalini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba vyombo vyote vya usafiri barabarani vinakaguliwa, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi inakusudia kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Magari (*Motor Vehicle Inspection Act*).

Chini ya sheria hii iwapo itapitishwa magari yote yatatakiwa yakaguliwe katika vituo vinavyotambuliwa na Serikali kila mwaka. Baada ya ukaguzi magari mazima yatapewa *sticker* na ndiyo pekee yataruhusiwa na kisheria kutembea barabarani. Chini ya sheria hiyo vile vile kazi ya *Police Traffic* itakuwa kusimamia utekelezaji wa sheria hii na sio kukagua magari kama hali ilivyo sasa.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza majibu ya Naibu Waziri sio kweli kwa sababu kampeni anazozisema zimekuwa za maadhisho na maadhisho maana yake ni sherehe.

Je, kampeni hizo ili ziwe kamili isingestahili zijae kufundisha sheria hasa kwa watumiaji wa magari, waendeshaji balskeli na waendao kwa miguu wakaelewa sheria ili kuepusha ajali hasa ambapo sasa hivi zimezidi sana nchini kwa sababu wengi hawafuati sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa amesema sheria hiyo itakuja hivi karibuni kupitia Wizara ya Ujenzi haoni jinsi ya kudhibiti ajali mbalimbali zinazotokea ingekuwa na nidhamu zaidi hasa ya Maaskari kwa sababu wengi wa Maaskari hujaa barabarani kwa ajili ya kungoja mabasi na malori kuliko kutoa elimu hasa kwa watumiaji wa magari?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, yale maadhimisho ambayo hufanywa kwa mwaka mara moja huwa ni kilele tu cha shughuli mbalimbali ambazo hufanyika mwaka mzima ambazo katika kila Mkao iko Kamati ya Usalama Barabarani katika kila Mkao na sasa hivi Kamati hizi zinateremka katika kila Wilaya ambapo Kamati hizi kwa kushirikiana na vyombo vya Serikali kila siku kazi yake ni kusimamia mambo ya usalama barabarani hususan utoaji wa elimu ambaeo ndiyo jambo kubwa sana, kutoa elimu kwa watumiaji wote, kuwaelimisha kuhusu sheria na taratibu mbalimbali za barabarani kwa sababu ajali nyingi kusema kweli ni uzembe tu wa kupuuza kanuni na sheria za barabarani.

Unakuta kuna ukungu mtu haoni mbele, mita mia haoni, anaona mita mbili anataka *ku-over take*, kwenye kona mtu anataka *ku-over take*. Kwa hiyo, haya ni masuala ambayo ni ya kuelimisha na tumeshaunda sasa Kamati za Mkao, Kamati za Wilaya ili zifanye kazi hii. Vile vile naomba vyombo vya habari, redio, magazeti na *religion* visaidie. Tatizo letu kubwa kabisa ni la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sheria ambayo inakuja, sheria inapitia Wizara ya Ujenzi kwa sababu ndiyo wataalam wa masuala ya barabarani, ndiyo wataalam wa masuala ya usalama barabara, wanatengeneza barabara na alama za barabarani na kadhalika. Sisi kwa upande wa Polisi kusema kweli kazi kubwa ni kutekeleza sheria ambazo zinatungwa na Wizara mbalimbali pamoja na hii itakayotungwa ya ukaguzi wa magari. (*Makofî*)

Na. 95

Ahadi ya Kuchimba Visima katika Kata

MHE. EDSON M. HALINGA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa ahadi nyingi huko nyuma za kuchimba visima Kata za Isansa, Msia Nambingo na Itaka na kwa kuwa ahadi hizo bado mpaka sasa hazijatimizwa:-

(a) Je, Serikali itamshirikisha vipi mfadhili wa maji toka Ujerumanî ili aweze kutoa msaada na utaalam wake?

(b) Kwa kuwa Wilaya ina miinuko (*undulating land*) na hivyo uwezekano wa kujenga mabwawa kwa kuzuia mito midogo midogo ungewezesha upatikanaji wa maji, je, Serikali iko tayari kufanya uchunguzi huo na kusaidia?

(c) Kwa kuwa wananchi Wilayani wamejithadi sana kujenga mabwawa hayo mengi, je, Serikali iko tayari kumleta mtaalam wa mabwawa ili asaidie kuwaelimisha wananchi wa Mbozi ili mabwawa hayo yawe ya kudumu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Edson Mbeyale Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mnamo mwaka 2001, Serikali ilitekeleza mradi wa uchimbaji wa visima katika Kata za Isansa, Myovisi na Igamba kwa kutumia Mfuko wa *STABEX* uliosimamiwa na kitengo cha *Coffee Management Unit*. Matokeo ya mpango huo yalijumuisha uchimbaji wa visima 18 vya kina cha kati na ufungaji wa pampu za mkono ambapo visima 16 vilichimbwa Isanga, Myovisi kimoja na Igamba kimoja.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari, 2003, Serikali za Tanzania na Ujerumani zilijadiliana kuhusu uwezekano wa kugharamia miradi ya maji Vijijini katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Iringa. Kutokana na kikao hicho, Serikali ya Ujerumani ilikubali kugharamia maandalizi ya programu ya maji Vijijini katika Mikoa hiyo mitatu ili iweze kujadiliwa tena kwenye mazungumzo yatakayofanyika mwaka kesho. Kwa hivi sasa Serikali ya Ujerumani inaendelea kufadhili ile miradi ya maji inayoendelea na haitatenga fedha kwa ajili ya programu ya maji Vijijini kwa Mikoa mingine.

Pamoja na maandalizi hayo yanayotarajiwa kufanywa, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa katika mradi wa Huduma ya Maji Vijijini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Wilaya ya Mbozi ni mojawapo ya Wilaya 38 ambazo zimeongezwa kwenye mradi huo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya maeneo katika Wilaya ya Mbozi yanaweza kutumia teknolojia ya mabwawa na malambo. Kwa kutambua hilo, Serikali imetenga katika Bajeti ya mwaka 2003 kwa Wilaya ya Mbozi kiasi cha shilingi 1,500,000 kwa ajili ya uchunguzi na upimaji wa vyanzo vya maji na shilingi 2,000,0000 kwa ajili ya kufanya uchunguzi kwa maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa madogo madogo. Katika mwaka 2003 kazi hizi zitafanyika katika Kata mbalimbali za Wilaya hiyo zikiwemo Msia na Itaka.

Aidha, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 4,000,000 kusaidia ukamilishaji wa ujenzi na ukarabati wa mabwawa madogo madogo kwa kushirikiana na wananchi. Lengo ni kuyafikia maeneo yote yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa ya namna hiyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ipo tayari kutoa msaada wa kiutaalam pindi utakapohitajika kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kufanya uchunguzi ili kubaini maeneo mazuri yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa na kutoa elimu na ushauri.

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Naibu Waziri. Katika ahadi hizi nimekuwa nikimwomba afike aone kweli kama visima vya mwaka 2001 vimechimbwa au sivyo, lakini hajafika mpaka leo. Nataka

nimhakikishie kwamba visima hivyo anavyosema vilichimbwa mwaka 2001 havipo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, atakuwa tayari kuthibitisha hii ahadi aliyoisema kwamba kweli kutakuwa na msaada huo anaousema kwa sababu imekuwa ni tabia ya kuahidi lakini hakuna linalofanyika? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kawaida taratibu za utawala bora kwa sasa hivi zinazingatia matumizi ya Halmashauri za Wilaya na hivyo taarifa nyingi tunazopipata zinatoka kwenye idara husika kama Idara ya Maji katika suala hili kulingana na taarifa hizo tunakuja kutoa taarifa au majibu kwa Waheshimiwa kama nilivyofanya.

Hivyo basi, kama visima anavyovieleza Mheshimiwa Edson Halinga, havijachimbwa badala ya kuja kutupa taarifa tukiwa ndani ya Bunge itakuwa ni vizuri sana tuletewe taarifa rasmi ili tuone kama na sisi tumepewa taarifa ya uwongo ili hatua zinazohusika ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la miradi mbalimbali katika Wilaya ya Mbozi, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la miradi hiyo linahitaji fedha na kutohana na jitihada hizo ambazo anazifanya Mheshimiwa Mbunge ndio maana Serikali imeiweka Wilaya ya Mbozi katika mradi wa Benki ya Dunia ili ufaidike kutekeleza mipango ambayo Wilaya yenyewe ya Mbozi itakuwa imeipanga na hivyo kusaidia wananchi ikiwa pamoja na Mheshimiwa Mbunge.

Na. 96

Kero Kubwa ya Maji Nchini

MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO (k.n.y. MHE. JOEL N. BENDER)
aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la uhaba wa maji Mijini na Vijijini ni kero sugu katika nchi yetu hadi sasa na kwa kuwa maeneo kama Mji wa Korogwe, Magoma, Hale, Mgambo, Kitifu, Ngomeni - Hale, Kwasemagube, Kijango, Magunga Cheke, Kerenge Kibaoni, Kalalani na kadhalika kumekuwa na kero kubwa sana ya maji na tatizo hilo tunaweza kulifananisha na donda ndugu na kwa kuwa Serikali imeweza kutafuta gharama zinazohitajika ili kukamilisha miradi yote ya maji nchini ambayo kama ikitekelezwa ipasavyo itakuwa imeondoka na tatizo hilo na kwa kuwa katika tathmini hiyo ya Serikali imebainika kuwa kiasi cha Sh.bilioni 47 kitahitajika kwa kazi hiyo:-

(a) Kwa kuwa kupanga ni kuchagua; na kwa kuwa Maji ni Uhuru, je, Serikali haioni kwamba ni busara kutenga kiasi hicho cha fedha shilingi bilioni 47 katika kipindi cha miezi miwili ili kero hiyo ikamalizwa hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali inakusanya mapato yake ya zaidi ya sh. bilioni 110?

(b) Kwa kuwa maeneo niliyoyataja yana kero kubwa sana ya maji ya muda mrefu na tayari Vijiji na Kamati za Maji zimeshafungua *Accounts* za maji kumalizia miradi ya maji, je, Serikali inawasaidiaje wananchi wa vijiji hivyo katika kuhakikisha wanapata maji ili kuondokana na kero hiyo ya muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Serikali ilifanya tathmini ya miradi ya maji ambayo haijamilika au haitoi huduma kutokana na uharibifu mkubwa na kubaini kuwa kiasi cha shilingi bilioni 47 zinatakiwa ili kukamilisha na kukarabati miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kukarabati na kukamilisha miradi hiyo kuitia katika bajeti ya kila mwaka. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi 855,776,000/= kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa kuwa Serikali inagharamia sekta mbalimbali hapa nchini, ukamilishaji na ukarabati wa miradi ya maji utafanyika kwa awamu. Hivyo, haitawezekana kutenga shilingi bilioni 47 zote katika kipindi cha miezi miwili kwa kazi ya kukarabati miradi ya maji pekee kwa vile kuna kazi nyingine ambazo ni muhimu katika Taifa hili.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa maeneo ya Mji wa Korogwe, Magoma, Hale, Mgambo, Kitifu, Ngomeni - Hale, Kijango, Magunga Cheke, Kerenge Kibaoni na Kalalani yana matatizo ya kupata huduma ya maji ya uhakika.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa maeneo haya akiwemo na Mheshimiwa Mbunge kwa kuunda Kamati za Maji na kufungua akaunti za maji. Kwa kutambua kero ya maji inayowasumbua wananchi wa Wilaya ya Korogwe, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Serikali ilitenga shilingi milioni 51 kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji kwenye Mji wa Korogwe, aidha shilingi milioni nne zilitengwa kwa ajili ya upimaji na uchunguzi wa maji Vijijini.

Vilevile, kuanzia mwaka 2004/2005, Wilaya ya Korogwe itakuwa miongoni mwa Wilaya 38 ambazo zitaongezeka katika Mradi wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huu utaweza kuondoa kero ya maji katika Wilaya nzima ya Korogwe ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Mheshimiwa Mbunge akishirikiana na viongozi wenzake kama anavyofanya kila mara wahakikishe mpango wa maji yanayotokana na mradi huu wa benki ya dunia unashirikisha Vijiji hivyo ili vipunguze matatizo yaliyopo katika upatikanaji wa maji.

MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Katika swalii la kwanza la Mheshimiwa Joel Bendera, alisisitiza suala la kupanga ni kuchagua na kwamba maji ni uhai, je, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba katika mpango huu unaotazamiwa kutekelezwa katika Wilaya ya Korogwe kipaumbele kitatolewa katika Mji mdogo wa Korogwe ambao ni Mji wa barabarani na unahuishisha watu wengi sana na mara kwa mara panatokea magonjwa ya milipuko?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa katika mpango wa kupeleka maji kwenye Kijiji au eneo la Magoma katika Jimbo la Korogwe Mashariki mradi huo umehusisha Kijiji cha Turiani cha Jimbo la Bumbuli, je, Serikali itakubali kupokea shukrani zangu na za wananchi wa Kijiji hicho cha Turiani kwa kuwahusisha katika mpango huu? (*Makofisi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii tuliyonayo kama nilivyoeleza katika jibu la msingi Mji wa Korogwe tunaangalia uwezekano wa kuingiza katika bomba kuu la *Handeni Trank Mail* ambayo ni kama kilomita 12 kutoka kwenye Kituo cha Kusafisha Maji cha Tabora.

Kwa hiyo, utaratibu huo utakapokamilika matatizo ya maji ya Mji wa Korogwe yatakuwa yamepungua sana na ninapenda kupokea shukrani alizozitoa Mheshimiwa Mbunge.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tatizo la uhaba wa maji la Korogwe linafanana kabisa na lile lililopo katika Wilaya ya Kilolo katika Vijiji vya Ilula, Vitono, Isagwa, Luhambwi na Mahenge na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alishapita sehemu ya Ilula na kutuahidi kutusaidia. Je, Serikali itakuwa tayari kusaidiana na wafadhili (Walutherani) ambao wapo tayari kutuchimbia visima?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilipita katika Kijiji cha Ilula na kwa ushirikiano mkubwa wa Mheshimiwa Mbunge tuliahidiana kwamba wananchi waanze kutelekeza yale ambayo tulikubaliana yaani waanze ujenzi wa matenki ya maji ili kuboresha huduma za maji za Kijiji cha Ilula ambacho kinapata maji yake ya mtiririko kutoka milima iliyo jirani. Taarifa nilizonazo ni kwamba wananchi wamekubali na wapo mbioni kutekeleza hilo, mara litakapokamilika nitamwomba Mheshimiwa Mbunge atuletee taarifa ili tuone Serikali tunatoa mchango tuliowaahidi ili kutekeleza hilo ambalo sote tulikubaliana.

MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA aliuliza:-

Kwa kuwa hospitali ya Mtakatifu Gaspar ya Itigi ina miundombinu na mazingira ya kufaa kuwa Hospitali ya Rufaa:-

Je, Serikali kwa kushirikiana na uongozi wa Hospitali hiyo iko tayari kuifanya kuwa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kati kwa kuwapatia Madaktari Mabingwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni, napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mtakatifu Gaspar ina vitanda 100 na Madaktari wawili na haina Daktari Bingwa. Hospitali hii inamiliikiwa na Shirika la Damu Takatifu ya Yesu chini ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania. Hospitali hii ilianza kazi rasmi mwaka 1986 na inapata ruzuku ya vitanda na mishahara toka Serikalini kupitia Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika ili hospitali iweze kuwa ya Rufaa lazima iwe na vigezo vifuatavyo:-

(i) Lazima iwe na fani za ubingwa katika maeneo ya magonjwa ya ndani, watoto, magonjwa ya kinamama na uzazi, upasuaji, macho, magonjwa ya akili, magonjwa ya kinywa na meno na utaalam bingwa katika patholojia. Aidha, ni lazima kuwe na madaktari Bingwa wanne kwa kila fani ambao watakuwa wameajiriwa na hospitali husika.

(ii) Lazima kuwe na maabara ya daraja la juu yenye uwezo wa kufanya vipimo vya taaluma ya juu katika maneo ya damu (*Haematology*), *Biochemistry* (Kemia Uhai), Mikrobiolojia (*Microbiology*) na Mionzi (*Radiology*).

(iii) Lazima iwe na sehemu ya matibabu ya nje (*OPD*) yenye kukidhi taaluma nilizozitaja awali.

(iv) Lazima iwe na uwezo wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na wataalam mbalimbali wa afya.

(v) Lazima iwe na vitanda visivyopungua mia tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mtakatifu Gaspar ya Itigi haina miundombinu na utaalam wa kukidhi mahitaji ya kuwa Hospitali ya Rufaa. Kwa sababu

hiyo, kwa sasa si muda muafaka Serikali kufanya mazungumzo ya kuifanya hospitali hiyo kuwa hospitali ya Rufaa kwa Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeazimia kuwa na hospitali za rufaa za Kanda za Kati na Kusini. Hospitali hizi zinaweza kujengwa na Serikali au madhehebu ya kidini kama Hospitali ya *KCMC* na Bugando.

MHE. ISMAIL J.R. IWWATTA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nilikuwa na maswali madogo ya nyongeza.

La kwanza, katika jibu lake la msingi amesema kwamba hospitali ina vitanda mia moja, lakini kwa mujibu wa taarifa nilizo nazo mimi hivi sasa hiyo hospitali ina vitanda 200 na mwezi huu mwishoni hospitali hii inatarajia kufungua wodi ya watoto yenye vitanda 150, kwa hiyo, jumla vitakuwa vitanda 350. Sasa inawezekana mimi nikawa sina taarifa sahihi, je, atakuwa tayari kuwatuma wataalam wake kwenda kuthibitisha kwamba vitanda viro zaidi ya mia moja na siyo mia moja kama anavyosema?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kwamba inawezekana kwamba baadhi ya wataalam kama alivyoeleza katika jibu lake la msingi wanaweza kuwa hawapo katika hospitali yetu hasa ukizingatia kwamba ile hospitali ipo Kijiji na wataalam si wengi sana wanaopenda kwenda Vijijini.

Swali, je, atakuwa tayari yeye na Wizara yake na wataalam wake kusaidia katika upatikanaji wa hawa wataalam ambao tunawakosa na kufanya hospitali hii isikidhi haja katika kuwezeshwa kuwa hospitali ya rufaa Kanda ya Kati?

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri kwamba inaweza ikawa kwamba vitanda vilivyokuwepo katika hospitali hiyo sasa vimezidi mia moja. Hii takwimu ya mia moja inatokana na makubaliano tuliyokuwa nayo kati ya Wizara ya Afya na hospitali husika katika kufidia gharama za vitanda.

Kwa hiyo, huku nyuma kama watakuwa wanaongeza bila kuiarifu Wizara, basi sisi takwimu tulizokuwa nazo ni mia moja. Kwa hiyo, kama sasa hivi watakuwa na vitanda 350, tutakuwa tayari kuwatuma wataalam wakafanye hivyo. Lakini kama nilivyosema awali suala si kuwa na vitanda vingi tu, kuna miundombinu mingi ambayo niliitaja hapo awali na yenyewe lazima ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupata wataalam, naweza kusema kwamba nchi yetu imekuwa na matatizo au uhaba wa wataalam bingwa katika fani mbalimbali kwa nchi nzima kwa ujumla.

Hivi juzi tu nikijibu swali la nyongeza nilisema kwamba tumewekeana Mkataba wa kupata Waganga (*Specialists*) kutoka Cuba, idadi yao itakuwa ni waganga 70, saba kati ya hao watakenda Zanzibar na 63 watagawiwa katika hospitali za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bila shaka na hospitali hii tunaweza kuisaidia kupata waganga lakini siyo kwa kiwango ambacho kitaifanya iweze kutoa huduma za hospitali ya rufaa.

Na. 98

Utekelezaji wa Bima ya Afya

MHE. AARON D. CHIDUO aliuliza:-

Kwa kuwa kumejitokeza matatizo mengi katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa watumishi wa Serikali hasa wale wa Serikali za Mitaa:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba uanzishwaji na utekelezaji wa Bima ya Afya umefanyika bila maandalizi ya kutosha?

(b) Je, maandalizi yatakamilika lini ili kupunguza au kuondoa kabisa malalamiko ambayo yanaendelea kutolewa?

(c) Je, uhusiano wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*) ukoje kwa wale ambao wamelazimika kujiunga katika taratibu zote mbili kama ilivyotokea kwa wafanyakazi wa Serikali za Mitaa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya maandalizi yafuatayo yalifanyika:-

- Utaratibu wa awali na utafiti ulifanyika mwaka 1992 ambapo timu ya wataalam kutoka Kitivo cha Uchumi cha Chuo Kikuu cha London chini ya usimamizi wa Profesa Brian Abel Smith, mwanzilishi wa Bima za Afya Duniani, ilibaini baada ya utafiti kuwa kulikuwa na uwezekano wa kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya hapa nhini.

- Wizara ya Afya iliunda timu ya wataalam wa fani za Uchumi, Sheria na Bima ambao walifanya kazi ya maandalizi kwa miaka minne (1996-2000).

- Wadau mbalimbali, vikiwemo Vyama vya Wafanyakazi, walishirikishwa kutoa maoni yao na kuhamasisha wanachama wao.

- Tathmini ya kwanza ilifanyika mwaka 1996 ili kuona utaratibu mzima wa utekelezaji utakuwaje na wadau mbalimbali walijulishwa.

- Kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia, semina na warsha mbalimbali zimefanyika zikiwashirikisha watoa huduma, wateja wa Mfuko, viongozi wa Vyama veya Wafanyakazi na wadau wengine kadhaa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Mfuko huu yalikwishakamilika na maboresho yanaendelea kufanyika kwa sababu mfumo huu ni endelevu. Malalamiko ya msingi yataendelea kushughulikiwa kwa kadri yatakavyojitekeza.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano uliopo kati ya *CHF* na Bima ya Afya ni kwamba hii yote ni Mifuko ya Kisheria ya Afya. Hata hivyo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unawahusu watumishi wa Serikalini Kisheria wakati *Community Health Fund* unawahusu wananchi wasio katika ajira rasmi kwa kuchangia kiasi fulani kwa mwaka.

Endapo mfanyakazi wa Serikali anayekatwa mshahara kwa ajili ya kuchangia Mfumo wa Bima ya Afya yuko katika eneo ambalo pia lina linatoa huduma ya *Community Health Fund*. Mfanyakazi huyu hawajibiki kuchangia Mfuko wa *CHF* kwani atapata matibabu kupitia kadi yake ya Bima ya Afya.

Na. 99

Shirika la Taifa la Maendeleo

MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) limepewa jukumu la kuendeleza Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara kwa kushirikisha na Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Viwanda na Biashara:-

(a) Je, ni mikakati gani imewekwa ya kuendeleza Ukanda huo kwa kuzingatia msisitizo wa suala hilo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 2 Agosti, 2003 wakati wa Uzinduzi wa Daraja la Mto Rufiji?

(b) Je, Serikali inawahusishaje wananchi wa Mikoa ya Kusini katika kuleta maendeleo ya kuanzisha viwanda kutokana na rasilimali nyingi walizo nazo katika Ukanda huo?

(c) Je, ni lini *NDC* au kitengo chake kitahamia Mtwara na kufanya kazi zake kikiwa huko ili kuwa karibu zaidi na eneo la kazi na kuweza kuwashirikisha zaidi wananchi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mikakati ya kuendeleza Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara ipo katika kuendeleza miradi ya miundombinu ya msingi. Kikwazo kikubwa cha maendeleo ya ukanda huu ni ukosefu wa miundombinu ya kuaminika, ikiwa ni pamoja na umeme na barabara hususan kwa upande wa Tanzania. Kwa kutambua hili *NDC* imeweza kuhamasisha na kushawishi nchi zinazoshiriki kuweka uzito katika kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya msingi katika maeneo ya ukanda huo.

Kwa upande wa Tanzania miradi ifuatayo imepewa kipaumbele:-

(i) Barabara kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara na ya Mtwara - Songea hadi *Mbamba Bay*. Ujenzi wa daraja la Mto Rufiji katika barabara ya Dar es Salaam hadi Mtwara - Songea umekamilika, wakati upembuzi yakinifu wa barabara ya Mtwara - Songea - *Mbamba Bay* unaendelea kufanyika.

(ii) Kuhusu Daraja la Umoja katika Mto Ruvuma la kuunganishwa nchi za Tanzania na Msumbiji, tayari nchi hizi mbili zimetia sahihi makubaliano ya ujenzi wa daraja hilo na juhudzi zinafanywa kutafuta fedha.

(iii) Mradi wa umeme kutokana na Makaa ya mawe ya Mchuchuma umo katika hatua mbalimbali za maandalizi.

(iv) Upanuzi wa uboreshaji wa Bandari ya Mtwara pia upo katika maandalizi. Aidha, ipo miradi inayobainishwa kwa maana ya kukuza utashi kwa miradi hii mikubwa ya miundombinu. Hii ni pamoja na miradi ya utalii, viwanda na kilimo.

(b) Wananchi wa Mikoa ya Kusini wanahuishwa kuleta maendeleo ya Ukanda huu kwa kuwa miradi hii yote ina manufaa kwa kutoa ajira za muda mfupi na mrefu kwa wale wenye nia ya kuwekeza, Serikali inaendelea kubuni mikakati mbalimbali yenye lengo la kuwawezesha kupata mikopo katika mabenki kwa ajili ya mitaji ya kimaendeleo, kitu ambacho kimekuwa kikwazo kwa wananchi wengi kushiriki katika uchumi.

(c) Mradi huu wa Ukanda wa Maendeleo ya Mtwara ni kwa nchi zote nne zinazoshiriki ambazo ni Tanzania, Malawi, Zambia na Mozambique. Kwa hiyo, *NDC* kufungua ofisi huko Mtwara itakuwa ni uratibu wa miradi ya ndani tu na kwa hiyo haiwezi kuendeshwa kwa kutegemea fedha za wafadhili. Kwa hali ya sasa ya kifedha ni vigumu kwa *NDC* kufungua ofisi kwa sababu ya gharama za kuiendesha. Hali itakaporuhusu, suala hilo linaweza likafikiwa.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Tanzania inategemewa kuleta msukumo mkubwa katika kuanzisha huu uendelezaji wa Ukanda huu wa Maendeleo na pia kwa kuwa hapa Dodoma tulianzisha Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu. Je, kulitumika vigezo gani na vigezo hivyo haviwezi kutumika katika

kuanzisha kitengo cha kuendesha *Mtwara Development Corridor* kwa kule Mtwara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba, kwa kuwa Mikoa ya Kusini ni tajiri sana sana kutoptaka na rasilimali za gesi, makaa ya mawe na kadhalika. Je, Serikali ina mikakati gani na hasa inieleze umeme wa gesi utafika lini Mtwara au utawaka lini katika Mikoa ya Mtwara na Lindi?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mradi wa Mtwara unahusisha nchi nne kama alivyosema Naibu Waziri, lakini vile vile ndani ya nchi yetu mradi wa Mtwara unahusisha Mikoa nane ambayo n Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya lakini Mikoa miwili ni Pwani ambayo inahusisha Wilaya ya Rufiji na Mkoa wa Morogoro ambao unahusisha Wilaya mbili za Ulanga na Kilombero.

Kwa hiyo, kazi ya kuratibu shughuli za *Mtwara Corridor* lazima zifanywe Makao Makuu ya *NDC*, Mjini Dar es Salaam kwa sababu ina *coordinate* Mikoa nane. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, katika hili ni kwamba Tanzania ndiyo mratibu sasa hivi wa nchi zote nne katika *Mtwara Corridor* na huyu *manager* aliyepatikana wa ku-*coordinate* lazima akae Dar es Salaam kwa sababu ndiyo Makao ya Makuu ya *NDC* na hiyo ndiyo kwa mujibu wa makubaliano kati ya hizi nchi nne. Mfadhili wa Mradi huu ni Serikali ya Afrika Kusini, kwa hiyo lazima tukubaliane na taratibu ambazo tumekubaliana ili huyu *coordinate* akae Dar es Salaam aendeshe mradi chini ya Uendelezaji wa Ukanda wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jibu la swali la pili, ni kweli jeshi ni moja ya miradi mhimili katika *Mtwara Development Corridor* ikiwa pamoja na mradi wa Songo Songo na Mradi wa *Mnazi Bay*. Hivi sasa ninavyozungumza makubaliano yamefikia mbali sana kuhusu *Mnazi Bay* kuufanya na wenyewe uzalishe umeme. Kwa hiyo, Mipango hii inaendelea lakini siwezi kutaja lini tutaanza kupata umeme Mtwara, lakini mambo yatakapokamilika tutapata huo umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kimekwisha na maswali kadhaa hatujayafikia leo. Lakini kwa nia ile ile kwamba Mheshimiwa Mbunge anaposimama kutaka kuuliza swali la nyongeza angependa kupata ufanuzi ili wapiga kura wake wamsikie kwamba yuko Bungeni na anawakilisha mawazo waliyompa. Kwa hiyo, hayo maswali yaliyobaki Katibu ataendelea na utaratibu wetu wa kawaida.

Sasa katika kujibu maswali hapa ni ufanuzi tu kwa ajili ya *Hansard*. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali namba 96, Mbunge wa Kilolo aliitwa Mbunge wa Chilolo. Chilolo ni jina la Mheshimiwa Mbunge wenzetu humu ndani ya Bunge. Kwa hiyo, Jimbo lile ni Kilolo.

Sasa kuna matatizo ya vikao, Mheshimiwa Dr. Samuel Malecela anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba wahudhurie kikao cha Kamati kitakachofanyika katika ukumbi namba 133 ghorofa ya kwanza saa 5.00 asubuhi.

Lakini pengine kabla sijaendelea na matangazo ya vikao na mimi nawatangazia wajumbe wa Kamati ya Uongozi ile Kamati inayoratibu shughuli za Bunge humu ndani ile ambayo Wenye viti ndiyo Wajumbe tukutane saa 5.00 asubuhi, kabla vikao vingine havijaanza ama mteue watu wa kuwawakilisha tukamalize jambo dogo ambalo ni la dharura tu. Kamati ya Uongozi ya Bunge ambayo inaratibu shughuli za Bunge tukutane saa 5.00 asubuhi kwenye chumba chetu cha kawaida.

Pia Mheshimiwa Halima Kimbau, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa Chama cha Mapinduzi kwamba wakutane leo chumba namba 231 saa 7.00 mchana baada ya kuahirisha shughuli zetu za Bunge.

Pia Makamu Mwenyekiti wa *TWPG* nadhani hiki ni chama cha Wabunge Wanawake wote bila kujali Chama, Mheshimiwa Janeth Mashele, anawaomba wakutane kwa dharura alitaka wakutane saa 4.30 asubuhi, lakini nitawaomba mtafute muda mwingine, huu ni muda wa Kikao cha Bunge na hii ni *NGO* tu.

Pia Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi anawaomba wajumbe wote wa Kamati ya Chama cha Mapinduzi wakutane humu ndani ya ukumbi wa Bunge saa 7.00 mchana baada ya kuahirisha shughuli za Bunge. Hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani nadhani kuna tangazo lingine ambalo limesahauliwa.

NAIBU SPIKA: Hili limekuja tayari nimeshamaliza matangazo mengine. Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 asubuhi.

Lakini Mheshimiwa Eliachim Simpasa nitamwomba anisaidie hapa, kule ataendelea mtu mwingine, kwa sababu mimi ninakwenda kwenye kikao cha Kamati ya Uongozi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Eliachim Simpasa, afike hapa ili aweze kunisaidia.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa Alikalia Kiti)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Majini wa Mwaka 2003
(The Merchant Shipping Bill, 2003)

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kuniruhusu nichangie katika Muswada huu. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Muswada huu. Lakini vilevile kuna mambo kama manne hivi ambayo napenda kuyasemea kuhusiana na Muswada huu.

La kwanza kabisa ni katika kifungu cha 144 ambapo wanazungumzia *Illness caused by own fault*. Sasa katika kifungu hiki nadhani watu wengine wanaweza wakapoteza haki zao kama mwajiri anaweza akatafsiri baadhi ya magonjwa kwamba wewe ulijitakia. Niliona baadhi ya maelekezo katika Mfuko wa Bima ya Afya wanassema ugonjwa kama Ukimwi na magonjwa mengine hawatashughulika kutoa fedha kwa ajili hiyo.

Sasa katika hili inawezekana kabisa mtu aliugua kwa kudungwa sindano au ilimtokea bahati wakamuongezea damu, halafu mwajiri akamwambia huyu kwamba huu ugonjwa mimi sihusiki na kukutibu ama sihusiki na kukulipia muda wako ambao ulikuwa umesafiri. Kwa hiyo, nadhani kifungu hiki Mheshimiwa Waziri atafute namna ya kukipunguza makali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifungu tena kingine cha 160(4) ambapo wanazungumzia *expense of medical and other treatment during voyage*. Kinasema: “*Where a person dies while employed in a Tanzanian ship, his next of kin shall be entitled to compensation of not less than the equivalent in Tanzanian shillings or United States dollars twelve thousands or to imprisonment for a term not exceeding five years or to both.*”

Sasa kwa sababu sikuona marekebisho nadhani kama hilo tukiliacha hivyo watu watafungwa aende pale kudai fedha zake, halafu anafungwa vibaya sana. Kwa hiyo nadhani wanaohusika wafanye marekebisho kwenye kifungu hicho kwa sababu hatukuyaona marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 162 kinasema: “*The Minister may make regulations referred to in this Act as the “manning, Training and Certification Regulations....”*” halafu anaendelea. Halafu *section one* anasema: “*The Minister may,*” sasa kama tunaweka hapa utaratibu, halafu Sheria tena inapunguza inasema Waziri anaweza akajisikia au hasijisikie kwamba anataka hawa watu wawe wanaendelea huko ndiyo baada ya miaka mitano sheria imekwishatungwa halafu ndiyo na ye ye anatunga kanuni itakuwa si vizuri. Kama tumekubaliana kanuni zinatungwa zitungwe kwa mujibu wa sheria hii *when the Minister must be compelled kuhakikisha kwamba anatunga hizo kanuni.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bahati mbaya nimehesabu neno *Minister lilikotajwa* katika Muswada huu na madaraka aliopewa kwa kweli yanatokea zaidi ya mara 2,014. Sasa madaraka yote amepewa Waziri, anapewa, anapewa, sasa na vile vyombo vingine sijui vitafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kifungu hiki cha 163(1): “*The Minister may exempt any ship or description of ship from any requirements of regulations made under section 162.*”

Sasa mimi ninavyojuu meli sijui mtunga Muswada ameangalia Dar es Salaam ambako kuna meli kubwa, sijui ameangalia meli zitakazokuwa katika Mto Kagera na maziwa mengine madogo madogo kama Burigi. Maana kama ni suala la meli ndogo mpaka lije limfikie *Minister* ndiyo aanze u-exempt sasa watumishi wengine wafanye nini?

Mimi nadhani watumishi wengine na wao waaminiwe kwamba wanaweza kufanya *exemption*. Halafu na hii *exemption* tumekubaliana hapa masharti ya msingi na tumesema kwa meli za Polisi, meli za Jeshi la Wananchi na zile ambazo zinaweza kumilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano tayari sheria hii haizingizi huku. Sasa tunaweka utaratibu halafu sasa mtu mwagine anataka ku-exempt, ana-exempt nini na kuna nini huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuelewa kuna kitu gani huko anataka kuki-exempt, vinginevyo kifungu hicho mimi nadhani kiondolewe. Kama tumesema masharti waende wakayatimize masharti hayo. Hapa anaposema kifungu 3(2)(d) hivi vyombo vingine vya Serikali vyenyewe visifuate masharti hata ya usalama hata kama ni kuchafua mazingira waende wachafuechafue tu eti kwa sababu wao ni Serikali.

Mimi nadhani ni utaratibu ambao tufike mahali na wao tuwambie wasiende kuchafua chafua na kama wanamuajiri mtu inakuwa basi na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ni cha 123(b) mpaka (c) ambapo sasa Waziri vilevile amepewa madaraka ya kutunga kanuni zinazohusu mambo mengi tu. “*Engagement on board foreign ships of Tanzania nationals, the implementation of any convention relating to the employment, welfare, security, certification and status of seafarers, medical care, sickness and injury benefits for seafarers; wages in general...*” halafu inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Waziri atakwenda tena atunge kanuni, aseme nyinyi mtakayemuajiri mlipe mashahara huu. Kwa utaratibu tunavyojuu ni kwamba Serikali ya Jamhauri ya Muungano wa Tanzania ndiyo inawalipa watumishi wake fedha kidogo ikilinganishwa na Mashirika mengine kama *TBL* na *CRDB*. Sasa akiwa na mawazo kichwani mwake kwamba na hawa wapate mishahara midogo kama watumishi wengine wa Serikali atawaathiri sana hawa. Tunadhani watu wanafanya biashara waende wakakubaliane.

Mimi naamini ye ye anajua watumishi kwenye meli ya Serikali ambao amesema wasiguse na sheria hii, labda Kapteni wa meli wanamlipa shilingi 200,000/= sasa huyu wameishakubaliana wamlipa shilingi 500,000=/. Halafu ye ye anasema lakini zisipungue shilingi 200,000/= maana yake hii itawaathiri awaache waende kule wakakubaliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni mambo ambayo nadhani katika Muswada huu yarekebishwe. Halafu kwenye vifungu vyote ambapo yaani *the Minister may* mpaka kwenye Vyuo kote huku anateua. Nadhani labda Mheshimiwa Waziri anataka kuwadhibiti watu wasije wakamletea utata kama walivyofanya kwenye hii *TTCL*, nadhani ye ye alikuwa hajawa Waziri wakati wanatunga ule Mkataba wa *TTCL*. Sasa japo haipo hiyo ya *TTCL* sitaki kuisema sana. Kwa sababu nilikuwa na hoja nataka kuileta hapa wakanidhulumu na nilitaka kuwapigia fimbo sasa nitatafuta mpini hatuwezi kukubali watu wanatudhulumu. Sasa labda hayo ndiyo Waziri alitaka kuyadhibiti, lakini ninadhani kwamba baadhi ya madaraka awape Makamishna ili waweze kuyashughulikia. Sasa nategemea yale ambayo amesema kwamba mtu akija kudai fedha za ndugu yake afungwe, hayo atayaondoa pamoja na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. Kama watayarekebisha mambo na kuyapunguza huenda wakati tunapitisha vifungu tutaunga mkono. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nakushukuru kupata fursa hii kuchangia katika Muswada wa *Merchant Marine*. Niseme tu kwamba kwa kweli naunga mkono Muswada huu na mimi ni mjumbe wa Kamati, kwa hiyo, tumeupitia Muswada huu kwa kina. Lakini nina machache ya kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa kuleta Muswada huu, kwa sababu umekuja kutekeleza kitu ambacho kwa muda mrefu tulikuwa tumekisahau. Nadhani kwa mujibu wa magazeti ya juzi na jana sasa ni dhahiri kwamba uchumi wa Tanzania utakuja kupita ule wa Kenya itapofika mwaka 2005, na maana yake ni ndogo tu kwamba soko la Tanzania linaonekana sasa linafaa kwa biashara ya Kimataifa na kwa kweli biashara ya Kimataifa inafanywa zaidi kuititia ubebaji majini, kwa sababu ndiyo njia rahisi kwa usafirishaji wa bidhaa.

Lakini vilevile ni muhimu kuzingatia kwamba biashara hiyo ya Kimataifa inayokuja Tanzania haiishii hapa hapa Tanzania. Kwa bahati Tanzania ndiyo nchi ambayo inapakana na nchi nyingi kwa eneo letu la *East Africa*, ni nchi nane karibu na katika hizo nyingi zao zimekuwa *landlocked*, hazina bandari. Kwa vyovyote vile kuwepo na *competition* kati ya bandari za Tanzania na zile za majirani zetu kama Msumbiji na Kenya.

Sasa nadhani sheria hii ambayo inakuja kuzungumzia suala zima la ubebaji na kama wanavyosema Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba mengi yatakekelezwa chini ya Waziri mwenyewe nadhani tumelielewa hilo, kwamba kutakuwa na vyombo maalum kama *SUMATRA* na kadhalika ambavyo kwa kweli vitakasimiwa madaraka ya Waziri.

Kwa hiyo, hakuna wasiwasi kuhusu hilo. Lakini ni vizuri tu hata katika utengenezaji wa vyombo hivyo ikaeleweka kwamba sisi tuna-*compete* sasa na bandari nyingine katika eneo letu. Kadri sisi tunavyotengeneza shughuli zetu ziwe rahisi zaidi ndivyo wale wabebaji watavyopendelea bandari ya Dar es Salaam na kwa maana hiyo

kutupa fursa ya kuweza kuhudumia nchi hizi nyingine karibu sita ambazo zitakuwa ni tegemezi kwa bandari yetu.

Sasa sitegemei sheria yetu iwe ni sheria ya aina ya kuwazuia hao wabebaji na Mashirika hayo makubwa kufika kwetu kwa sababu ya masharti magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lazima tulinde maisha ya mabaharia wetu na maslahi yao. Lakini lazima tuangalie kwamba vyote hivyo vinaendana na mfumo wa soko huria. Sidhani kwamba Serikali ya Tanzania ina ubavu wa kuanza kuyaambia Mashirika ya Kimataifa walipe fedha kiasi gani au kuweka masharti magumu ambayo mwisho wake yanaweza yakasababisha watu hawa wakimbie hata kuja kutumia bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi nilikuwa napenda uliangalie hilo. Sheria isije kuwa ni ngumu kiasi kwamba watu waone bandari zetu hazina maana, kwa sababu zinawaongezea gharama na kwa hiyo kukimbilia Kenya na kuipa nafasi Kenya au Msumbiji kuhudumia nchi zile ambazo zimekuwa *landlocked*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie kidogo ni suala hili la utekaji nyara na uharamia. Nakubali kwamba lazima ziwepo sheria za kuhakikisha kuwa utekaji nyara na uharamia baharini unadhibitiwa kwa ushirikiano *of course* na Mashirika mengine na nchi nyingine duniani. Lakini kuna maziwa, tunaona kwamba sheria hii kwa mara ya kwanza imeingiza na masuala ya maziwa tofauti na sheria ya mwaka 1967. Kwa kweli tukichunguza katika maziwa haya utakuta kwamba ile *onus* au jukumu la kusimamia utekaji nyara na uharamia katika maziwa yetu kwa kiwango kikubwa liko chini ya Serikali ya Tanzania.

Sasa mimi kidogo nina wasiwasi hapo kwamba kwa kweli kwa mfano, kwenye Ziwa Tanganyika sisi tuna uwezo! Maana yake kila siku kuna utekaji nyara na ni mambo tu ambayo kama ilivyo kwa Mikoa ya pembezoni ambako hakuna hata Waandishi wa Habari, kwa hiyo, matukio mengi hayaandikwi mara nyingi. Lakini ukweli ni kuwa watu wanatekwa nyara kwenye boti na watu wanafanyiwa uharamia wa kila aina na kwa vyovypote vile hakuna msaada, na hii ni kwa sababu hatuna chombo kama ilivyo trafiki katika kushughulikia masuala ya magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningependa kushauri kuwa kwa kweli katika maeneo ya maziwa ambako Mheshimiwa Waziri amepewa uwezo wa kutunga sheria ndogo, sheria hizo zitungwe haraka iwezekanavyo na zitafutwe fedha basi ili tuweze kuweka miundombinu ya kuhakikisha kwamba maisha ya raia wetu katika maeneo hayo yanalindwa. Kwa mfano, kwa Ziwa Tanganyika, kuna boti mbili tu ndogo ndogo za Polisi zina *speed* kali kidogo, lakini tumeambiwa kwamba zingine zilinunuliwa *second hand* sasa hazina nguvu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ninaloliona kule ni kwamba hizo boti ambazo tunazitegemea kwa ajili ya ulinzi wa wananchi wanaosafiri ziwani Tanganyika kwa mfano, eti zikitaka kuondoka kwanza inatakiwa wananchi wachangie mafuta na hiyo ni

boti ya Serikali inakunywa lita 3,500 kwa *trip* moja wananchi kwanza wachangie na kama hawakuchangia fedha za mafuta hata kama akionekana mtu anaua watu kilomita mbili kutoka nchi kavu boti ile haiendi na haina maana kuwepo pale. Sasa sijui Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itafanya nini?

Nimeona kuna mkakati wa vikosi *guard*, nadhani kwa huko Dar es Salaam kwa sababu tuna *Navy* hawa wapo wanasaidia. Nimewaona jana kwa mfano hawa watu wa *TRA* wamekamata meli iliyokuwa inakwenda Msumbiji huko, wameipeleka Bagamoyo, kuna ubishi mkubwa kuhusu ni *court* gani, nadhani hata tulipokuwa tunapitia sheria hii au Muswada huu katika Kamati hilo lilijitokeza kwamba ni *court* katika ngazi gani? Wale wenye meli iliyokamatwa na hizo tani nyingi za sukari wanasema kwamba hatuwezi kwenda sisi kwenye Mahakama za Wilaya bwana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa hilo liangaliwe vizuri. Kwa kweli mimi nafikiri katika maeneo ya maziwa na ningependa nilisemee hilo kwa sababu kwa wanaosemea upande wa bahari ni wengi sana. Lakini isisahaulike kwamba tunapopokea mizigo kwa tani nyingi sehemu kubwa ya mizigo ile inakwenda katika nchi za nje, Kongo, Burundi na Zambia. Unakuta katika Ziwa Tanganyika kuna meli zaidi hata ya 200 na nyingine kubwa kabisa zinabebea *container* 50, 60 hii ni kwa sababu kuna umuhimu wa ubebaji wa mizigo hiyo kuipeleka nchi nyinginez.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatujui, mimi nina tatizo kidogo kuhusu kwa mfano, bandari ya pale Kigoma, nimekuwa nikipiga kelele sana kwamba kwa nini bandari kubwa kama ile inayaoingiza fedha za kigeni nyingi tu kuliko hata *Dar es Salaam International Airport*, eti iko chini ya *Railway* ambapo sijui mimi utaalamu wao katika masuala haya.

Nashukuru kwamba kumekuwa na utaratibu kuwa inawezekana baadaye bandari hii ikaingizwa iwe chini ya *THA*. Lakini nasema bandari moja tu haitoshi kwa ziwa refu namna ile. Unakuta una Bandari ndogo ya Ujiji kwa mfano, Bandari ya Kibirizi ambavyo kwa kweli ni vituo muhimu na vinakuwa kama ni vituo vya polisi huku nchi kavu kwamba *infrastructure* ya kuweza kudhibiti mambo haya, hizi hakuna, hazijapewa hadhi yoyote na kwa kweli hazijajengwa kwa namna yoyote zipo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependekeza kwamba katika kuongeza usalama na katika kupunguza utekaji nyara na kadhalika bandari hizi za Ujiji na Kibirizi na zenyewe ziweze kuboreshwa na ziweze kuwekewa miundombinu ambayo itasaidia kama panatokea matatizo. Kwa sababu ni mwendo mrefu kutoka Kigoma mpaka Ujiji kwa usafiri wa majini, inachukua muda mrefu na kwa hiyo kama huduma zitakuwa zinaanza pale tutakuwa tunaweza kudhibiti matatizo mengi ambayo kwa mara nyingi yanatokea upande wa Kongo. Utekaji nyara na uharamia kwa kweli mara nyingi unatokea upande wa Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna hili suala la kuratibu au kiutendaji kusimamia nini kinachoitwa meli. Nimesikia hapa tafsiri iliyotolewa jana kwamba meli ni chombo chochote kinachoelea ni kweli, lakini vyombo hivi vinapitana ukubwa. Kwa

mfano, sijui kama meli ni lazima iwe ya chuma au hata ya mbao. Uzoefu wetu sisi katika Ziwa Tanganyika, tunatengeneza boti za mbao ambazo moja ya boti hizo zinaweza kabisa kubeba tani tangu 60 mpaka 100, unapakua kabisa mabehewa mawili na unayajaza ndani ya boti moja. Sijui sasa tunaya *classify* vipi na yenyewe yatahitaji bima au hayahitaji bima na mara nyingi kunatokea hata ajali kwa meli kama Liemba ambayo ni kubwa zaidi kugonga boti na kuua watu na kuzamisha mizigo, lakini ni utaratibu gani kwa kweli unaofuatwa ili watu wapate fidia.

Mara nyingi hili jambo halijaangaliwa na ndiyo maana nasisitiza kwamba hizi sheria ndogo ambazo zimeruhusiwa chini ya sheria hii tunayoitunga sasa, ni bora zitungwe haraka iwezekanavyo ili kuweza kutoa nafasi kwa vyombo kama hivi. Katika maziwa makuu tofauti na baharini ambako kwa kweli tunawalenga zaidi wafanyakazi au Mashirika ya Kimataifa, huku ni wananchi wetu ndiyo wenye vyombo vingi vya usafiri na ndiyo wenye vyombo vingi vya ubebaji.

Lakini bado na wenyewe wanafanya biashara hiyo hiyo sijui tunawawekea unafuu gani katika *ku-compete*. Ninavyoelewa kwa mfano, Burundi wana meli zisizopungua 40 kubwa zinabeba ma-container na kadhalika. Wao tutawa-regulate vipi na mpaka sasa tuna tatizo kwa mfano, tunayo bandari kubwa kabisa, tuna makampuni 18 ya kigeni yanafanyakazi pale ya ubebaji wa mizigo lakini hayalipi kodi, hatujui labda wanawalipa *TRA*. Sisi watu wa pale hatujaona hata senti yao moja na tunaona ajabu kubwa sana ni nani anayeratibu shughuli za usafirishaji katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi yangu yalikuwa ni hayo, kwamba tunapoandika sheria hii ambayo kwanza mimi naikubali, kwa sababu imekuja wakati muafaka wakati ambao Tanzania tunatakiwa sasa kutafakari nafasi yetu katika eneo letu kibiashara.

Kwa hiyo, naomba sheria hii isije kuwa *indictive*, isije kuwa ni sheria ya kujaribu kuweka matakwa. Wazungu wanasema: “*If wishes were horses all beggars would ride one.*” Kwa sababu ukipenda tu kitu si lazima kiwe lazima tuangalia na hali halisi.

Sisi kama Watanzania tuna *compete* vipi katika suala la bandari *East Africa* katika kuhudumia, kwa sababu nadhani tukijiweka vizuri usafirishaji kuanzia huku majini kupitia kwenye reli zetu halafu kwenye maziwa makuu kinawenza kuwa ni chanzo kimoja kikubwa sana cha mapato kwa nchi yetu.

Kwa hiyo, nashauri tu kuwa sheria hii isiwe *indictive* iangalie *opportunitie* na iangalie mianya ambayo inaweza ikaisaidia nchi yetu na wakati huo huo kuangalia ndugu zetu ambao wengi wao wanashughulika katika maziwa tofauti na ilivyo katika bandari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. (*Makofî*)

MHE. SAMWEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja hii kabla ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu mimi ndiye mtu wa mwisho nitakayezungumza.

Vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomsya, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha Muswada vizuri. Kwa kweli lazima nikiri kwamba Muswada huu ulicheleweshwa sana kuletwa.

Kwa hiyo, napenda tu kuwashukuru sana kwamba wanafanya vizuri kuuleta wakati muafaka pamoja na kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa mchangiaji wa mwisho nikimaanisha kwamba mengi yamezungumzwa, lakini si vibaya na mimi nikizungumza kidogo. Nilitaka kuzungumza mambo ya meli kugongana, lakini yote yameshazungumzwa.

Napenda tu kusitiza kwamba kwa kuwa jimbo langu Kata mbili ni Visiwani yaani Kome na Maisome. Kuna Kata mbili ni Visiwani kabisa, kwa hiyo nina jimbo ambalo kuna Visiwa vidogo vidogo zaidi kumi na moja viko majini na nchi kavu ninayo sehemu kubwa. Kwa hiyo, ninayo haki kabisa ya kuchangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi sana ya wananchi wavuvi na vyombo vyao hasa hii mitumbwi midogo midogo, wamekuwa wakigongwa na meli usiku hivi kuna ulazima gani namwuliza Mheshimiwa Waziri wa meli hizi ndogo kufanya safari za usiku wakibeba abiria na wakati huo huo wakifanya safari hizo kwenye sehemu ambazo zina wavuvi wadogo wadogo wakivua usiku, kama kuna ulazima huo basi wapewe tahadhari waambiwe wawaogope na wawaheshimu wanaovua huko ziwani wakiwa na vyombo vyao aidha wamelala usingizi.

Kwa mwaka huu tu kuna matukio kama mawili ambayo nina ushahidi nao ya kugongwa na meli au *ferry* ikiwagonga wavuvi amba wanalala kwenye ile mitumbwi midogo wakisubiri nyavu zao zisiibiwe.

Napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kuna meli moja inaitwa Karai kwa jina la utani ni boti ya Kenya iko *Lake Victoria* na inafanya safari Jimboni kwangu Buchosa. Inafanya safari kwenye Visiwa vya Zilagula, Iyozi na Chamagati na sehemu zingine ndani ya jimbo la Buchosa, eneo la Maisome. Lakini meli hii imekuwa ikizimika zimika sana ni boti *as such* lakini wanatia meli, ni boti ndogo. Imekuwa ikizimika zimika ziwani na kuwatishia usalama abiria waliomo ndani ya boti hiyo.

Mimi mwenyewe nimeshashuhudia zaidi ya mara tatu nikiwa kwenye meli nyingine, lakini naiona ile inazimika zaidi ya mara tatu Ziwanu. Kama ilipanga labda kufika mwisho ya safari yake baada ya masaa 8 inafika labda baada ya masaa 16. Mimi nafikiri hii ni hatari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chombo ambacho mwaka jana au juzi kimeundwa kwamba kuwe na ukaguzi wa majini. Lakini nikiangalia ukaguzi huu unaofanywa na Shirika la *Mbondo Fishing* sijui nini. Ukaguzi huu wa vyombo umekuwa ni kero kwa sababu unakuta huyu bwana anayekagua huyu *Mbondo Fishing* sijui nini anakagua mitumbwi midogo midogo kwa kupima futi. Mtu ametengeneza mtumbwi wake labda kwa thamani ya shilingi 100,000/= au 70,000/= lakini anakuja kum-charge shilingi 40,000/= au 50,000/= na akikataa anafunga mitumbwi hii midogo midogo anaipeleka sehemu anayoitaka yeye.

Hii imekuwa ni kero kabisa kwenye jumbo la Buchosa. Sisi tulishaamua kwamba labda yeche angepitisha semina akawaeleza wananchi pole pole wakaelewa. Lakini semina hataki kabisa kuja kufanya na hata Madiwani. Sasa ujue hiyo ni kero kubwa kwa sababu huyu anakuja anataka apewe fedha kiasi fulani. Sawa anawakatia hiyo invoice nafikiri hatoi risiti sijui anawakatia invoice na anawatoza labda shilingi 30,000= Ukienda watu wa Maliasili Serikali sasa na yenyewe inakuja pale wanasema kwamba sisi tunahitaji kila mtumbwi shilingi 16,000/= au 20,000/. Sasa wananchi wanashindwa kujua ushuru halali walipe wapi au waache wapi.

Mimi naomba hili Mheshimiwa Waziri ulifanyie kazi ni kero kabisa hasa Jimboni kwangu ambapo wavuvi wengi wapo na kazi yao kubwa wanafanya shughuli ya uvuvi. Ninaomba hili uje uliangalie kwa mapana na marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada hii kwa ujumla ni mizuri kwa sababu itarejesha heshima baadhi ya watu wetu ambao aidha wanadandia meli kwenda nje na baadaye kutozwa bila sababu yoyote ni kwa sababu tu wamedandia tu zile meli.

Muswada huu ulioletwa na sheria hizi zinazotakiwa sasa hivi zianze za kazi mara moja zinahusu meli zote. Lakini kuna kitu tunaita kama ubaguzi. Nikisema maji ya chumvi nina maana maji ya bahari. Kule vyombo vya uvuvi, meli za uvuvi zinaruhusiwa kufanyakazi. Sisi kwa nini *Lake Victoria* tunazuiwa kutumia meli ili tuvve wanatuacha tuendelee kuchonga mitumbwi ya kawaida ya mininga na miti mingine. Sasa kama hizi sheria zinahusu meli zote basi na sheria ya uvuvi na sheria ya meli ya uvuvi ambazo wamezisema hapa zitahusiana na meli zote basi na *Lake Victoria* ipewe ruhusa hiyo ya wananchi waweze kununua meli za kisasa ili wavue kuliko kutumia hizi *local* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimesema kwamba nimekuwa wa mwisho na umesema labda makusudi kwamba niwe wa mwisho kuzungumza mengi yameshazungumzwa hapa na nitakayotaka kuzungumza nitakuwa narudia rudia na huwa sio kawaida yangu.

Mimi napenda kukushukuru ila namwomba tu Waziri hili jambo la Mbondo alifanyie kazi kabisa ni kero kwa wananchi wangu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshasema hatutaki kero kwa wananchi sasa hili la Mbondo kwenda kukamata mitumbwi ya watu na kutozwa pesa ambazo aidha, ni nyingi zaidi au ni kidogo lakini ni kero. Ninaomba alifanyie kazi tu kwa umakini mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaunga hoja hii mkono asilimia mia moja bila upungufu. Ahsante sana. (*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. LEONARD M. SHANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Awali ya yote naunga mkono Muswada huu na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watalaam wa Wizara kwa kutuletea Muswada huu wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea usafirishaji na biashara ya meli kinachojitokeza mara moja ni suala la uhusiano kati ya vyombo vya meli na shughuli zote za bandarini - bandari ndogo au kubwa ukweli ni kuwa meli na shughuli za bandari huwezi kuzitenganisha. Nilitegemea Muswada huu ungeweka wazi uhusiano wa biashara ya meli na shughuli za bandari.

Kwa hapa namaanisha Muswada huu ungeweka wazi kuwa makampuni ya meli yatoe mchango unaodhahirika katika maendeleo na uundaji wa miundombinu ya bandari inayotakiwa kutumiwa na meli na bidhaa zake kwa mfano mahali pa kuegesha meli na majengo (*godowns*) ya kuhifadhi bidhaa zinaletwa au kuingizwa na meli na zile zinazochukuliwa na meli. Haitoshi kuona kuwa ni Serikali au taasisi za bandari peke zinatakiwa kuchangia maendeleo ya kujenga miundombinu mbalimbali za bandari *some infrastructures are so specialised for their use only by ships and shipping.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lingemulikwa katika Muswada huu ni suala la kushiriki kikamilifu kama taifa la Kitanzania katika shughuli nzima ya usafirishaji na biashara ya meli.

Muswada huu tunaupitisha kwa manufaa ya nchi zingine na sio Tanzania. Ningependa kuona kuwa Tanzania ingejiandaa kufaidika kikamilifu na biashara ya meli hasa kwa mfano kwa kiwango gani katika bandari zetu tumekwishajitarisha kimiundombinu, kiutalaamu na kihuduma kunufaika na kukua kwa biashara za meli kwa mfano *drydocks, repairworks, supplies to ships, volume of imports and exports, etc.* Kwa sasa Tanzania haionyeshi kuwa imejitarisha kutoa huduma kwa kiwango cha ubora wa Kimataifa. Zaidi sana sisi hapa Tanzania tunaelekea kushabikia biashara za kupitisha tu bidhaa na huduma yaani tunao uwezo wa kugusagusa tu kwa kila eneo la biashara za meli *transit and light works services, etc.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu kuhusu upungufu wa Muswada huu ni suala zima la kwenda na wakati katika biashara ya meli hasa ukilinganisha na teknolojia katika maendeleo ya biashara ya meli. Sheria hii kwa sababu inagusa maeneo ya maeneo ya Kimataifa hasa katika bahari lazima ingeona umuhimu wa Tanzania kuanza kuwa na vyombo vya kulinda usalama wa vyombo hivi. Leo Tanzania hatujafikiria kununua na tuwe na vyombo vya usalama kutuhakikishia usalama wa vyombo vyetu na pia kulinda usalama katika maeneo ya bahari yaliyo chini ya miliki za Taifa letu (*marine security in the territorial waters*).

Leo hii tunasikia kuwa meli za kigeni zinaingia katika bahari yetu na kuvua au kuingiza bidhaa kimagendo na hakuna uwezo wa kukabiliana na matatizo kama haya. Sheria hii inaelekeza nia nzuri ya kukabiliana na majanga haya lakini haina meno ya kuuma kwa mfano, ajali iliyotokea Ziwa Victoria ilionyesha jinsi Taifa hili halina uwezo leo miaka imepita lakini hakuna maandalizi ya kuokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni suala linalohusu usafiri, usafirishaji katika maziwa na mito ndani ya nchi lazima sheria itoe miongozo ya kulinda maisha na mali za wananchi. Kwa kweli kiwango cha usafiri na usafirishaji katika maziwa na mito ni chinbi sana na *at most it is a ruvugu match*. Sheria hii ingemulika zaidi na kusafisha sekta hii ya usafiri na usafirishaji. Sekta hii inaonekana inaendeshwa kama hakuna Sheria na wananchi (abiria) na bidhaa zao hawana haki kabisa. Sheria hii iimarishe na ifagie uchafu nyumbani kwanza usafiri na usafirishaji katika maziwa na mito iwe kioo cha Taifa katika Sekta hii ya usafiri, usafirishaji na biashara ya meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada huu wa mwaka 2003.

Muswada huu tunaupitisha kwa manufaa ya nchi zingine na sio Tanzania. Ningependa kuona kuwa Tanzania ingejiandaa kufaidika kikamilifu na biashara ya meli hasa kwa mfano kwa kiwango gani katika bandari zetu tumekwishajitarisha kimiundombinu, kiutalaamu na kihuduma kunufaika na kukua kwa biashara za meli kwa mfano *drydocks, repairworks, supplies to ships, volume of imports and exports, etc.* Kwa sasa Tanzania haionyeshi kuwa imejitayarisha kutoa huduma kwa kiwango cha ubora wa Kimataifa. Zaidi sana sisi hapa Tanzania tunaelekea kushabikia biashara za kupitisha tu bidhaa na huduma yaani tunao uwezo wa kugusagusa tu kwa kila eneo la biashara za meli *transit and light works services, etc.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu kuhusu upungufu wa Muswada huu ni suala zima la kwenda na wakati katika biashara ya meli hasa ukilinganisha na teknolojia katika maendeleo ya biashara ya meli. Sheria hii kwa sababu inagusa maeneo ya maeneo ya Kimataifa hasa katika bahari lazima ingeona umuhimu wa Tanzania kuanza kuwa na vyombo vyaya kulinda usalama wa vyombo hivi. Leo Tanzania hatujafikiria kununua na tuwe na vyombo vyaya usalama kutuhakikishia usalama wa vyombo vyetu na pia kulinda usalama katika maeneo ya bahari yaliyo chini ya miliki za Taifa letu (*marine security in the territorial waters*).

Leo hii tunasikia kuwa meli za kigeni zinaingia katika bahari yetu na kuvua au kuingiza bidhaa kimagendo na hakuna uwezo wa kukabiliana na matatizo kama haya. Sheria hii inaelekeza nia nzuri ya kukabiliana na majanga haya lakini haina meno ya kuuma kwa mfano, ajali iliyotokea Ziwa Victoria ilionyesha jinsi Taifa hili halina uwezo leo miaka imepita lakini hakuna maandalizi ya kuokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni suala linalohusu usafiri, usafirishaji katika maziwa na mito ndani ya nchi lazima sheria itoe miongozo ya kulinda maisha na mali za wananchi. Kwa kweli kiwango cha usafiri na usafirishaji katika maziwa na mito

ni chinbi sana na *at most it is a ruvugu match*. Sheria hii ingemulika zaidi na kusafisha sekta hii ya usafiri na usafirishaji. Sekta hii inaonekana inaendeshwa kama hakuna Sheria na wananchi (abiria) na bidhaa zao hawana haki kabisa. Sheria hii iimarishe na ifagie uchafu nyumbani kwanza usafiri na usafirishaji katika maziwa na mito iwe kioo cha Taifa katika Sekta hii ya usafiri, usafirishaji na biashara ya meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada huu wa mwaka 2003.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Kwanza nakupongeza sana kwa kuleta Muswada huu muhimu wa usafiri wa majini.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ukaguzi wa meli ufanyike mara kwa mara kabla ya kuanza safari ili zisilete madhara kwa abiria. Meli zote mbovu siziruhusiwe kutembea au kusafiri majini ili kuzuia hatari zinazoweza kutokea majini na kuleta maafa makubwa kwa abiria.

Pili, meli zisiruhusiwe kubeba abiria au mizigo mizito kuliko uwezo wake hii ni hatari kwa abiria na mizigo. Meli zimekewe muda maalum wa kutumika au kusafiri zikianza kuchakaa zipigwe marufuku kusafiri na zinunuliwe meli mpya ili kuepusha ajali nyingi ndani ya maji, bandari na maziwa. Wenye meli wasijali biashara na kupata faida tu, pia wajali abiria na mali zao. Usalama na ulinzi ndani ya meli ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa Muswada huu.

Pamoja na pongezi hizo naomba ufanuzi ni kwa kiasi gani mahitaji maalum kwa wasafiri kama wazee, watu wenye ulemavu na wajawazito yamezingatiwa kuwa ni moja ya sifa kwa mwenye meli kupata usajili na leseni pamoja na sifa zilizoainishwa katika sehemu ya IV, ibara ya 13 kipengele (1)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kuwa endapo hilo halikuwepo, yafaa lizingatiwe kwenye Kanuni zitakazotungwa kutokana na Sheria hii. Baada ya uchangiaji huo naunga mkono hoja.

MHE. MARGARETH J. BWANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na wote waliochangia kwa namna moja au nyingine kwa lengo la kuboresha Muswada huu. Napenda kutamka kuwa, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha Muswada huu, napenda kuzungumzia mambo yafuatayo:-

Bandari zilizoko katika Ziwa Tanganyika naomba zifanyiwe maboresho ili ziweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi nchini hususan bandari ya Kasanga, Karemo na Kasiva.

Kuwepo na *speed boat* ambayo itatumika kufanya doria kwa lengo la kuimarisha ulinzi katika ukanda wa Ziwa Tanganyika. Hivi sasa kuna vitendo vingi vya uhalifu vinavyofanyika katika ukanda huu. Je, ni lini *speed boat* hiyo itakuwa imenunuliwa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe matumaini ya ununuzi wa boti hiyo.

Tunaomba Serikali ifikirie kununua meli mpya ya kisasa itakayohudumia wananchi wa ukanda wa Ziwa Tanganyika. Aidha, kuwepo pia na boti zitakazobeba abiria, magari na mizigo. Wizara iweke utaratibu wa kuratibu na kufanya ukaguzi wa meli hizo mara kwa mara japo mara moja kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wa Wizara husika kwa ujasiri mkubwa wanaofanya kuleta Bungeni mikataba kadhaa ya kimataifa kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mikataba hiyo ni ya siku nyingi na imekuwa imelala bila kuchukuliwa hatua zozote za kuridhiwa au kutoridhiwa na Bunge kufuatana na Kanuni zilizopo. Kwa lengo la kuboresha sheria kongwe ambazo zimepitwa na wakati, Wizara hii kwa ujasiri mkubwa inafanya marekebisho ya kuboresha sheria hizo na kuzingatia kuainisha sheria hizo na mikataba ya kimataifa inayoendana na sheria zetu mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ningeomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi juu ya bandari yetu ya Dar es Salaam kutokuwa na vifaa vya kutolea uchafu kutoka kwenye meli na kwa msingi huo basi meli hizo zinatolea wapi uchafu, hasa meli ambazo zinatia nanga bandari ya Dar es Salaam moja kwa moja bila kupitia bandari nyingine, hasa meli za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wafanyakazi wengi wa meli hukaa baharini muda mrefu kabla ya kufika nchi kavu na kupata nafasi ya kutoka na kuingia mitaani, je, Muswada huu mpya unasema nini kuhusu tabia mbaya za uasherati unaofanywa na wafanyakazi hao wageni ndani ya nchi yetu hali ambayo inachangia sana kueneza magonjwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli nyingi za biashara na hata za kijeshi zinatambuliwa kwa bendera ya Utaifa wake na pia kwa jina la meli yenye hata hivyo suala la kuwepo kwa jina la meli sioni kama limelitiliwa umuhimu wake ndani ya

Muswada huu. Ningeomba ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri juu ya umuhimu wa kuwepo kwa jina la meli kwa meli zote zinazoingia nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kikamilifu Muswada huu.

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kutayarisha Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu naelekeza kuhusu usafiri wa bandarini, kwa kipindi kirefu sasa usafiri wa baharini kutoka Dar es Salaam kwenda Pemba una matatizo. Zamani ilikuwepo boti maalum iliyokuwa inaondoka Dar es Salaam moja kwa moja mpaka Pemba, lakini sasa usafiri huu haupo. Kwa nini Serikali haichukui hatua ya kutafuta boti nyingine yenye mwendo wa kasi ya kila siku ili iwaondolee usumbufu wananchi, Serikali inatoa kauli gani kuhusu jambo hili.

Ushauri wangu ninaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili itatue masuala ya usafiri wa boti inayokwenda kwa kasi kutoka Dar es Salaam mpaka Pemba. Safari hizo ziwe za kila siku kama ilivyo kuwa siku za zamani.

Baada ya maelezo hayo naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Muswada wa *Merchant Shipping Act, 2003* ambayo ndiyo hoja ya Bunge lako Tukufu leo.

Kwanza, naomba nimpongeze sana Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Watendaji wote kwa juhudini zao za kuandaa Muswaada huu.

Mimi kwa kuanzia naomba nipate ufanuzi wa mambo yafuatayo:-

Nashindwa kuelewa kichwa cha au jina la Muswada huu ninapousoma kwa lugha ya Kiswahili halafu tafsiri yake kwa lugha ya Kiingereza, kwa mfano, *Merchant Shipping Act, 2003* yaani Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Majini wa mwaka 2003. Tafsiri hii haiko sahihi. Naomba maelezo.

Mapendekezo ya Wizara kwenye Muswada huu kuna maeneo mengi ambayo yameachwa nje. Lakini pana eneo ambalo linampa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwamba atajazia vingine kwenye sheria kwa kutunga sheria ndogo ndogo na kanuni mbalimbali. Je, usafiri kwenye maeneo mengine ambayo siyo ya baharini yaani *Inland Waters* kama maziwa yetu, mito yetu na kadhalika. Sheria inasemaje kwenye hili?

Kwa vile shughuli ya usafiri wa majini, unaweza kuhusisha watu na vyomb o vingi ambavyo usimamizi wake unafikia ngazi ya kuunda unoja wa shughuli hii kama vile kuunda ushirika au umoja wa watu hawa. Sheria yetu hii inatoa nafasi gani ya kuwaruhusu au kuwapa nafasi ya kuungana kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kupata maelezo kwenye maoni yangu na nitafurahi sana kama yatapokelewa. Mimi naunga mkono hoja hii.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Wataalam wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuanda Muswada huu mzuri ambao umekubali kuleta mabadiliko mengi katika Muswada wenyewe. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Waziri ni kusimamia kwa dhati meli zinazobeba mafuta kwa sababu ya athari za mazingira yetu. Mara nyingi meli huvuja wakati zikiwa safarini , utaalamu wa kugundua hali hii upewe kipaumbele kufuatana na *Internatinal Convention or Civil Liability for Oil Pollution Damage* ya mwaka 1992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia umuhimu wa Waziri kupewa madaraka ya kuteua Bodi ya Usalama kwa vyombo vya majini. Lakini pamoja na kusema kuwa anaweza kuteua chombo hiki kwa kuzingatia Kifungu 4(i) cha Sheria hii. Tatizo ni *Public Institution* gani ambayo Mheshimiwa Waziri anaifikiria katika kutamka bayana katika Sheria. Kwa nini Mheshimiwa asiunde chombo *independent* ambacho kinajumuisha *public* na *private institutions* kwa pamoja ili kuwe na uwakilishi mzuri kutokana na upeo mkubwa unaoweza kupatikana toka nje ya *public institutions*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya baharini ni vizuri ikafafanuliwa vizuri kwa pande zote zinazohusika kwa nchi tunazopakana ili kuwepo maelewano wa pande zote zinazohusika na kuona jinsi ya kujenga mahusiano ya kiuchumi, kimazingira na kiusalama. Lazima pawepo na mikakati ya kuhakikisha kuwa usalama wa meli unapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli zetu nyingi zilizomo kwenye maziwa yetu na bahari zetu, ni budi ziwe zinakaguliwa kila bada ya miezi kadhaa, ukaguzi ni budi ukafanyika kwa ushirikiano wa wataalam wetu na wataalamu wa kutoka nje ya nchi. Hii itapunguza mwanya wa majanja wa kutaka kulipualipua kazi kwa kutegemea kulipwa chochote (rushwa) ili kupitisha kibali kwa meli zinazomilikiwa na watu binafsi. Hii tunaiomba ili iwe kama safety value ya kukwepa jambo hili lisitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono asilimia mia moja.

MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Katika Muswada huu mambo yafuatayo yapewe umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo hivyo ni pamoja na vyombo nya kufikisha abiria nchi, maboya kwa tahadhari wakati wa dhoruba, upotetu wa mali za abiria uangaliwe upya na fidia ya abiria atakayepoteza maisha yake ijulikane. Ni vema watumishi wote wa meli wajue kuogelea kwa muda mrefu. Meli ya Liemba ni muhimu ipanuliwe au iboreshwe.

MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Mashirika na wafanya kazi wote wa Wizara hii ambayo ni moyo wa maendeleo ya nchi yetu katika kuleta mabadiliko makubwa ya teknolojia ya kisasa.

Nimetumwa na wananchi 240,000 wa jimbo la Rarya Wilaya ya Tarime kufikisha pongezi na shukrani zao kwako wewe Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomosya, kwa uzalendo, upendo na huruma yako kwao kwa kuwatemebelea na kufanya mikutano nao. Wanakupongeza wewe kwa mapinduzi makubwa ya kiuchumi uliofanya wa kutoa agizo la kukarabati bandari ndogo ya Soto ambayo ilikuwa haifanyi kazi kwa muda wa zaidi ya miaka thelathini.

Napenda kutoa taarifa kwako kuwa ukarabati wa bandari ndogo ya Soto umekamilika na meli kubwa kutoka nchi za jirani zimetia nanga mara nne Soto. Wananchi wameniomba umfikishie Ndugu Kiondo, Mkurugenzi wa Kanda ya Ziwa, pongezi na shukrani zao kwa kazi nzuri aliyoofanya pamoja na mafundi wake. Wanaomba Ndugu Kiondo, apewe hati ya shukrani kwa kazi nzuri.

Bandari ndogo ya Kinesi, jana niliongea na viongozi wa Tarafa, wamenihakikishia kuwa kazi ya ukarabati inaendelea vizuri na mafundi kutoka Mwanza wako kazini. Ukarabati utakamilika baada ya wiki mbili hongera sana. Baada ya shukrani za wananchi wa jimbo la Rarya na shukrani zangu napenda kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha na kuimarishe Muswada kama ifuatavyo:-

Serikali ya Ufarasa kwa kushirikiana na *IMO* itatoa fedha kwa lengo la kuimarishe usalama katika Ziwa Victoria yaani kwa ajili ya *Navigational Aid* pamoja na *Hydrographic Survey* kwa ajili ya mipaka.

Pendekezo, Tanzania iwe Makao Makuu ya kufanya utafiti huo kutokana na ukweli kuwa asilimia kubwa ya maji ya Ziwa Victoria iko Tanzania. Bandari nyingi ziko Tanzania.

Ili kuboresha na kuimarishe usalama wa bandari ndogo ya Soto, wananchi wa Jimbo la Rarya wanaomba bandari ya Soto ipatiwe umeme. Umeme umefika Shirati na kutoka Shirati hadi Soto si mbali.

Kuhusu uteuzi wa wajumbe wa Bodi, napendekeza, Mkurugenzi ambaye atateuliwa kusimamia usafiri wa meli katika maziwa na mito awe Mjumbe.

Nakushukuru na kukupongeza sana kwa kuleta Muswada huu kwa wakati, ijapokuwa umechelewa sana. Naunga mkono mia kwa mia moja hoja.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchuzi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na wataalam wa Wizara kwa Muswada mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja tu napenda kulitoa. Bandari zetu, ni hazina kubwa zeny uwezo mkubwa wa kutupatia mapato. Lakini kwa sasa mapato yake ni madogo sana kutoptana na utendaji hafifu, tija ya chini sana na urasimu mkubwa. Hali hii inawafanya wasafirishaji wengi kuhamisha bidhaa zao kupitia Mombasa, Kenya na bandari za *Mozambique* na *South Africa*. Naomba turekebishe hali hii. Ahsante.

Kuhusu utendaji kazi wa bandari zetu. Suala la ushindani kati ya bandari za mwambao wa Afrika Mashariki na Kusini linalelewka na Mamlaka ya Bandari pamoja na kampuni ya *TICTS* inayotoa huduma katika kituo cha Kontena Dar es Salaam. Hivi sasa kituo cha Kontena ndicho chenye ufanisi na tija ya juu kushinda bandari zote.

Vile vile kutoptana na ufanisi mzuri ulioko katika bandari ya Dar es Salaam shehena ya shaba kutoka Zambia hupitia Dar es Salaam takriban asilimia 65shehena inayohudumiwa katika bandari zetu inakua kwa 3% na kutoptana na hali hiyo mapato yamekua pia. Ili kuendelea kunatibu na kudhibiti hali ya ushindani mbinu za utafutaji masoko (*marketing strategies*) zinafanyika kwa bidii kubwa kwa pamoja na wadau wengine waliopo katika mlolongo wa usafirishaji bidhaa nchi kavu.

MHE. ABDULA S. LUTAVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na hasa Mheshimiwa Waziri Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Katibu Mkuu na wote maafisa wa Wizara ambao katika ngazi mbalimbali wamesaidia na kuuandaa Muswada huu. Ni kazi nzuri iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umezingatia na kurekebisha mapungufu ya dhahiri ya Sheria 43, 1967 kwa mfano kwa sheria hii sasa bima kwa vyombo (meli) na kwenye mito na maziwa yetu siyo tena suala la *business prudence* ni sharti la kisheria. Hii ni hatua njema hata kwa biashara kwa vyombo vitakavyosajiliwa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada umetambua pia umuhimu wa kudhibiti uchafuzi wa mazingira majini. Ikipitishwa sheria hii pia kutakuwa na taratibu zinazolelewka kudhibiti usalama wa vyombo, mali, maisha ya abiria au watu na mazingira kwenye maziwa na mito yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inayo zaidi ya kilomita za mraba 54,000 za maji ya maziwa na mito inayopitika. Ukipita Muswada huu kutakuwa na sheria inayoonyesha kutambua umataifa wa maziwa na mito yetu hiyo ambayo karibu yote matumizi yake yanahusisha pia nchi majirani zetu (nchi tunazopakana nazo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaaminika kwamba pamoja na maendeleo makubwa yaliyotokea katika teknolojia ya uundaji meli bado zaidi ya 95% ya ajali za baharini (zilizofanyiwa uchunguzi) zinachangiwa na makosa ya kibinadamu (*Human error*). Mkataba wa kimataifa *STCW* 78 ulirekebishwa kwa kutambua umuhim u wa kuboresha *competence* ya mabaharia, ikapatikana *STCW* 95. Muswada huu ni moja ya jitihada za nchi yetu kutekeleza matakwa ya marekebisho hayo (*STCW* 95). Na hivi leo tayari Tanzania imeshaorodheshwa kwenye *White List* ya *IMO* kwa kutambuliwa uzito tuliuweka kwenye sekta ya mafunzo ya mabaharia na kudumisha viwango vya ubaharia. Haya siyo mafanikio madogo, lazima hali hii idumishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Muswada wote huu usingeundwa kama siyo haja ya kuboresha usalama wa usafiri na usafirishaji majini ikihusisha mali, maisha, vyombo pamwe, na mazingira ya majini. Utekelezaji wake utatulazimisha kuweka mifumo thabiti katika maeneo muhimu ya *shipping*, *Uvuvi Port State Control, Offshore drilling, maritime safety*, udhibiti wa uhifadhi wa mazingira majini, *maritime search and Rescue*, usimamizi wa mafunzo na maendeleo ya mabaharia wa Kitanzania pamoja na kuweka na kudumisha *Registry* ya Tanzania yenye hadhi, heshima na kukubalika katika jamii ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya ni makubwa na yanayojitegemea. Kwa maana ya mikataba ya Kimataifa ya *IMO* inayoguswa na utekelezwaji wa sheria hii (ikipitishwa) ipo isiyopungua mikataba 50 hivi sasa na ili kujiwekea na kudumisha heshima inayotarajiwa kwa hatua hii ya kutunga sheria hii mpya nchi yetu inawajibika kuhakikisha ufanisi wa hali ya juu katika kusimamia utekelezwaji wa sheria hii. Itatusaidia zaidi, kama usimamizi unaohitajika katika sheria hii utawekwa chini ya chombo makhsusi kitakachoundwa maalum kwa ajili hiyo. Hili ni muhimu ukikumbukwa uhalisi wa mambo kwamba mbali ya vyombo, mali na raia wa Tanzania sheria hii itahusisha pia vyombo, mali na raia wa nchi zingine kutokana umataifa wa sekta senyewe, viwapo ndani ya ukanda wa maji wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia uchanga wa sekta hii nchini ningependekeza viwekwe vivutio kwa maeneo kadhaa ya uchumi wetu. Tunahitaji msamaha wa kodi kwa uagizaji au uingizaji wa mali zenyewe, ziwe za abiria au mizigo angalau kuanzia ukubwa fulani utakaokubalika (kwa mfano 400grt na kuendelea). Ingefaa tozo kama *VAT* zisihuishwe katika uagizaji wa vitu kama injini za meli, vipuri vyake, vifaa vya usalama majini, vifaa vya kuokolea, vifaa vya mawasiliano nchini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana wazo linalojitokeza kwenye Muswada huu kuhusu jinsi ya kushughulikia *stowaways* na suala zima la utekaji nyara wa meli *marine piracy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kwa Muswada huu kuanzisha *Maritime Education and Training Fund*, nina matumaini makubwa kwamba mfuko huu utapewa nafasi ya kuwapo na kufanya kazi inayotarajiwa, ingawa ikumbukwe kwamba mfuko wa

aina hii iliwahi kubuniwa chini ya Sheria Na. 3 ya *CFB*, 1981 hatujaona matokeo na mafanikio yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifarijika mno nilipoona kwenye rasimu ya Muswada huu kwamba kinyume na ile Sheria 43, 1967 matumizi ya sheria hii mpya yangehusisha pia Zanzibar. Busara ilitawala mtazamo huu hasa ikizingatiwa kwamba mikataba yote ya kimataifa inayolengwa kutekelezwa na Sheria hii iliridhiwa au ili sainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kwa ushiriki wa Zanzibar).

Lakini kama hadi katika hatua hii ya kufikishwa Muswada kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano, bado kunahitajika kuendeleza mashauriano na Serikali ya Mapinduzi inaleta fadhaa na mashaka juu ya uelewa uliopo kwa pande mbili hizi za Muungano wetu kuhusiana na umuhimu wa kuwa na sheria ya pamoja juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii muhimu sana kwa maendeleo ya sekta hii ya usafiri na usafirishaji majini katika nchi yetu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu ya Sheria ya Usafiri Majini.

Kwanza kabisa napenda nitoe pole kwa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wote wale ambaao walifiwa na wazazi wao na wapendwa wao wa karibu tunawaombea roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin*.

Natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge ambaao walipata matatizo mbalimbali Mwenyezi Mungu awaponeshe haraka ili tuweze kumaliza nao kipindi hiki kilichobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Mimi kama Mzanzibar naamini ndugu zangu wa Zanzibar watapata muda wa kutafakari Muswada huu na kuona wapi wangependa tuwe nao pamoja kwa manufaa ya pande hizi mbili. Wizara iko tayari kushirikiana nao katika kusaidia kufanikisha yale yote ambayo yatakuwa ya manufaa kwoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nitachangia na kujaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kadhaa katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza masuala yote yanayohusu ajira, utumishi, likizo, afya za Mabaharia, watu wanaopata dharura baharini na Bima. Mengine ni mambo yanayohusu uhusiano kati ya vyombo vya majini na Bandari ni vipi Muswada huu unawalinda wenye vyombo vidogo vidogo kama meli ndogo ndogo, mitumbwi, majahazi na kadhalika. Pia kuhusu meli ya mafuta iliyoungua kule Musoma na namna ya kushughulikia meli mbovu na mabaki, vifaa vya kupokelea uchafu na mengine kama muda utaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la utaratibu wa kuajiri wafanyakazi melini. Muswada huu unalenga kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanakuwa na mikataba

mizuri ya kazi na mkisoma kifungu 111 mtaona kinaleza wazi shughuli za Mabaharia kuanza au kuacha kazi kwenye meli za Tanzania itasimamiwa chini ya Msajili wa Mabaharia.

Aidha, Msajili wa Mabaharia atakuwa na kumbukumbu za Mabaharia wote wanaofanya kazi katika meli za Tanzania au wanaomba kazi kuitia kwake au waliowasimamia kuacha au kuanza kazi. Hakuna Taasisi au mtu atakayeruhusiwa kuchukuwa Watanzania kwenda kufanya kazi kwenye meli ya Tanzania au nje bila ya kuwa na leseni kutoka kwa Msajili wa Mabaharia inayoruhusu kufanya hivyo. Kwa mfumo huo Muswada unaweka njia au kumwezesha Msajili wa Meli au chombo husika kusaidia Mabaharia kupata kazi nje na ndani ya nchi kwa kuwa na Mikataba mizuri. Mkataba huu unawalinda sana Mabaharia kuona haki zao. Mkisoma kifungu 111 ukurasa wa 76 na 77 kinajieleza wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, jana lilizungumzwa suala la ajira ya Wanawake, napenda niseme kwamba kiutamaduni sekta hii inamilikiwa na wanaume kwa miaka mingi. Lakini sasa hali imeanza kubadilika nitatoa mifano machache katika *Marine Service Company Ltd.* tunaye Mwanamke ambaye ni Mhandisi Mkuu Msaidizi, Chuo cha Bandari tunaye Mkufunzi mwanamke ambaye ni *Marine Engineer* ingawaje hivi sasa yuko Norway anasomea Shahada ya Kwanza katika fani ya *Naval Architecture*. Tunaye Mkufunzi mwengine wa *Computer Science*. Pale Wizarani tunao wataalamu wanawake wengi tu.

Tuna Mkurugenzi Msaidizi wa Usafiri Majini ambaye ndiye anayesimamia hasa masuala haya ya usafiri majini na ni mwanamke. Wanasheria wa Wizara ni wanawake, Afisa Usafirishaji ni mwanamke, Afisa Usafirishaji wa *Maritime Adminstration* ni mwanamke vile vile. Mamlaka ya Bandari tunao wanawake 3 katika Wakurugenzi saba.

Napenda tu niwakumbushe kuwa *gender* inashughulikiwa ipasavyo kwenye Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Hivi sasa ukichukua *in general* ukiacha masuala ya *Marine, Director General* wa *Civil Aviation* ni mwanamke na aliyejewa *MD* wa *TTCL* alikuwa ni mwanamke sasa yuko *ITU*. Ni hayo machache naweza kuchangia kwa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira ya watoto Muswada huu umezingatia kwa maana ya kudhibiti ajira ya watoto katika vifungu vifuatavyo. Kifungu 120 ambacho kinazungumzia, “*No person under the age 18 shall be employed in Tanzanian Ship,*” isipokuwa kwenye meli za mafunzo zitakazopata kibali cha Waziri au pale Msajili wa Meli ameridhika kwamba afya na maumbile kwa faida yake anaweza kuajiriwa. Tunazo meli ambazo zina *library*, meli kama zile wanaruhusiwa watu wenye umri kidogo chini kufanya kazi. Kifungu cha 169 pia kimetamka hakuna mtu chini ya miaka 18 atakayeajiriwa kwenye meli za Kitanzania mpaka awe ameruhusiwa na kanuni zinaleza mazingira yanayoruhusu ajira hiyo kufanyika. Kwa hiyo, hili nafikiri limejieleza wazi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililojitokeza ni Kampuni gani za Bima nchini zinazoweza kutoa Bima za Meli. Bima za Meli ziko za aina nyngi, ziko kubwa ambazo zinawekewa *hull* na *machinery*. Ziko zile Bima za Mizigo na *Protection and Indemnity* pia kuna Bima ya kupoteza mapato kutokana na hayo ni kawaida kwa wenyewe meli kuwa na Bima mbalimbali na Taasisi tofauti.

Katika nchi yetu yako Mashirika ya Bima yanayohusika na Bima za Meli. Lakini kwa vile Bima za aina hii uhitaji malipo hususan katika fedha za kigeni Mashirika na Kampuni zetu za Bima hutumia njia ya *Reinsurance* ambapo *Underwriters* wanakuwa na Kampuni ya Kimataifa kwa mfano Mamlaka ya Bandari na Kampuni ya Huduma za Meli imeviwekea vyombo vyake vya Majini Bima kwa njia hiyo. Hata hivyo ni bora kwa wenyewe meli kuzingatia kukata Bima inavyostahili kufuatana na shughuli zake.

Muswada huu unasisitiza malipo kwa waathirika wengine yaani *third party* hivyo kwa kuzingatia ukubwa wa malipo yanayoweza kutolewa ni bora mwenye meli kuwa na Bima kadhaa kwa ajili ya athari mbalimbali zinazoweza kujitekeza katika shughuli za meli. Hapa napenda tu niunganishe na lile la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, watu wanapopata madhara baharini watapataje haki zao. Sheria hii inaweka bayana kwamba kila mwenye meli anatakiwa akate Bima ya Mali na abiria kifungu 11 kinajieleza wazi. Kifungu 160 pia kinatoa fidia kwa Baharia aliyekufa kazini. Kama yote yanafanyika bado mtu akaona hatendewi haki uhuru unatolewa kwa mtu huyo kudai haki yake Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la afya ya Mabaharia na kulikuwa na mawazo kwamba unapomwajiri mtu ukampima na ukamkuta yuko *okay* lakini yuko kwenye *transition period* mfano ana Ukimwi lakini kama hukumpima tena katikati, pale anaweza maradhi yale yakajitekeza. Lakini nimsisitizie tu Mheshimiwa Dr. Lucy Nkyia, kanuni ambazo zimewekwa kusimamia ukaguzi wa afya ya Mabaharia zinashughulikiwa ipasavyo. Taratibu zinataka Baharia apimwe afya yake kabla ya kupanda melini na pia zinataka abiria apimwe afya yake kabla ya kupata cheti na kufuzu mafunzo na taratibu pia zinataka Baharia apimwe afya yake na Daktari ameteuliwa na Serikali kwa madhumuni haya. Tangu tuanze shughuli hizi sisi hatujapata malalamiko yoyote lakini kama yapo tuko tayari kuyashughulikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uhusiano kati ya vyombo vya majini na shughuli za Bandari liliulizwa jana. Mimi nasema upo uhusiano mkubwa sana kati ya vyombo vya usafiri majini na Bandari. Kwa mfano, Bandari ni kituo na ni mahali penye Miundombinu inayounganisha usafiri wa majini na wa nchi kavu. Bandari hutoa fursa ya kuwepo huduma zinazoweza kuegesesha vyombo hivyo na kupatikana huduma mbalimbali. Uhusiano wa vyombo vya usafiri majini na bandarini ni wa Kibiashara kwa hivyo kuwekeza Miundombinu katika bandari huzingatia misingi ya matakwa ya Kibiashara kwamba wawekezaji hujilipa pamoja na faida. Shehena inayohudumiwa bandarini ndiyo mgodi wa biashara yenywewe. Shehena ipitayo humu takriban asilimia 70 nchini ni ya kwetu na asilimia iliyobaki ni ya nchi jirani. Hasa shehena zinazopita Bandari ya Dar es Salaam. Lingine ni kwamba baadhi ya shughuli za kibiashara katika

Bandari hutoa huduma na matengenezo ya meli kama *Dock yard ship repair* tunayo Mwanza na hata Dar es Salaam tunayo ingawaje bado haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililojitekeza ni kwamba ni hoja ni vipi Muswada huu unavilinda vyombo vidogo vidogo kama meli, mitumbwi, majahazi vinapogongwa na meli kubwa. Muswada huu unatamka wazi kuwa Mheshimiwa Waziri atatunga kanuni ya kuepusha kugongana Baharini na katika kutunga kanuni hizo atazingatia kanuni za Kimataifa zinazozua kugongana. Iko *Convention* ambayo tutaileta Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni. Hii ni kwa sababu vyombo vyote duniani vinapaswa kutumia kanuni zinazofanana ili kutoruhusu kugongana kwa sababu tofauti ya kanuni zinaweza zikaleta athari.

Aidha, katika kanuni hizo vyombo vidogo vinapewa upendeleo wa kupishwa na meli kubwa. Kama meli itagonga chombo kidogo basi kuna uwezekano mkubwa kuwa meli itakuwa katika makosa. Hata hivyo, vyombo vidogo pia vinapaswa kuchukua tahadhari na hatua kuonyesha kuwa wapo na wapo Baharini usiku kwa kuweka taa. Gharama za kufidia uharibifu huchangiwa zaidi na meli iliyoshindwa kufuata kanuni za kuzuia kugongana. Hivyo meli inapogongana na chombo kidogo itawajibika zaidi kwani inapaswa kupisha chombo kidogo. Hivyo kanuni za Kimataifa za nchi zinalinda vyombo vidogo vidogo na nina hakika wenye mitumbwi wanaovua kule Kigoma kwa Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou watazingatia masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na suala la kuungua kwa meli katika Bandari ya Musoma ambayo aliileta Mheshimiwa Marwa. Nakubali suala hili lilijitokeza tarehe 26 Januari, 2002. Meli hii ilikuwa imeandikishwa Kenya kwa jina la *MT Sukumani*. Wizara iliunda Tume na ripoti ilitolewa na ilionyesha kwa meli hiyo ilikuwa na mapungufu makubwa ya ujenzi wake pamoja na vifaa vya kupakulia mafuta vilikuwa hafifu. Tume iliyoteuliwa ilitoa mapendekezo yake ambayo yote yalizingatiwa na Wizara napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bado majadiliano unaoendelea mwenye meli ili aweze kulipa fidia na kama tukishindwa basi *Marine Services* watampeleka mwenye meli Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililoletwa na Mheshimiwa Herbert Mntangi, ni swali, kwa nini meli za kigeni haziandikwi majina kwenye meli. Kwa kweli kutokana na taratibu za Kimataifa meli zote ziwe za kigeni au zilizosajiliwa hapa nchini zinatakiwa ziwe na bendera ya nchi iliyosajiliwa pamoja na jina la meli ambalo lipo kwenye *particulars* za meli wakati inasajiliwa. Meli zinazoingia nchini zinatakiwa ziwe na jina ambalo linakuwa limeandikiwa ubavuni mwa meli. Iwapo meli yoyote itajitokeza bila ya kuwa na jina tunaweza tukaitilia shaka mara moja na tunayo sababu tu ya kuikagua. Tunayo haki ya kuikagua na kujua sababu za kutokuonyesha jina la meli hiyo. Kwa hiyo, taratibu hizi zinaturuhusu kufanya hivyo na meli yoyote inatakiwa iwe na jina ubavuni mwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo alitupa Mheshimiwa Nimrod Mkono, ni namna ya kushughulikia meli mbovu na mabaki. Tuseme tu kwa sasa hivi hakuna mkataba wa Kimataifa unaosimamia uondoaji wa meli mbovu na mabaki.

Tukipitisha Muswada huu tutakuwa tumekamilisha kazi hii ipasavyo. Lakini ile Kamati ya *Legal Committee* ya MO iliendelea kujadili rasimu ya Mkataba wa kuondoa meli mbovu katika kikao chake cha Oktoba, 2003.

Kwa hiyo, tukisema tumeridhia Mkataba huu mimi naweza kusema kwamba si sahihi kwa sababu mpaka sasa hatujauridhia lakini tukipitisha hizi sheria na tunesoma kwenye sheria, *Lakes* zinavyoshughulikiwa katika sheria hii. Lakini tukumbuke na tena niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba mabaki hayo yatakuwa na umri wa miaka 100 ndani ya maji basi kuna sheria yake ambayo inatakiwa ishughulikie inaitwa *The UNESCO Convention on the Protection Under Water Cultural Heritage*. Vile vitakuwa ni vitu tunaitaje *Cultural Heritage* vya kuwekwa kwenye urithi niseme kama mabaki yanabaki kwenye meli iliyozama ndani ya bahari kwa miaka 100 na hatukuwahi kuyashughulikia, yatashughulikiwa chini ya sheria hii niliyoisema ya *The UNESCO Convention on the Protection of Under Water Cultural Heritage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilichangie ni lile ambalo aliloliulizia Mheshimiwa Herbert Mntangi la vifaa vya kupokelea uchafu yaani *Reception facilities*. Nakubaliana naye kwamba ni kweli Bandari zetu zote zikiwemo Bandari ya Dar es Salaam hazina vifaa vya kupokelea uchafu unaozalishwa melini yakiwemo mafuta machafu. Sababu kubwa ya kutokuwa na vifaa hivyo ni gharama kubwa inayohitajika wakati ujenzi na namna ya kuhudumia baada ya ujenzi.

Hata hivyo kuna mipango mahsus ya kuwa na vifaa hivyo kwa kuanzia na Bandari ya Dar es Salaam na suala la kupokelea vifaa, uchafu limesisitizwa kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Uzuiaji wa Uharibifu wa Mazingira yaani Muswada huu si bado hatujauridhia lakini uko njiani kuletwat katika Bunge hili Tukufu ili tuweze kuuridhia. Muswada huu unatoa mwongozo wa aina gani ya vifaa vinavyotakiwa na namna ya kuviveka na kuvihudumia ili vikidhi viwango vinavyobainishwa kwenye Mkataba. Mkataba huo unashughulikiwa kwa ajili ya kuletwat Bungeni kama nilivyosema ili uweze kuridhiwa. Jana Mheshimiwa Waziri aliorodhesha katika hotuba yake Mikataba ambayo tumeiridhia na Mikataba ambayo iko njiani ikishughulikiwa kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, alizungumzia kifungu 160 na akataka kifungu hiki kirekebishwe. Napenda tu nimkumbushe tu kwamba kifungu 160 kimerekebishwa kwa kuondolewa kwa neno: “*To imprisonment for a time not exceeding five years or both.*” Kwa hiyo, hii phrase imefutwa na nafikiri na yeche atakuwa ameridhika nayo. Lingine labda ni lile alilolizungumzia Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou kwamba Tanzania ni kweli. Katika ushindani huu wa biashara sheria yetu haitopaswa kuwa ngumu kuwafanya wabebaji watuchoke na wakimbia.

Mimi naamini katika hizo kanuni atakazozitunga Mheshimiwa Waziri *nita-take into consideration* masuala hayo. Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, mawazo yako tumeyachukua ya kuyafanyia kazi tutayafanyia kazi, lakini niseme kwamba jukumu la kusimamia masuala ya usafiri majini kule Kigoma. Serikali ipo Kigoma na inayo uwezo kwa sababu mimi nasema Serikali ipo pote ndiyo maana tuna Mkuu wa Mkoa, tuna Afisa Usalama, Afisa wa Polisi wa Mkoa kwa hivyo Ziwa Tanganyika linashughulikiwa

ipasavyo Mheshimiwa Mbunge na tunazo boti pale wewe ni shahidi inapotokezea dharura hata kabla ya wewe hujatukuambia zinafanya hizo shughuli. Lakini kama kuna suala la kwamba meli hizi wananchi wanachangia wanaohusika wamesikia na nina hakika watalifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ya Kigoma Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, kuna mradi ule wa *Lake Tanganyika Development Programme* chini ya *UNDP*. Lakini nafikiri uko kwenye *initial stage* na tutapata nafasi ya kuzungumza na wewe kuona mradi ule kwa upande wetu unahu nini kwa sababu ni *Multi-sectoral*. Alivyoniambia anayehusika ni kwamba anashughulikia kutafuta fedha ili aweze kuukamilisha ipasavyo. Maboti yanayotengenezwa yenye uzito wa zaidi ya *60 tonnes* sheria hii nafikiri ita-take care. Kwa hiyo, wanatakiwa wawawekewe Bima, mali na abiria wanaochukua katika maboti yale.

Mheshimiwa Samwel Chitalilo, tunakubali yote uliyotupa na tutayafanya kazi na wale wanaohusika na wao pia wamesikia na nina hakika watayashughulikia ipasavyo. Kwa sababu muda nilioupati mimi ni mchache napenda nichukue nafasi hii niwashukuru wataalam na Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao adhimu ninaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana nao katika kuona kwamba utekelezaji wa sheria hii hauwi ni kikwazo kwa wananchi au kwa kutoa huduma zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ya kina ambayo inatusaidia katika mambo yafuatayo. Inatusaidia katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ambayo tumekabidhiwa, vile vile inatusaidia katika maandalizi ya kanuni, taratibu na sheria ndogo. Michango ya Waheshimiwa Wabunge inatusukuma tukamilisha kuridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa tukizingatia ushauri alioutoa Mheshimiwa Shekifu kwamba tuanzie na ile Mikataba ambayo ina manufaa kwa Taifa letu. Kwa hiyo, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mheshimiwa Mwenyekiti wao au Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo. Imeuchambua Muswada huu kwa kina kama ilivyoeleza katika ripoti yake. Muswada huu una sehemu 23 na vifungu 430 na vitaongezeka kama vitatu baada ya marekebisho ambayo tumeyaleta pale Bungeni. Kwa hiyo, ni Muswada mkubwa na Muswada wa kina sana lakini walikipitia kipengele kwa kipengele tumefaidika sana nawashukuru sana. (*Makofi*)

Naomba niwashukuru na vile vile niwatambue wale wote Waheshimiwa Wabunge waliochangia nianze na wale waliochangia kwa kusema nao ni 18. Waliochangia si wengine bali ni Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, ambaye alikuwa akimwakilisha Mwenyekiti wa Miundombinu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani na vile vile Waziri Kivuli wa Mawasiliano na Uchukuzi na naomba aendelee kubakia kivulini kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ali, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Samwel Chitalilo na mwishowe Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, kwa kuwa pamoja nami katika kusimamia majukumu mapana na makubwa sana ya Wizara hii. Nimefarijika sana kuwa karibu naye na wakati mwingine nasema sijui ningefanya nini bila yeye. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kuwatambua waliochangia kwa maandishi, wako kumi na moja, nao ni: Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Margareth Bwana na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kutoa maelezo kutokana na michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge hasa wale ambao vile vile ni Wanasheria waliobobeaa katika fani hiyo ya sheria. Nao si wengine bali ni Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Philip Marmo. Kwa lugha yao, pamoja na mimi kusoma vitabu vingi na kuwa Profesa bado sijamaliza kusoma, wao ndiyo wasomi (*learned brothers*) hawa. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa michango yao. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo napenda kusema kwa kifupi tu kwamba, mambo mengi aliyozungumza Mheshimiwa Philip Marmo ni ushauri mzuri tu ambao tunauchukua na tutauzingatia na kuendelea kutekeleza sheria hii mtakayopitisha wakati utakapofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nimrod Mkono, ye ye kama kawaida yake alituandikia mada au niseme hoja yenye kurasa zaidi ya 30, ameuchambua sana Muswada huu na kila wakati ninapowasilisha hoja Bungeni inayohusu Muswada wa Sheria ya Mawasiliano na Uchukuzi anakuwa ameusoma sana na ninadhani anafanya hivyo kwa Miswada mingine yote, lakini anatusaidia sana, tunamshukuru na napenda kusema kwamba tumeyazingatia aliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba dhima (*liability*) inayotokana na uchafuzi wa mazingira kutokana na mafuta tumeizingatia baada ya mchango wa Mheshimiwa Nimrod Mkono. Yaliyo katika mkataba husika aliouzungumzia na yale aliyotushauri yametufanya tuongeze vifungu viwili vipya, navyo

ni vifungu namba 378 na 379 kama inavyoonyesha katika orodha ya mabadiliko. Kwa hiyo, tunamshukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufidia upungufu iwapo gharama za kusafisha mazingira na hasara ni kubwa, tumezingatia aliotosaidia na vile vile tumezingatia yale yaliyo katika Mfuko wa Kimataifa alioutaja kwa kuongeza kifungu namba 380 kinachohusu *The International Oil Pollution Compensation Fund*. Kwa hiyo, tunamshukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Mheshimiwa Nimrod Mkono, amezungumzia yanayohusika na *The International Conventional on Maritime Liens and Mortgage* ya mwaka 1993, inayohusika na madai ya meli na uwekaji rehani wa meli. Ningombaa kumtaarifu Mheshimiwa Nimrod Mkono, kwamba bado Tanzania hatujaridhia mkataba huo, lakini tumezingatia mambo ya *lien* katika sheria hii tuyafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, suala la wadandiaji limezungumzwa na kwa uchungu sana. Ni kweli hawa *stowaways* ni tatizo la kijamii, ni tatizo la kiuchumi, ni katika kutafuta ajira katika kutapatapa na ni tatizo la Kitaifa. Lakini kutosa mzamiaji au wazamiaji ni kosa la jinai, ingawa kudandia meli vile vile ni kosa kwa mujibu wa sheria hii. Sasa, ukimtosa mdandiaji kama wewe ni mwenye meli, basi kwa mujibu wa sheria hii, sehemu ya 21 ya Muswada huu itatumika kama uko kwenye maeneo ya Tanzania. Vile vile, sheria ya makosa ya jinai itatumika kwa sababu ni sawa sawa na kujaribu kuua, au kama aliyetoswa amefariki basi ni mauaji, kwa hiyo ni kesi ya jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile, mdandiaji kama amepona anaweza akafungua kesi ya madai. Kesi hizi kwa maana ya Taifa na Taifa hasa kwenye maeneo ambayo yako mbali sana na eneo la nchi, basi Wanasheria huwa wanatumia hii *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act* na haya masuala yameainishwa katika Sheria ya Bahari ya Kimataifa (*The Law of the Sea*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtosaji ni kweli anatambua kwamba mdandiaji amekosea, lakini sheria inamtaka amrudishe alikotoka katika bandari inayofuata baada ya kugundua kwamba kuna mdandiaji na wala siyo kumtosa baharini na kama nilivyosema, kama tendo hilo limetokea katika eneo la Tanzania, basi ni kosa la mauaji au kujaribu kuua na kama ni nje ya eneo la Tanzania, basi Sheria za Kimataifa zitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadhani kwamba kwa kuwa na Msajili wa Mabaharia moja ya kazi zake itakuwa ni kuratibu masuala haya, kuwatafutia hawa vijana kazi, kuwaelekeza nini cha kufanya na kuratibu mawakala ambao wanawatafutia hao mabaharia kazi. Sheria hii itatusaidia sana na hicho cheo cha Msajili wa Mabaharia kitatusaidia sana katika kupunguza hili tatizo la udandiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetolewa ushauri kwamba tuangalie uwezekano wa kuhakikisha kwamba meli za mafuta zinazokuja zinakuwa na kuta mbili. Wengine wanasema kuta mbili na wengine wanasema ni magamba mawili (*double hull*). Ni kweli

hizi meli zenyne *single hull* ni hatari sana, mwaka jana zimemwaga mafuta mazito kwenye eneo la pwani ya Spain, imekuwa ni tatizo kubwa sana kusafisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, kikao cha 46 cha *Marine Environment Protection Committee* ya *International Maritime Organization (IMO)* kilichofanyika tarehe 23 hadi 27 Aprili, 2001 kimekwishatoa ratiba ya kufuta meli zote zenyne gamba au zenyne kuta moja (*single hull*). Ratiba iliyokubalika na *IMO* na sisi vile vili ni *part* ya *IMO* ni kuwa ifikapo mwaka 2015 au mapema kabla ya hapo meli zote zenyne gamba moja au kuta moja ziwe zimeshafutwa. Kwa hiyo, sisi tutatumia mwongozo huo katika kufuatilia utekelezaji wa hili suala la *double hull ships*. Ni kweli kwamba ingebidi hizi meli ziondolewe mapema iwezekanavyo, lakini zitavuruga sana biashara ya mafuta duniani ndiyo maana imechukuliwa muda ambao unawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu matumizi ya bendera za unafuu au usajili wa huria yaani *flag of convenience* au *open registry*. Hizi ni bendera ambazo zinatumwa na mwenye meli, hazina uhusiano na utaifa wa meli. Kama ninavyosema ni bendera za unafuu tu, mwenye meli anaandikisha meli yake, lakini utaifa wake ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bendera kwenye meli ni alama ya Utaifa kawaida na usajili wa meli. Sasa hii *flag of convenience* inatumika duniani na ina faida. Faida ambazo zinapatikana kutokana na kutumia bendera za unafuu unaweza ukaziweka katika sehemu mbili na nitazieleza kwa pamoja. Moja, ni faida inayopata mwenye meli na faida inayopata nchi inayoruhusu usajili huria. Nchi zinazoruhusu usajili huria zinapata mapato kutokana na ada ya usajili ingawaje hazina usimamizi wowote na hizo meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vili vili, wenyne chombo au wenyne meli wanapata faida na faida yenye ni urahisi wa kupata usajili, kwa sababu ni kama wanunuua usajili, hawapitii ile misingi thabit ya kudhibiti usalama, kwa sababu wanatoa hela wanapata usajili haraka sana.

Kwa hiyo, wao kwao ni faida ingawaje kwa nchi inakuwa ni hasara. Hawa wenyne meli kodi yao ya malipo ni ya wasiwasi kwa sababu huko kwenye hizo nchi za kwao wanasema hizi meli siyo za nchi zao na huko ambako wamesajili meli maadam wao wameishapata kipato kinachotokana na ada ya usajili hawajali sana, kwanza hawawezni kujuu hata hizo meli ziko wapi. Kwa hiyo, ni urahisi, ni kama wanakwepa kwepa kodi. Kwao ni faida, lakini kwa mwenye asili ya meli na vili vili kwa nchi ambayo inasajili ni hasara ya kukosa mapato.

Mheshimiwa Mmwenyekiti, kuhusu ajira katika meli hizi, wao wanaona ni faida kwa sababu wanaweza wakaajiri popote pale na hawa misingi yao ya ajira hawataki hata mambo ya Vyama vya Wafanyakazi. Kwa hiyo, ni faida kwao, lakini ni hasara kwa nchi ambazo sisi tunajaribu kuendeleza fani ya ubaharia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ni hasara, kwa kweli hawa si rahisi kutambulika (hawa wamiliki). Wamiliki hawa wanabadilisha badilisha vitambulisho vyao, huwezi hata kuwabana. Wafanyakazi hawana haki kama vili kuanzisha Vyama,

malipo na mapato na mishahara ya wafanyakazi ni midogo, ni shida hata kuzikagua hizi meli na hazina usalama wala hazina usimamizi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya ajali kubwa zilizoleta uharibifu mkubwa hasa katika mazingira zilitokana na meli zenye usajili wa namna hii (*flags of convenience*) kama vile meli ya *Torey Canyon* mwaka 1967, *Amoco Cadiz* mwaka 1978, *Exxon Vardiz* mwaka 1989, *Scandinavian Star* mwaka 1990, *Sea Express* mwaka 1996 na meli inaitwa *Erika* mwaka 1999. Nchi zenye *open registry* ni nchi kama vile Antigua na Barbuda, Aruba, Bahamas, Bermuda, Cambodia, Freeman Ireland, Cyprus, Molta, Mauritius, Sri Lanka, Vanuatu na Tuvalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutaka kujiweka na sisi katika kundi hilo kwa sasa na usimamizi hatunao na jina letu ni zuri, tukasema ngoja kwanza tuangalie mpaka tutakapoijiimarisha, tutakapoona hasara ni chache kuliko faida ndipo tutakapokuwa na nafasi ya kuingia. Kwa sasa kwa kweli hizi faida za kupata fedha ndogo ndogo na heshima yetu ikapotea tukawa na meli ambazo labda ni za watu wanaofanya biashara ya magendo, biashara ya madawa ya kulevyta na vinginevyo na huwezi kuwadhibiti, itatuharibia jina zuri sana la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi wa Meli Duniani linapinga sana hizi *flags of convenience*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mamlaka ya Waziri limezungumziwa sana, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Kabourou amelieleza na amelielewa, ninafikiri Mheshimiwa Mutungirehi naye atalielewa. Pamoja na kwamba tumezungumza Waziri, Waziri, Waziri kila mahali, siyo Waziri atakayefanya kazi, hawezi kuwa mjuzi wa meli wala baharia na Waziri huyu wa sasa ni mwoga kweli kwa meli, kwa sababu anatoka milimani Rungwe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa kazi Serikalini ni kwamba, Wizara na Waziri ni sawa sawa wanashughulika na sera na mipango na kuleta Miswada Bungeni na usimamizi wa jumla wa utekelezaji. Haya masuala ya udhibiti wa usalama ambayo ndiyo kazi kubwa ya huu Muswada, udhibiti wa usalama wa uchukuzi wa meli katika bahari, maziwa na mito yatasimamiwa na Mdhibiti (*Regulator*) na utekelezaji wake ndiyo hawa ma-operator, mawakala, makampuni binaffsi na wengineo. Kwa hiyo, kuna mgawanyo mzuri tu, Waziri hatatunga hizo *regulation* kwa sababu tumeishasema kwamba atagawa, atakasimu madaraka mengine na mengine atayatoa, ni lazima ayatoe kwa chombo ambacho ataelewa yeeye mwenyewe atakielekeza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba msiwe na wasiwasi, pamoja na kwamba Waziri ametajwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa Muswada, basi yote haya atayafanya, la hasha! Inawezesha tu kukumbusha kwamba mwishoni jukumu kubwa la Serikali ni kusimamia, lakini watendaji watakaosimamia kwa maana ya kazi za kila siku nao wametambuliwa katika sheria hii na Waziri atawapa maelekezo. Kwa hiyo, naomba mlielewe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijibu tu lile la Mheshimiwa Samwel Chitalilo, la ukaguzi wa vyombo vidogo vidogo. Nitoe maelezo tu ya ziada kwa aliyotoa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, nayo ni kwamba, katika sheria tumeliona hilo na katika sheria hii tunajaribu kulisawazisha, ni kero kwa kweli.

Kwanza tumetenganisha, hivyo vyombo vidogo vidogo tumevipa tafsiri tofauti na meli yenye. Halafu vile vile tumesema havitapata leseni. Tunachotaka sisi viwe tu na chombo kinachoweza kutambulika kiusalama ili kupunguza athari ya mgongano na meli kubwa. Kwa hiyo, kazi yake huyu Bwana Mbondo kwa sheria hii itakuwa imepunguka sana na kuwanyanya hao wenye vyombo vidogo vidogo kutakuwa hakupo. Tungependa ushirikiano wa hawa watu wenye vyombo vidogo vidogo. Washirikiane na sisi katika suala la usalama, hili suala la kugongana na hizi meli lipungue sana. Kwa hiyo, tunadhani tutalishughulikia hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, amezungumzia kuhusu bandari zake za Ujiji, Tibirizi na Kigoma. Ziko karibu sana, lakini katika maendeleo bado ni mbali, huwezi ukatembea na lazima watu watoke Tibirizi na Ujiji waende vile vile kwa meli mpaka kwenye bandari ya Kigoma. Kwa hiyo, tumelizungumzia siyo katika Muswada, lakini kisera. Yeye mwenyewe amesema tumeamua kwamba bandari zote sasa zitasimamiwa na chombo kimoja nacho ni Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumesahau sana hizi bandari kwa sababu mwenye reli jukumu lake kubwa kwa kweli ni reli, bandari ilikuwa ni kitu ambacho naye akikitumia anakiacha vile vile, ndiyo maana bandari za maziwa makuu zimeharibika sana hasa za *Lake Tanganyika*, *Lake Nyasa* na *Lake Victoria* si nzuri kwa kweli, tulikuwa tumezisahau, lakini nadhani tumezipatia ufumbuzi sasa na mategemeo yetu ni kwamba bandari za Karema na Katanga tutaziangalia na zote zile za *Mbamba bay* na Manda tutaziangalia na kuziendeleza katika mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu sana kujibu hoja zote walizotoa Waheshimiwa Wabunge, zote ni nzuri na kama nilivyosema zote zitatusaidia, tumezichukua na tunaahidi kuandaa kabrasha ambalo tutaandika hoja na majibu pamoja na haya ambayo tumeyatoa halafu tutazisambaza kwa Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo kawaida tunavyofanya ili iweze ikasaidia kwamba Serikali huwa inatoa majibu wala haipuuzi yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayatoa wakati wa kutoa michango yao katika hoja za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala muhimu, suala zito ambalo nilidhani lisingetokea, lisingeulizwa, lakini limeulizwa na Wajumbe wengi sana. Suala hilo ni lile linalohusu nafasi za Zanzibar katika shughuli zote hizi. Napenda kukiri na kwa ajili ya rekodi zetu, sheria hii kwa kweli ni matokeo ya ushirikiano mkubwa kati ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wengi wengine wa Zanzibar na Tanzania Bara.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii nimshukuru kwa dhati kabisa Waziri mwenzangu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar; Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na watendaji katika Wizara ile, tumesaidiana sana na tumefanya kazi pamoja. Kweli ni lazima nikiri, kama mnaona hii sheria imekaa vizuri siyo kwa sababu ya Wizara yangu tu, ni Wizara zote mbili. Nawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kusema kwamba, pamoja na kwamba kwa sasa Zanzibar haitahusika na sheria hii, uzoefu tuliuopata wa kufanya kazi pamoja utawasaidia wenzetu Zanzibar katika kuangalia uwezekano wa kufanya marekebisho katika sheria zinazohusu usafiri wa majini, sheria za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na sheria hizo ziko kama nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizo ni Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 1894 (*Merchant Shipping Act, 1894*). Kuna Sheria ya Taratibu za Bandari, sura 130 ya Sheria za Zanzibar (*Port Rules, Chapter 130*). Kuna Sheria ya Mabaharia Watorokaji, wenzetu walienda mbali kidogo, Sura 132 ya mwaka 1909 (*Seamen Deserters Law*). Halafu kuna Sheria ya Uingizaji Mabaharia sura namba 131 ya Sheria za Zanzibar ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Zanzibar nayo ina sheria zake na imekuwa hivyo mpaka sasa. Kwa sababu hawatakuwemo katika sheria hii kwa sasa hamna lolote litakalopungua, kwa sababu yote yamezingatiwa kwa upande wa Zanzibar katika sheria hizi nilizoziainisha na ndizo ambazo zinatumika na ndizo zinazotawala uhusiano katika uchukuzi wa majini kati yetu na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza tu kwamba, iwapo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaona vema ikafanya mabadiliko katika sheria zake ili zilingane lingane na hii sheria ambayo kwa kweli tumeandaa pamoja, basi hakutakuwa na tatizo la utekelezaji hata kidogo, hakuna. Kwa hiyo, naomba tusivunjike moyo kwa kutoiona Zanzibar katika hii, si ishara mbaya hata kidogo, hakuna lililopotea. Naomba sana tusivunjike moyo, hakuna lililoharibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, watendaji wetu wamefanya kazi kubwa sana mpaka tulipofika hapa. Watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa wao wanalionia hili suala kiutendaji na kisheria tu, kwa hiyo kwa upande wamefadhaika. Lakini hili suala siyo rahisi namna hiyo, hili suala linahusu maslahi ya Zanzibar na linahusu vile vile maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tunachojaribu kufanya katika mazungumzo ni kutafuta mahali pa makutano, sasa tukifika makutano mahali ambapo maslahi ya Zanzibar na maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanafanana, yanashabihiana na yanakutana, basi hapo ndio mahali tunapopatafuta. Tunaposema tunaendelea na mazungumzo ni hilo na hilo si jambo baya, ni jambo zuri tu, linachukua muda, lakini tuwe na uvumilivu, tutafika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya namna hii ya kimuungano katika nchi nyingi yanachukua muda mrefu sana, mpaka leo Waingereza baada ya miaka sijui mingapi hawajafikia muafaka kuhusu Ireland ya Kaskazini. Sasa sisi tunategemea kweli tumalize mambo yote katika miaka arobaini? Haiwezekani. Kwa hiyo, tuwe na subira tu tutajenga tu na mambo yataimarika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni tafsiri gani au tafsiri pana ya mambo gani ni ya kimuungano kikatiba na mambo gani si ya kimuungano. Ni kweli kwa suala la uchukuzi majini Katiba inazungumzia bandari.

Kwa hiyo, tunapoendelea na mazungumzo kwa kweli ni kujaribu kupatana au kukubaliana kuhusu yale mambo ambayo si ya muungano ambayo hayamo katika Katiba, lakini inabidi kwa sababu ya mfumo wa kijiografia tuyafanye pamoja. Tunawezaje kufanikisha malengo hayo kwa pamoja na je, ni mfumo gani huo amba tuwe nao na utambulike kisheria au tutumie taratibu tu za kawaida za maelewano ya utekelezaji kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo mapana, siyo ya kuyatafutia ufumbuzi siku moja. Kwa hiyo, tunaposema kwamba tunaendelea na mazungumzo kwa kweli ni kwa nia hiyo tu ya kuyapatia ufumbuzi wa kisiasa masuala haya na siyo ufumbuzi wa kitaalam, hasa ndilo tunalofanya. Mazungumzo yanaendelea na kwa kweli si katika Sekta hii tu, ni katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, katika masuala ya muungano ndivyo ilivyo, lakini watu wenyewe nia njema, wenyewe lengo moja naamini kwamba tutaaafikiana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ni kwamba, kwa upande wa bahari, bahari isitugawe. Kwa kweli bahari ituunganishe na kijiografia inatuunganisha. Sasa tukizingatia hilo nafikiri tutafika muafaka tu na Mwenyezi Mungu atatusaidia kuyafanikisha hayo tunayokusudia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba niwatakie mfungo mwema na kila la kheri na amani katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Majini wa Mwaka 2003
(The Merchant Shipping Bill, 2003)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu una vifungu kama mia nne, tukitaka kupitia kifungu kwa kifungu tunaweza kuchukua muda mrefu sana.

Kwa hiyo, tunaona ni busara twende sehemu kwa sehemu na vifungu vitatajwa, pale unapohitaji kupata ufanuzi basi utasimama. Muafaka katika hilo?

WAJUMBE FULANI: Ndiyo.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI: Ahsanteni sana.

Kichwa cha Muswada

(*Kichwa cha Muswada Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 1

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, bado ningombaa anisaidie ufanuzi katika hiki kifungu cha tatu kwani kidogo napata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameleeza nia njema ya Serikali pale ilipoamua kuiondoa Zanzibar katika Muswada huu, lakini sasa napata matatizo kuondolewa huku kama kutakuwa kumekamilika kutokana na haya maneno yaliyopo katika hiki kipengele (b) *subsection one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna neno hili *territorial sea* na hili neno *Jurisdiction of the United Republic of Tanzania*. Ninavyoliewa lina upana zaidi, lina-cover eneo lote la Tanzania.

Hapa ningeliomba anisaidie ili nieewe vizuri kama dhana hiyo itakuwa imekwenda sambamba na kile kipengele (e) kilichofutwa? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri nadhani umemwelewa, kama umemwelewa tunaomba maelezo, kama kifungu hakijaeleweka arudie.

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge, arudie. Aniwie radhi.

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba, nimeridhika na maelezo yake, lakini naomba ufanuzi wa nyongeza katika kifungu cha 3, *application of the Act*. Kipengele (b) kuna neno pale mstari wa pili naomba ufanuzi wa neno hili, mipaka yake inaishia wapi, unapozungumza *territorial sea*? Halafu *jurisdiction of United Republic of Tanzania*, dhana hiyo vipi itakwenda sambamba na kile kipengele (e) kilichofutwa ambacho kimeiondoa Zanzibar katika *application* ya sheria hii? Nafikiri nimeeleweka hapo.

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu Katiba inatambua Serikali mbili, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, hamna *jurisdiction* ya Tanzania Bara. Madhumuni ya kutenganisha kwa sasa Zanzibar, moja ambalo sikulitaja wakati natoa maelezo ya ujumla ilikuwa katika mazungumzo yetu ni kupata muafaka kuhusu jinsi gani sheria hii inayohusu usalama wa meli inaingilia masuala ya kibiashara ambayo si ya kimuungano. Kwa hiyo, hii ni *formulation* ambayo inatumika kwa sababu hatuna mipaka ya Tanzania Bara, isipokuwa kuna mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kuzungumza hapa ni kwamba, iwapo tutasema kwamba, sheria itakuwa inafanya kazi katika *jurisdiction of United Republic of Tanzania* maana yake inafanya kazi Tanzania nzima kwa tunavyoifahamu. Sasa zipo sheria tunazipitisha nyingine, mfano hiyo itakayofuata ya *fisheries*, imeeleza *shall apply to Mainland Tanzania!* Sasa kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, anasema kwamba, hii sheria itatumika *Tanzania Mainland*. Sasa ukizungumza *jurisdiction of United Republic of Tanzania*, ile dhana ya kufuta *sub-section (e)* itakuwa haipo. Hiyo ndiyo ninayoizungumzia. Sasa ninataka anifafanulie anapozungumza hili kwa sababu hata unapokuja katika tafsiri ya maneno *territorial sea* haikuwa *defined* na vile vile *jurisdiction* tukuchukulie hapa kama ni mamlaka hii inaturudisha huku, ukitudisha katika Katiba inatupeleka katika ibara ya 2(1). Sasa naomba usafanuzi zaidi, bado naona swali langu hili kama halijajibiwa vizuri. (*Makofii*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumfanulie Mheshimiwa Zahor Juma Khamis. Tupolifuta *application*, kutumika kwa sheria hii kwa Zanzibar maana yake sasa ni kwamba, sheria hii iatumika Tanzania Bara. Lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, ndiyo inashughulikia pia na masuala ya Tanzania Bara, kwa maana hiyo sasa kama Sheria inasema kwamba, sheria hii itatumika Tanzania Bara peke yake, maana yake ni kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa kwa shughuli hiyo. Sasa *jurisdiction* ambayo anaisema Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, lazima uipatie maana hiyo, huwezi ukaipatia maana nyingine. Akilifahamu hilo na siyo mara ya kwanza kuandika sheria katika sura hii, nadhani tutakuwa tumesaidia kulielewa suala hili. Ahsante sana.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kuongezea tu hapo kwenyethree hiyo. Madhalani Mheshimiwa Waziri mhusika, ameeleza kinaganaga kwamba Zanzibar wana sheria zao ambazo zinafanana na za kwetu. Kwa hiyo, sheria hizo mbili zikisomeka pamoja hatuna utata. Kwa maelezo hayo je, isingelikuwa vizuri katika (c) (1) kusema "*unless otherwise expressly, provided this shall not extend to Zanzibar*", halafu tukafuta (a) (b) (c)? *Shall not extent to Zanzibar*, maana wao wana ya kwao, sisi tuna ya kwetu, lakini zile mbili zikiungana utata unakwisha. Sasa haya mambo ya *jurisdiction* na kadhalika utata unapotea kama tukifanya tu *this Act shall not extent to Zanzibar*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *schedule of amendment*, namshukuru Mheshimiwa Nimrod Mkono, tulichofanya ni kufuta (1) (a) hadi namba hizo (b) na (c) kama (a) na (b). Sasa kwa maana hiyo (1) (a) ungeweza ukasema it shall apply to Tanzania Mainland ukaishia hapo. Sasa hiyo ya (c) ambayo ndiyo tunaisemea, ambayo Mheshimiwa Zahor Juma Khamis inakusumbua ndiyo nikasema shughuli za masuala haya ya *merchant shipping* mamlaka inayokabidhiwa kuyasimamia ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hiyo ndiyo hoja *jurisdiction* ya pale. Sasa ndiyo maana nikamwomba Mheshimiwa Zahor Khamis Juma, kama akilielewa kwa namna hiyo hakuna tatizo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu matukio yatakayotokea katika sehemu hiyo ya Jamhuri ya Muungano, ambayo na wenyewe wana mamlaka nayo, yatasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi kwa kutekeleza sheria husika iliyopitishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, sioni kama lipo tatizo.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo *section (2)* kwenye *definition*, nilitaka kupata ufanuzi kama *a Bareboat Charter Term* na *charter period* waliziingiza hapa, kwa sababu *clause 2* ukiisoma *hai-make a proper definition "a Bareboat Charter Term"*. Hizi *amendment* za kwenu sijazona, lakini niliomba nitoe ushauri sasa sijui ulifikia wapi huu ushauri? Kwa sababu *definition is missing* kwa hiyo, *Bareboat Charter Term*, pamoja na *charter period*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, maelezo au bado unaendelea?

MHE. NIMROD E. MKONO: Bado ninaendelea. Pia kuna mabadiliko ya *Court, means the High Court of Tanzania, High Court of Zanzibar*, nilitaka kuona kama marekebisho yaliyofanyika yameondoa hiyo *High Court of Zanzibar*, maana hii sheria *hai-extend* Zanzibar. Sikupata hizo *schedule of amendment* pengine ndiyo tatizo nililolipata.

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nimrod Mkono, atuwie radhi kama hajapata hizi *schedule of amendment*. Kwa hiyo, ni kama nilivyomhakikishia, mengi aliyoyazungumza tumeyafanya mabadiliko na nilimshukuru sana nilipokuwa namalizia hoja yangu. Kwa hiyo, tulichofanya tume-*define* *Bareboat Charter* na yale yote aliyozungumzia nayo yamo katika mabadiliko ambayo tumeyaleta. Namshukuru sana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 2

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 3

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 4

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 5

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie hapa, kwenye kifungu cha 83, *right to fly flag of Tanzania*, sasa hoja inakuja hapa kwamba, tumezungumzia tutakuwa na sheria nyinginezo zitakazokuwa zina-*apply*, tutazame sasa Bendera ya Taifa ni hii hii moja tu? Sasa na hiki kinaendelea kuna vifungu vingine ambavyo vinazuia kuwa *registered* na sheria hii kama *right*, unakuwa huna. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie ufumbuzi wa tatizo hili. Ahsante.

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, kwa swali lake analohitaji ufanuzi amba ni wa kimsingi sana. Labda nirejee kwa hali ilivyo hivi sasa kwa sababu haitabadiika mpaka hapo tutakapofikia muafaka. Ilivyo sasa meli zilizosajiliwa Zanzibar na Zanzibar ina usajili wake wa meli, zinapeperusha Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niendelee tu kwamba, Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania si Bendera ya Tanzania Bara ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, meli za Zanzibar zina haki kabisa kupeperusha Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kuna vipengele amesema vinaweza vikaleta utata, havileti utata kiutekelezaji kwa sababu ndiyo hali halisi ya sasa.

Usajili Zanzibar, usajiri Dar es Salaam, lakini Bendera wote tunapeperusha pamoja. Sasa iwapo kuna matatizo yanayotokana na utekelezaji wa maeneo ya sheria hii, kama nilivyosema wenzetu Zanzibar wataitafakari kwa sababu tumeandaa kwa pamoja, wataangalia ni jinsi gani inawaletea matatizo katika mabadiliko ya sheria zao, kama kuna matatizo basi pale tutakapofikia muafaka na itapelekea kubadilisha sheria hii, hatutasita kuja Bungeni kuomba mabadiliko hayo. Ahsante sana.

Kifungu cha 6

Kifungu cha 7

Kifungu cha 8

Kifungu cha 9

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 17

Kifungu cha 18

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

Kifungu cha 20

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 21

Kifungu cha 22

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 23

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka kupata ufanuzi kwa kifungu cha 425 mpaka 427, sasa kitasomeka vipi ingawa nimeona haina mabadiliko? Nataka kujua tu nia ya Serikali inaposema, "for the purpose of giving effect to any international agreement or other international treaty or instrument relating

to shipping or the prevention of pollution of the marine environment, to which Tanzania is a party, the Minister may make such regulations, as appear to him to be necessary." Nilitaka kujua hizi *treaty* sisi hatuna au pengine zipo zimetangazwa, kwa nini wasingeziifanya ziwe *part ya schedule?* Maana ni *treaties* ambazo tumekuwa nazo na kwamba zina-be *given effect*, sasa mnatuambia msomi yejote aliyeo Musoma akaziangalie wapi, tukazipate wapi? Isingekuwa jambo la busara kuzi-*annex* hizo *convention* ama *treaty* tunazozizungumza?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Nimrod Mkono. Tunachosema hapa ni kwamba, ile Mikataba ambayo Waziri ataizingatia katika kutunga kanuni ni Mikataba ambayo itakuwa imeridhiwa na Bunge na ikiridhiwa na Bunge basi ni sheria za nchi kwa hiyo, hatakwenda nje ya hapo isipokuwa alilokuwa anauliza Mheshimiwa Nimrod Mkono ni kwamba, kwanza kwa nini haziletwi kama *schedule* pamoja na sheria hii? Kwanza ukubwa tu wa hii *bill* unamtememesha huyo mtu wa Musoma. Sasa ukimwekea *page* nyingine 1000 basi ndiyo umemfukuza kabisa katika kusoma hizi sheria. Kwa hiyo, kwa sababu zipo na zinakuwa zimesainiwa na zimetunzwa na ziko Bungeni na siku hizi ziko hata kwenye Tovuti, naamini Mheshimiwa Nimrod Mkono, Tovuti imeshafika Musoma kwa sababu Mheshimiwa Nimrod Mkono ni mtu wa maendeleo sana. Kwa hiyo, zitapatikana tu haziwezi kufichika, hizi ni *public documents*. Mahakama zitakuwa nazo, unapozitaka wakati wowote ule kama haziko kwenye *library* zao. Kwa hiyo, namwomba akubali tu kwamba, zikishapita humu kama zimeridhiwa na Bunge, basi ni *documents* katika *public domain*. Namshukuru sana.

MHE. NIMROD E. MKONO: Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, bado sijaridhika kwamba, sheria inayo-*implement a treaty has important* kama hiyo ya *pollution* ambayo inampa mtu uhalali wa kwenda Mahakamani akaombe. Anapokwenda Mahakamani anasema *chapter so and so, rely* pengine *Merchant Shipping Act, 2003*. Nasema aangalia Mikataba yote iliyopitishwa, siyo utaratibu unaofanywa katika kutunga sheria. Waingereza hufanya hivyo, Kenya hufanya hivyo kwa nini sasa tuifichefiche hiyo? Kuna ubaya gani kuifanya Mikataba ya Kimataifa iwe *part* kwenye *schedule* tu, inaweza kuwa albaki lakini wenzetu walivyofanya, maana mimi ni *practitioner*, ninajua matatizo ya Mahakamani ni nini?. Sasa ukifanya ni *schedule* unajua haina matatizo?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Nimrod Mkono, kwa maana Mikataba peke yake iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haiwi Sheria moja kwa moja, ni pale ambapo katika utekelezaji unapoamua vifungu fulani sasa vya Mikataba huu viwe sehemu ya Sheria ya Nchi kwa hiyo, unafanya hivyo. Kwa mapendekezo anayoleta, wazo la Mheshimiwa Mkono na lenyewe ni tatizo kidogo kwa sababu siyo vifungu vyote ambavyo kwenye *convention* hiyo unataka uvi-*domesticate*, uvifanye sehemu ya Sheria za Nchi, ni vile vinavyolengwa na ukiona Muswada huu wa masuala ya *safety* baharini unaona ni kama tume-*lift* vile vifungu ambavyo viko katika *convention* hizo na kuziingiza humu. Sasa ukitaka kuainisha unaweza ukasema tuwe na kifungu tu kinachosema:

"Mikataba yote ambayo Jamhuri ya Muungano imeridhia, itachukuliwa kwamba ni sehemu ya Muswada huu."

Hiyo mimi sina tatizo, tunaweza tukaingiza kifungu kipyaa cha 425 (a) ili tusiharibu huu mtiririko wa Muswada na kusema: *"Any International Agreement or other International Treaty or instrument relating to shipping to which the United Republic of Tanzania is a party, shall be deemed to form party of this Act.*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkono umeridhika?

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwanasheria Mkuu, kwa kuzingatia hilo jambo. Ahsante sana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 24

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Jedwali

(*Jedweli lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na mabadiliko yake*)

(*Bunge lilirudia*)

**(Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Majini wa Mwaka 2003
(The Merchant Shipping Act, 2003)**

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu na imeukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Majini wa 2003 (*The Merchant Shipping Bill, 2003*), sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe
Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

MWENYEKITI: Taratibu za Muswada huu zimeshakamilika. Katibu Shughuli nyingine inayofuata.

Muswada wa Sheria ya Uvuvi wa Mwaka 2003
(The Fisheries Bill, 2003)

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MHE. ARCADO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kwanza niishukuru Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, chini ya uongozi wa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, kwa kuchambua Muswada huu kwa kina na hatimaye kutoa maoni na michango mbalimbali ya kuboresha Muswada. Maoni na michango iliyotolewa na Kamati imekuwa muhimu sana katika kuboresha Muswada huu na michango hiyo imezingatiwa kwa uangalifu kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Muswada huu, ambalo naamini kila Mheshimiwa Mbunge amepata nakala.

Pili, napenda pia kuwashukuru wataalam mbalimbali waliohusika katika kuandaa na kukamilisha Muswada uliopo mbele yetu. Wataalam hao ni kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawashukuru kwa kazi nzuri iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizi, napenda kuwasilisha Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo wengi wenu mnafahamu, Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000, inatamka wazi kwamba, katika kipindi cha 2000 - 2005, Serikali ya CCM itaendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna kwa busara, raslimali za maliasili kwa manufaa ya Taifa letu. Mali hizo ni wanyamapor, misitu, nyuki, samaki na viumbe vya majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutimiza jukumu lake kila Sekta ndogo ya Maliasili, inayo sera na sheria ambazo zimeweka taratibu za uvunaji, uhifadhi na uendelezaji wa raslimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ndogo ya Uvuvi ni mojawapo ya zile zenyera ambazo zinakidhi kwa kiasi kikubwa mahitaji yaliyofikiwa kisayansi, kiteknolojia, kiuchumi, kiutawala hapa nchini na ulimwenguni kote. Ingawa sera ya uvuvi ilipitishwa na Serikali mwaka 1997, sheria ambayo bado inatumika ni ile ya mwaka 1970.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka hadi mwaka 1985 nchi yetu ilikuwa haijaingia kwenye mfumo wa biashara huria, uvuvi ulikuwa unaendeshwa kwa madhumuni ya soko la ndani. Biashara ya mazao ya uvuvi ilikuwepo kwa kiasi kidogo sana. Hivi leo uvuvi umepanuka na kuwa shughuli muhimu katika uchumi wa Taifa. Mauzo ya mazao ya uvuvi kwenye soko la nje yanachangia asilimia kumi katika Pato la Taifa. Aidha, kutokana na Serikali yetu kuungana na Mataifa mengine katika kurekebisha mfumo wa uchumi na biashara na kuboresha mazingira na ubora wa mazao, sheria haina budi kubadilishwa ili kwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya uvuvi inayotumika sasa inayo mapungufu katika maeneo kadhaa. Kwa mfano, kuhusu uongozi na usimamizi, sheria hiyo haikuweka bayana majukumu ya Waziri anayehusika na uvuvi wala haina mchanganuo wa Maofisa mbalimbali wanaoweza kuteuliwa kusimamia sheria, haina kifungu kinachowabana Maofisa mbalimbali wenyewe maslahi binafsi kwenye maeneo wanayosimamia kutokana na taaluma zao. Sheria hiyo haioneshi uhusiano kati ya Wizara na Serikali za Mitaa katika kusimamia na kuendeleza raslimali za uvuvi. Sheria hiyo haina kifungu kinachohusu ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa majini. Ufugaji wa samaki unaongeza upatikanaji wa samaki na pia kupunguza shinikizo la uvuvi katika maji ya asili. Hakuna kifungu kinachoweka wazi majukumu ya jamii katika kusimamia raslimali za uvuvi. Ushirikishwaji wa jamii unaleta mahusiano mazuri kati ya Serikali na wananchi. Aidha, unawafanya wajione kuwa ni wadau muhimu na pia inaipunguzia Serikali gharama za usimamizi.

Suala la viwango vya ubora na usalama wa mazao ya uvuvi halikutajwa. Nyakati hizi masoko ya Kimataifa yanataka kufanya biashara na nchi ambazo zimeweka mfumo wa udhibiti wa ubora na pia unaowezesha kufuatilia mazao hadi kwenye chanzo chake. Hakuna kifungu cha sheria kinachoruhusu kuwa na mfuko maalum wa kuendeleza shughuli za uvuvi. kuhusu makosa na adhabu. Sheria haina kifungu kinachomwezesha Mkurugenzi wa Uvuvi kuadhibu makosa madogo madogo au kuendesha kesi Mahakamani. Aidha, hakuna kifungu kinachowezesha utoaji wa adhabu kulingana na uzito wa makosa.

Suala la tathmini ya athari za miradi kwenye mazingira halikupewa uzito kwenye sheria inayotumika. Sera ya biashara huria pamoja na ile inayoruhusu wawekezaji kutoka nje zimesababisha miradi mikubwa kuanzishwa hapa nchini. Baadhi ya miradi ina madhara kwenye mazingira majini na nchi kavu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini mapungufu yaliyopo kwenye Sheria ya Uvuvi ya mwaka 1970, ambayo baadhi yake nimeyataja, hatua zilichukuliwa za kuandaa Muswada huu ili kuwa na sheria madhubuti itakayoshughulikia masuala ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria mpya ya uvuvi imetungwa kwa kuzingatia hati mbalimbali kama vile sera ya uvuvi ya mwaka 1997, miongozo ya Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa kuhusu *Code of Conduct for Responsible Fisheries*, baadhi ya sheria za nchi nyingine zenyе mazingira yanayofanana na yetu, *agenda* ya 21 ya Mkutano wa Rio De Janeiro, kuhusu mazingira uliofanyika mwaka 1992 nchini Brazil, Mikataba ya Kimataifa inayohusiana kama vile *The African Convention Conservation of Nature and Natural Resources, The Biological Diversity Convention 1992*, Itifaki ya SADC kuhusu uvuvi, *The Lusaka Agreement and Cooperative Enforcement Operation Directed at Illegal Trade in Wildlife Fauna and Flora* ya mwaka 1994, pamoja na mengine ambayo tunayazingatia.

Maandalizi ya kutunga Sheria Mpya ya Uvuvi yalianza mwaka 1998, kwa kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Wadau walioshiriki walitoka kwenye sekta iliyo rasmi na isiyo rasmi, nao ni pamoja na Wizara za Serikali, pamoja na Taasisi zake, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, wavuvi wakubwa na wadogo, Wafanyabiashara, wenge viwanda vinavyosindika mazao ya uvuvi, wafugaji wa samaki, wanamazingira, wanasheria na vikosi vya ulinzi wa raslimali. Matokeo ya kazi hiyo iliyofanywa na wadau hao takriban kwa miaka mitano, ni Muswada uliopo mbele yetu leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu ni kutunga sheria ambayo itaweka masharti ya usimamizi na uangalizi wa shughuli zote zinazohusiana na Sekta ya Uvuvi. Muswada unakusudia kufuta Sheria ya Uvuvi ya mwaka 1970 na kuweka sheria mpya ambayo itazingatia mabadiliko ya sera, pamoja na maendeleo mengine ya kiteknolojia na kiuchumi na kijamii. Sheria mpya itajumuisha mabadiliko katika nyanja za mazingira. Muswada huu unaweka mkazo katika suala la ufugaji wa samaki na vile ubora wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu kumi. Sehemu ya kwanza imeweka masuala ya utangulizi yanayohusu jina la Muswada, kuanza kutumika kwa Muswada, mipaka na matumizi na ufanuzi wa maneno na misemo yenye maana maalum katika sheria inayopendekezwa. Sehemu ya pili imeweka majukumu na taratibu za usimamizi wa masuala ya uvuvi. Sehemu ya tatu, ya nne na tano inahusu uendelezaji wa uvuvi, ufugaji wa samaki na zinaweka masharti ya usimamizi ikiwa ni pamoja na utoaji wa leseni.

Sehemu ya sita imeweka masharti ya udhibiti wa viwango vya ubora wa mazao na hasa tunazungumzia udhibiti (*certification*). Sehemu ya saba imeweka vifungu vinavyohusu masuala ya fedha hususan utozaji wa ada na uanzishaji wa mfuko wa kuendeleza uvuvi. Sehemu ya nane imeweka vifungu vya Hima Sheria ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa Kikosi cha Doria, mamlaka ya kuendesha mashtaka na ukamataji wa viliviyotumika katika uhalifu.

Sehemu ya tisa imeweka masharti kuhusu makosa na adhabu juu ya uvunjaji wa sheria inayopendekezwa, utozaji faini kwa wanaokiri makosa na utaifishaji wa mazao au

vifaa vilivyokamatwa. Sehemu ya kumi na ya mwisho ya Muswada huu imeweka masharti ya ujumla kama vile madaraka ya kutengeneza kanuni, misamaha na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo katika kuwasilisha Muswada uliopo mbele yetu, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. HASSAN RAJAB KHATIB (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 (*The Fisheries Bill, 2003*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2003, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati hii kuhusu Muswada wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 (*The Fisheries Bill, 2003*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umeletwa mbele ya Bunge hili katika muda muafaka kwani umelenga kuboresha shughuli ya maisha ya wavuvi wadogo wadogo kwa kuwaondolea umaskini kwa kuwaanzishia Mfuko maalum wa uvuvi na kuwapa mafunzo ya jinsi ya kuendesha shughuli za biashara ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakusudia kutunga sheria inayohusu Sekta ya Uvuvi, ambayo itaweka masharti ya usimamizi na uangalizi wa shughuli zote zinazohusiana na sekta hii. Aidha, Muswada huu unakusudia kufuta Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 1970, kwa kuzingatia mabadiliko yaliyotokea tangu mwaka huu hadi sasa, kwani sheria hii mpya itakayotungwa italenga katika usimamizi wa raslimali za uvuvi kwa kuzingatia mabadiliko katika nyanja za mazingira. Hali kadhalika, Muswada huu umeweka mkazo katika ufugaji bora wa samaki kwa kuzingatia viwango kwa ubora wa mazao ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kupata matokeo mazuri yaliyotokana na maandalizi mazuri ya Muswada huu hususan katika kuihusisha kwa namna moja au nyingine, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wa kutengeneza sheria hii. Naamini kuwa kwa kufanya hivyo, wananchi wa Tanzania Visiwani watafaidika kwa kiasi fulani, wakati wa utekelezaji wa sheria hii katika masuala ya uvuvi, shughuli ambayo inategemewa na wananchi kwa kiasi kikubwa sana katika kujikwamua kiuchumi na kuondoa umasikini.

Wizara hii imekuwa na mahusiano mazuri katika Wizara nyingine hususan Wizara ya Serikali za Mitaa, Idara ya Misitu, Nyuki, Baraza la NEMC, pamoja na nchi za

nje, kwa kuhimiza utekelezaji wa mpango wa kudhibiti *Deep Sea Fishing*. Katika Pwani ya Bahari ya Hindi, inayopakana na mipaka ya Tanzania kuitia nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na EU, kuanzishwa kwa Mfuko maalum wa uvuvi kudhibiti uvuvi haramu kwani zinanunuliwa zana bora na nyingi za kupambana na wahalifu ikiwa ni pamoja na kuwakopesha wavuvi wadogo wadogo ili waweze kununua zana na vifaa bora vya uvuvi na hivyo kujiongezea kipato katika maisha yao ya kila siku.

Kuelimisha wadau kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 1998 kwa kuitia Semina mbalimbali za jinsi Sheria hii mpya ya Uvuvi itakavyowanufaisha wadau hao, pamoja na walioko katika Sekta rasmi na ambayo siyo rasmi (*NGOs*). Wavuvi wakubwa hufanya biashara ya samaki na mazao yatokanayo na samaki, wafugaji wa samaki, wamiliki wa viwanda vya kusindikia samaki, wanamazingira na vikosi vya ulinzi na raslimali za jamii. Aidha, barua za maoni zipatazo 423 zilipelekwa ndani ya Wizara hii kutoka kwa wadau mbalimbali na zote ziliafiki maudhui ya sheria hii.

Kuendeleza kilimo cha mwani katika bahari kwenye ukanda wa Pwani, jambo ambalo linawasaidia wanawake kujikwamua kiuchumi na kibashara. Kuendeleza Chuo cha Uvuvi cha Mbenyani huko Bagamoyo. Ni matumaini yetu kuwa kwa kufanya hivyo, wataalam wengi zaidi wanapatikana ili kutosheleza mahitaji ya kusimamia na kudhibiti ipasavyo shughuli za uvuvi katika maeneo mbalimbali ya mabwawa, maziwa na bahari ya nchi yetu na kufanya jitihada za makusudi za kuhifadhi samaki wa ajabu aliyepatikana hivi karibuni huko Songo Mnara, Kilwa Masoko, ili samaki huyu aweze kuingiza pato kubwa kiatalii. Tunaishauri Wizara kuhakikisha ile *proper process* ya kuhifadhi katika Makumbusho ya Taifa ya Dar es Salaam.

Nawashukuru sana Mawaziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na wataalam wa Wizara ya Maliasili na Utalii, wakisaidiana na Wawakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuwasilisha maelezo ya kina kuhusu Muswada huu kiasi kwamba, sisi Wajumbe wa Kamati hii tulifarrijika sana na kuelewa fika Muswada wenyewe kutokana na uchambuzi na ufanuzi mzuri uliotolewa katika vipengele kadhaa ambavyo vingeweza kuleta utata wakati wa utekelezaji wa sheria yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki ya Muswada huu katika maelezo na ufanuzi kuhusu Muswada huu, Kamati imejifunza kuwa Sekta ya Uvuvi ni mojawapo ya zile Sekta zenye sera ambazo zinakidhi kwa kiasi kikubwa maendeleo yaliyofikiwa kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi hapa nchini na duniani kote. Hivyo basi, utekelezaji wa sheria hii utawanufaisha wananchi wengi Tanzania Bara na Visiwani kutokana na kwamba uvuvi utapanuka na kuwa shughuli muhimu katika uchumi wa Taifa. Pia mauzo ya mazao ya uvuvi kwenye masoko ya nje yataweza kuchangia zaidi ya asilimia kumi zinazopatikana hivi sasa katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, itaondoa mapungufu katika maeneo kadhaa ya ile Sheria ya zamani ya Uvuvi ya mwaka 1970, jambo ambalo litaongeza na kuinua ubora wa shughuli za uvuvi katika maeneo ya mabwawa, maziwa na bahari nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilielezwa pia kuwa Muswada huu umelenga kutunga Sheria mpya ya Uvuvi kwa kuzingatia masuala muhimu yafuatayo:-

- Hati mbalimbali za ndani ya nchi na nje ya nchi yetu;
- Baadhi ya sheria za nchi nyingine zenyenye mazingira yanayofanana na yetu;
- *Agenda ya 21 ya Mkutano wa Rio*, kuhusu mazingira uliofanyika mwaka 1992; na
- Mikataba mbalimbali ya Kimataifa inayohusiana na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mwelekeo huu, sheria hii itawanufaisha wananchi wa Tanzania Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ili kufanikisha utekelezaji wa sheria hii mpya, Kamati ya Maliasili na Mazingira inashauri Wizara ya Maliasili na Utalii na Serikali kwa ujumla, kuzingatia mambo yafuatayo:-

(1) Kuboresha zaidi, kukuza biashara ya mazao ya uvuvi, ndani na nje ya nchi yetu kwa lengo la kununua maisha ya wananchi wake;

(2) Kuendeleza utaratibu wa kutoa elimu kwa shughuli za uvuvi kwa wadau na wananchi kwa ujumla kuanzia ngazi ya Vijiji, Wilaya, Mikoa na Taifa kwa kuwawezesha kimtaji ili waweze kushiriki vizuri katika Sekta hii ya Uvuvi.

(3) Kuangalia uwezekano wa kutafsiri sheria kwa lugha nyepesi ya Kiswahili ili wananchi wengi waweze kuisoma na kuilewa ipasavyo.

(4) Kuainisha wazi mipaka ya bahari katika Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, kwani sheria hii siyo ya Jamhuri ya Muungano, bali itatumika Tanzania Bara tu.

(5) Kuweka usimamizi na udhibiti mahsusini katika bahari na maziwa ya nchi yetu ambayo itawahuishwa wavuvi wakubwa, wenye meli kubwa na hasa wanaotoka nchi za nje. Lengo ni wao kuruhusiwa kuvua samaki kwa kufuata masharti ya sheria hii.

(6) Kudhibiti suala la uharibifu wa mazingira hasa katika ukanda wa mwambao kungojea kunakojengwa Hoteli ya Kitalii.

(7) Halmashauri za Wilaya katika Ukanda huu zikahakikishe kuwa wawekezaji katika biashara ya Hoteli za Kitalii wanatimiza kwanza masharti ya sheria hii kabla ya kuruhusiwa kuwekeza.

(8) Kuainisha adhabu/faini zitakazokuwa zinatolewa kwa wahalifu wanaobainika kutumia baruti na sumu ili kuvuna kwa urahisi samaki katika mabwawa, maziwa na bahari nchini mwetu, kwani madhara yake kwa shughuli za uvuvi yako sawa.

(9) Kudhibiti au kutoruhusu ujenzi wa makazi unaofanywa na baadhi ya wananchi/wavuvi katika visiwa vidogo vidogo viliviyomo ndani ya maziwa na bahari ya nchi yetu ili kulinda uasili wa Visiwa hivyo.

(10) Kupiga marufuku utumiaji wa makokoro na yale yanayoingizwa kutoka nje ya nchi ili kulinda samaki wadogo amba wanaendelea kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa hitimisho la taarifa hii ya maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada huu, kwa mara nyingine tena na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, napenda nikushukuru wewe binafsi, pamoja na Washirika wote waliohusika kwa namna moja au nyingine katika kuandaa, kufikiria, kujadili, kuchambua na hatimaye kupitisha Muswada huu. Pia ninamshukuru Katibu wa Bunge na Sekretarieti ya Kamati, kwa huduma mbalimbali wanazoipatia Kamati, kiasi cha kuwezesha kutekeleza na hatimaye kukamilisha ipasavyo kazi ya kuchambua Muswada huu amba ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waupitishe Muswada huu wa Uvuvi wa mwaka 2003 ili kuupa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyokuwepo katika Sheria ya Uvuvi ya zamani na hivyo kuwanufaisha wananchi wengi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono Muswada huu wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003. Naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautoshelezi kupata maoni ya upande wa Upinzani. Kwa hiyo, tutampa nafasi Msemaji wa Upande wa Upinzani, aweze kutoa maoni yake tutakapokutana leo jioni na baada ya hapo tutakuwa na wachangiaji. Sasa hivi wameshakuwa wachangiaji kumi wa kwanza kuchangia atakuwa Mheshimiwa Hashim Saggaf na Mheshimiwa Ngwatura atafuatia.

Kuna tangazo liko hapa linasema, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anaomba Wajumbe wote wakutane leo saa 10.00 katika Chumba Na.428. Tutakapokuja huko wao watakwenda huko. Tutangaziane maana mnafahamiana, wengine hawapo hapa. Ni muhimu watu wahudhurie Kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 10.00 jioni.

(Saa 6.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Wapinzani walikuwa bado hawajatoa maoni ya upande wao. Kwa hiyo, tunamkaribisha Msemaji Mkuu wa Wizara hii. Karibu.

MHE. MASOUD ABDULLA SALIM (k.n.y. MHE. PHILLEMON NDESAMBUTO - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII): Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 (*The Fisheries Bill, 2003*):-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu na Kambi nzima ya Upinzani, napenda kutoa shukrani kwako, Mheshimiwa Waziri na Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu, kwa kupata fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu mapungufu yaliyomo kwenye Muswada huu wa Sheria ya Uvuvi wa mwaka 2003. Naliomba Bunge lako Tukufu, liyaangalie kwa kina kabla ya kuitisha Sheria hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya Ibara hii, Ibara ya 5(3), ukurasa wa 17, *Central Registry*, Sheria hazijaweka wazi kuhusu usajili. Sheria haijaaeleza kama usajili utakuwa unaishia Mkoani au unakamilika baada ya kufika *Central Registry*. Kama Sheria hii itabaki kama inavyoeleza bila kufanya marekebisho, basi wachache wanaweza kuitumia vibaya kwa manufaa yao na wengi kukosa haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii inahusiana na vyombo vyote vya uvuvi kwenye mito, mabwawa, maziwa na bahari; je, usajili huo unakamilika *at what stage* katika *Central Registry* au pale anapowasilisha maombi yake *fisheries office*? Bila kutamka kuwa usajili unafanyika kwenye ngazi ya Wilaya, hali hiyo italeta usumbufu mkubwa wa watu wenye vyombo wanaotaka kufanya shughuli zao kwenye mabwawa kama Mtera, Nyumba ya Mungu, Mito kama Kilombero na kadhalika. Tunachosema hapa ni kwamba, *registry point* lazima ziwe nyingi ili kuzuia ucheleweshaji usio wa lazima wa shughuli za uvivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, Ibara ya 5(5), 5(6), 5(7) na 5(9) inaonyesha kuwa watendaji wanaweza kuteuliwa na Mkurugenzi, Waziri au Serikali za Mitaa. Hii inaweza kuleta migongano ukitilia maanani kuwa walioteuliwa watafanya kazi ile ile. Ni katika mazingira gani mteuaji atapaswa kuteua ili asiingiliwe na mteuaji mwingine? Hapa mamlaka zinazoteua ni nyingi mno, hali hiyo itaweza kuleta mwingiliano mkubwa. Ingekuwa ni jambo la busara Mkurugenzi au Mkurugenzi wa Wilaya angependekeza wateuliwe kwa Mheshimiwa Waziri na iwe ni wa mwisho kutangaza uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne, Ibara ya 11, kifungu kidogo cha pili, kanuni hii ya Sheria ifafanuliwe zaidi kuhusu utakapowazuia wananchi kuvua, mzuiaji atakuwa ametenda kosa katika mazingira gani kuhusiana na uzuiaji huo? Kuna *Administer Order* zinazotolewa na Wizara kuwazuia wananchi wasifanye shughuli za

uvuvi, Sheria hii itaidhibiti mamlaka kama hiyo. Naomba kunukuu kipengele hicho: “any person or group of persons who deprive a local community the access to fishing grounds, shall be guilty of an offence.” Je, wananchi wa Ukerewe ambao chakula chao ni furu na wamezuiwa kuvua na Serikali, kwa Muswada huu wananchi wamepewa ruhusa ya kumshtaki anayezuia kuvua, sijui Serikali inalionaje jambo hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne, Ibara ya (5)(2) mpaka (3) vifungu vinafaa kwa asilimia mia iwapo anayepatikana na kosa si raia wa Tanzania. Kwa mwananchi Mtanzania tunapendekeza kuwa adhabu ya kuharibu mali zake kwa gharama zake iwe pale tu itakapobainika kuwa alifanya uzembe au kwa makusudi kusababisha kwa mfano, magonjwa ya samaki na kadhalika. Itakapobainika kuwa ilikuwa ni bahati mbaya, ni vema Serikali au Ofisi ya Mkurugenzi, kutoa msaada wa kiufundi wa hali na mali katika kumsaidia mwananchi kwa kutilia maanani utaalam na uwezo wa mhusika katika kutenda kosa lililotajwa kulingana na Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba, Ibara ya 29, kifungu kidogo cha tatu, kuhusu Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Uvuvi, sheria haielezi Kamati itafanyaje kazi; je, itafanya kazi pamoja na Mkurugenzi na Ofisi yake au itajitegemea au itakuwa chini ya Mkurugenzi au Waziri ambaye ndiye atakayeiteua? Tunashauri labda kuidhinisha matumizi ya kanuni hii ya sheria, utolewe ufanuzi kwa ajili ya ufanisi wa kazi na kuepusha migongano kuhusu matumizi ya pesa na ugomvi wa madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa ya Ibara ya 48(1) mpaka cha (5) kuhusu mali iliyotelekezwa, kwenye vipengele viliviyotajwa hapo juu, havielezi mali hiyo itafanya nini na Serikali mara baada ya taratibu za Mahakama kumalizika. Tunaomba sheria iweke wazi kama itabidi mali hii ije itaifishwe na Serikali au itapigwa mnada na mapato kwenda Hazina au watapatiwa waajiriwa wake au itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi, Ibara ya 53(2) kuhusu kufanya utafiti, siyo lazima tafiti zote za kisayansi kuhusu Kamati zote zitoke Ofisi ya Mkurugenzi, kuna vituo vya utafiti na watafiti wanaojitegemea ambao wanaweza kufanya utafiti huku matokeo yake yakiwa na manufaa kwa nchi nzima, mfano wataalam wazalendo ambao utafiti wao mara kwa mara ni kupanda daraja kupata shahada ya pili, yaani *masters* ya udaktari (*Ph.D*) *holder* au kuwa *professor*. Katika hali hiyo basi, si vizuri kuwalazimisha watafiti wengine kupata kibali cha Wakurugenzi au Mkurugenzi kama ilivyoainishwa na Ibara hii au kupata kibali cha Waziri, Ibara ya 56(a) mpaka (c) kwani kufanya hivyo kunaweza kukarefusha muda muhimu wa utafiti. Vile vile, mashirika yanayogharamia tafiti hizo, huwa yako makini na kipengele cha muda ukitilia maanani ugumu wa kuwasiliana na Mkurugenzi au Waziri anayehusika. Badala yake vibali vya utafiti vitolewe na wawakilishi wa Mkurugenzi Mkoani na Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaunga mkono Muswada huu na inaliomba Bunge lako Tukufu liupitishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuchangia katika hoja hii ya *Fisheries Act*, ambayo tumeleteewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Muswada huu na vile vile kuhakikisha ndani ya Muswada ya kuwa kuna mambo mengi sana, nyufa nyingi sana zimezibwa ambazo zilikuwepo katika Sheria ile ya mwaka 1970. Kwa mara ya kwanza naona ya kuwa Serikali inaanza kutambua na kuheshimu mali za nchi yake kwa sababu Muswada huu unaonyesha dhahiri ya kuwa Serikali sasa inaanza kuwa makini katika mali za Tanzania na siyo kuzigawa ovyo ovyo na ndiyo maana vipengele vingi vilivyomo humu ndani vinaziba nyufa za ile Sheria ya mwaka 1970.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasikitika tu ya kuwa imechukua miaka 33 kwa Serikali kugundua ya kuwa hii mali tuliyokuwa nayo, yaani bahari hii tuliyokuwa nayo, *territorial waters*, pamoja na *exclusive economic zone* ya maili 200 ya bahari, ni mali ya Tanzania, lakini kwa miaka mingi tumekuwa tunaibiwa na hatuibiwi kwa mwizi ambaye ni mdokozi ambaye anadokoa kidogo kidogo, meli za nje hasa za Kigiriki na ninasema wazi wala sifichi, zimekuwa zikija hapa na zikipewa *licence* na zinakuja kwenye bahari yetu ya *exclusive economic zone* na wanavua samaki wanavyotaka na hakuna mtu wa kuweza kuwazuia. Jambo hilo limefanyika kwa miaka 43 sasa na hakuna pingamizi la aina yoyote, watu walikuwa wanachukuliwa kama ni nchi yao kuliko nchi yetu sisi, kwa hiyo walikuwa wanafanya wanavyotaka. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kuwa Sheria hii sasa itajitahidi kuzuia hayo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria kama hii inapoletwa kwetu lazima tuelewe kitu kimoja nacho ni kuwa mali yako lazima uitunze, huwezi kumwachia mtu mwингine akakutunzia mali yako kwa sababu hatofanya hivyo. Waingereza wanasema, *you have to spend a funny to make a funny*, lazima shilingi ile uitumie ili iweze kutengeneza shilingi mbili zaidi. Sasa kwa miaka yote hii sisi hatukuwa na doria ya aina yoyote ya kukidhi haja ya kuweza kutunza mali yetu huko baharini. Ni mategemeo yangu kuwa sasa Serikali itakuwa na vyombo vya kisasa na kudhibiti ubadhirifu unaotokea hasa unaofanywa na meli zinazomilikiwa na makampuni ya nje.

Vile vile, tunapoletewa Muswada kama huu wakati kama huu, wakati ambao tumekuwa na mabadiliko makubwa yaani hatuko tena katika siasa za ujamaa, tuseme wazi, sasa hivi tuko katika ubinafsishaji, tuko katika soko huria na pia tuko katika mashindano kwa hiyo tunapoletewa Muswada kama huu tuweze kuupitisha, Sheria haina nafasi ikawa na kigugumizi. Nasema hivyo kwa sababu ukifungua ukurasa wa 47, sijui Mheshimiwa Andrew Chenge atatufafanulia vipi? Mimi si Mwanasheria lakini katika ukurasa wa 47 hapa katika kifungu (j) nadhani kifungu hicho kinasema: “moja katika kazi ambazo zitafanya na *director* ambaye atateuliwa kutohana na Muswada huu ukishakuwa Sheria ya kuwa yeche *ata-prohibit* au *ata-restrict the use of explosives for the purpose of fishing*.”

Sheria hii ina *prohibition* au *restriction of the use of any poisonous chemical or toxic substances for the purpose of fishing*. Sasa hiki ni kigugumizi kwa sababu

ukishatambua kama wewe ni mamlaka na Serikali ndiyo mamlaka yenyewe, Wizara ndiyo mamlaka kuu, ukishatambua ya kuwa kuvua samaki kwa kutumia baruti au kwa kutumia kemikali ni haramu, kwa nini unasema ama ita-*prohibit* au ita-*restrict*, uki-*restrict* maana yake utapunguza kazi kwa maana nyingine ni kuwa utaruhusu iendelee. Kwa hiyo, napenda kusema ya kwamba, hii ibadilishwe, hili neno *restricting* liondolewe kabisa hapa. Serikali itambue ya kuwa hii ni haramu na kwa hiyo ina *prohibit* kabisa, hakuna sababu wala wakati wowote ambao Serikali itaruhusu, ile ndiyo maana ya *restrict*. Restriction maana yake siyo *complete prohibition*, inaacha upenyo hapo, kwa hiyo hii isiwe na upenyo, *prohibition* iondolewe. Kwa hiyo, hicho ni kigugumizi ambacho nimekiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa ujumla wake, Muswada huu una vipengele vingi sana ambavyo ni vizuri hasa pale katika ukurasa wa 21 inapoelezwa jinsi itakavyowawekea mazingira mazuri wavuvi wadogo wadogo na kuweza kuwasaidia katika teknolojia nyepesi nyepesi, ambazo tunaweza kuzimudu na vile vile kuwaachia *territories water* za maili 12 ziwe ni shamba, yaani ni bahari ya wavuvi wetu wadogo wadogo na wale wenye meli kubwa kubwa au wenye meli za nje wasiruhusiwe kuvua katika eneo hilo. Hilo ninalifurahia lakini kuna mengine ambayo naona ni alinacha, kama vile ilivyoainishwa katika ukurasa wa 25 na 26(n) na (q). Ukurasa wa 26 kuna ahadi nyingi sana tunapewa pale ambazo nyingine haziwezi kutekelezeka kwa mfano, wanasema ya kuwa *management and control of the fishing industry* watakachokifanya ni ku-*restrict your foreign fishing vessels in territorial waters*. Kama hatukufanikiwa kwa miaka 43 kwa sababu vyombo hatuna, sidhani kama leo tutaweza kufanikiwa.

Kipengele kingine ambacho ni (n) kinasema: "*examining the performance of the existing fishing gear, methods and substituting for them those which are consistent with responsible fishing*" au katika (q) inayosema: "*establishing effective mechanism for fisheries monitoring, surveillance, control and enforcement, to ensure compliance with conservation and management measure as well as those adopted by regional or sub regional organizations or arrangements.*" Mimi sidhani kama huko tunaweza kufika kweli kwa sababu hatuna vyombo lakini nitaeleza baadaye mbadala gani mzuri ambao tunaweza kuufanya ili kuweza kutimiza lengo hili na kuweza kupata usalama katika bahari zetu ili watakaoshiriki katika kuvua kule wawe wanavua kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 33 na hasa katika maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria, Kamati yenyewe ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, inaeleza ya kuwa kulikuwa na ushirikiano mzuri baina ya Tanzania Bara na Visiwani. Hapa mtanisamehe lakini nitaitetea Zanzibar, sioni ya kuwa hayo masikilizano yaliyotajwa katika maoni haya yameainishwa humu, sioni hata ile Zanzibar, sijui labda imetajwa Zanzibar nimeipita sikuisoma vizuri, lakini ninavyoona ni kuwa hata neno Zanzibar halikutwaja, sasa ni vipi mnasema ya kuwa hapa inasema kuihusisha kwa namna moja ama nyingine, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wakati wa kutengeneza Sheria hii na ya kuwa Zanzibar kwa namna moja au nyingine itafaidika na Sheria hii?

Kwanza, ukisikia meno linasema kwa namna moja au nyingine, ujue hakuna kitu hapa, usikishasikia kwa namna moja au nyingine, hakuna kitu. Hakuna kitu chochote humu, Zanzibar inatajwa katika ukurasa wa 16 kama Kisiwa wala sio kwa jina lake, tena inatajwa katika *definitions*, nini maana ya *definition* ya *territorial waters* inasema, *territorial waters means the waters within the area extending offshore to a distance of twelve nautical miles, measured from the mean low water line along the coast of Mainland Tanzania and the adjacent islands* na visiwa vilivyo karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema hayo kwa sababu kumekuwa na mapungufu mengi sana, hizi Sheria tunazozitunga hatuzitengenezi hapa Bungeni hasa ukijaribu kuzi-fit katika Muungano wetu wa Zanzibar na Bara, kuna mapungufu mengi ndiyo maana Mheshimiwa Andrew Chenge, anapata shida sana mara nyingine anachukua uzi na sindano kujaribu kuunga unga, kushona shona vitu na mara nyingine havishoneki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yapo malalamiko, Unguja wanalamika ya kuwa hakuna mipaka huko baharini ya *exclusives economic zone*, haikuwa *defined* vizuri, wao wanayo ile *solve mails* ya *continental shape* ile ya *territorial waters* lakini wakiingia kwenye *economic zone* kule wanamezwa na Bara. Kwa hiyo, hata mara nyingine wanapata shida sana kutoa *licence* wakawaelekeza wale wavuvi wavue sehemu gani kwa sababu wanajikuta wanavua sehemu nyingine ambayo inamiliwa na huku Bara. Lakini vile vite kuna *contradiction* kubwa nyingine kwa sababu sisi ni *signatory* wa *convention* ya *international maritime organization* na kama *signatories* wa *maritime organization*, tumeingia kule na *we are signatories* kama *Republic of Tanzania*. Katika *convention* yao imetoea *definitions* nzuri kabisa baina ya huku Bara na *Island*, zime-*define* vizuri *territorial waters* na *ime-define exclusives seas economic zone*, lakini sisi hizo hatuziheshimu. Kwa hiyo, huu Muswada tulioletewa una upungufu huo wa kuwa hatujawatendea haki Wazanzibari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri wetu wote hawa kwa bahati nzuri wanaishi *Oysterbay* na wanapokaa huko usiku wa manane mara nyingine huwa wanaamshwa na mabomu yakipasuka, yanapopasuka mabomu yale yanaashiria ya kuwa kule Pwani kuna watu wanapasua mabomu yale wanatumia *dynamite* kwa ajili ya kuvua samaki. Serikali yetu haijafanya lolote kuzuia hilo kwa miaka 43, afadhali wakati wa ukoloni kulikuwa hakuna jambo hilo, watu walikuwa wanaheshimu Sheria. Mimi nilikuwa nataka kuuliza kwamba, sijui wanapata wapi hizi *dynamite* za kuweza kutumia kuvulia baharini? Hatuulizi maswali hayo na wala hatujitahidi kujaribu kuzuia *dynamite fishing!*

Lakini *dynamite fishing* athari zake ni kubwa mno kwa sababu matumbawe yale ya Pwani, ukienda pale Dar es Salaam, Msasani yote ile unakwenda pamoja na Kunduchi na mpaka unakaribia Mbegani, yote ile imekwishapasuliwa huko chini, imekwisha *crack* kwa hiyo na huko ndiyo kwenye mazalio ya samaki, ndiko wanakotaga kule. Kwa hiyo, matumbawe yote yameharibika kwa sababu ya hawa watu wanaotumia *dynamite*. Sasa tunaambiwa ya kuwa Sheria hii itatoa adhabu kwa watu watakaotumia *dynamite*, ni matumaini yangu kuwa tutafika huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa kueleza ya kuwa miezi miwili iliyopita nilipata watu kutoka nje, wawekezaji amba walitaka kuleta meli zao hapa ili wavue, nikawapeleka kwenye Idara ya *Fisheries* ya Wizara hii kule *Ardhi House*. Nikaenda nadhani ghorofa ya pili au ya tatu, nikaelekezwa kwenye chumba kimoja ambacho kwa macho nikakipima kilikuwa kama mita nne kwa mita tatu na nusu. Chumba kile ni muhimu sana kwa sababu ndiyo kinachotoa *licence* za meli zote za nje na za ndani zinazokwenda kuvua na vile vile ndiyo chumba ambacho kinamhifadhi Afisa anayeshughulikia doria na udhibiti (*Surveillance and Control*). Ni akina mama wawili wazuri sana na sizungumzii uzuri wao wa sura tu, yaani walikuwa wazuri kwa tabia, walnipokea vizuri pale yaani *public relation* yao, sisi tunajua ya kuwa unapokwenda kwenye Ofisi za Serikali ni ujeuri tu, ukisalimia hali yako dada au hali yako mzee, vipi mambo, anakwambia hebu subiri kule kwanza nina kazi hapa, lakini wao walikuwa na *public relation* nzuri na nimefurahia sana. Afisa Mkuu wa Leseni za Uvuvi alikuwa ni *dictionary* ya *information* yote tuliyokuwa tunaitaka...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hashim Saggaf, naona hiyo ni kengele ya pili.

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sikuisikia kengele ya kwanza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya pili ili niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Muswada huu. Vile vile, nisingependa kumsahau Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoa na wataalam wake wote, ambao wametuletea hasa kitu ambacho tulikuwa tunakisubiri kwa miaka mingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo, napenda nianze na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa lengo la kuboresha Muswada, napenda nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na hili eneo la utawala na nitakwenda kwenye Ibara ya 4(4) na (5), sehemu hiyo inasema hivi na ninanukuu: "Where the Director is required or empowered by this Act to make a determination affecting or likely to affect the rights of any person or the opportunity for any person to undertake any activity, shall give that person reasons for such decision." Then five: "any person

aggrieved by the decision of the Director made in accordance with subsection (4) may within thirty days appeal to the Minister."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi na ukiangalia sana kazi ya huyu *Director* atakayeteuliwa, ndiye atakuwa mshauri mkuu na mtaalam aliyebobea katika masuala ya uvuvi na wataalam wake. Sasa kama anatoa maamuzi ya kitaalam kama yalivyoainishwa katika Muswada huu ambao una maneno mengi, tasfiri zaidi ya 100, ni dhahiri kabisa yule atakayekwenda kwa Waziri, atakapokwenda Waziri atatoa maamuzi kwa kuzingatia masuala ya kitaalam. Labda Muswada ueleze wazi kabisa kwamba, Waziri atakuwa tena na kundi la wataalam ambao watamshauri ili kuweza angalau kutenda haki, vinginevyo kama Sheria inabaki hivi hivi, nadhani tutakuwa kama vile tunampaka mafuta tu yule anayekwenda kwa Mheshimiwa Waziri kukata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kushauri kwamba, hiki kipengele kiangaliwe, ninafahamu kuna Sheria nyingi sana, kuna utamaduni mwangi sana na mimi nimekaa miaka 30 kwenye Serikali, naweza kuwahakikishieni kabisa kwamba, wataalam wakishaamua, Waziri kwa kweli hana la kuamua, kazi ya Mheshimiwa Waziri ni sera na siyo utendaji. Kwa hiyo, ningedhani labda hiki kipengele tukiangularie kwa undani zaidi kwa lengo la kuwatendea watu haki vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa nilizungumzie kuhusu Muswada huu ni Ibara ya 6(1) na (2), hapa inahu *conflict of interests*. Kinachozungumzwa hapa ni kwamba, ikiwa Ofisa atakuwa anahusika moja kwa moja au kwa njia moja au nyingine na shughuli zinazohusiana na Muswada huu, inatakiwa atoe taarifa kwa mkubwa wake. Lakini Sheria hii haisemi popote kama asipotoa atafanywa nini kwa sababu hili ndiyo tatizo kubwa sana katika utendaji wa Serikali na sasa hivi tunazungumzia Utawala Bora, tunazungumzia uwazi na ukweli lakini inabaki nadharia tu.

Ukiangalia sana ukaenda kwenye kifungu kinachozungumzia kuhusu adhabu, hakisemi lolote kuhusiana na huyu Ofisa ambaye ameshindwa kutimiza hiyo kanuni. Labda mimi nashauri kipengele hiki kama tunashindwa kuweka apate adhabu gani, basi huyu awajibike moja kwa moja kwenye Sheria ya Maadili na Viongozi labda hapa itakuwa na maana lakini tukiacha hivi hivi patakuwa na *omission* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ninayotaka kuijadili kwa kifupi ili kupata ufanuzi ni Ibara ya 8(1), ile sentensi ya kwanza inasema: "*The Director shall use his best endeavors to ensure that ...*". Kadhalika neno hili linajirudia tena kwenye kifungu kidogo cha pili, sentensi ya mwisho nayo inasema: "*their best endeavors.*"

Mimi ninavyoolewa neno "*best*" kisayansi halikubaliki, sina hakika kama kisheria linakubalika kwa sababu halina mipaka, itafika mahali ukimwuliza mtu ulifanya nini anasema *I did my best endeavors, so is undefined*. Nadhani ni vizuri maneno ya namna hii tuyepuke hasa wakati huu ambapo tunahitaji kufanya vitu ambavyo tunaweza tukavipima. Ninavyofahamu hili neno *the best endeavors* ni zuri sana katika masuala ya kisanii.

Ninaomba suala hili nalo tupate maelezo hasa tukizingatia kwamba, *the learned brother is preceding kwa hiyo*, atatusaidia sana Mheshimiwa Ntagazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda nichangie Sehemu ya Tatu inayozungumzia maendeleo ya sekta ya uvuvi. Mambo mengi sana yamezungumzwa lakini huwezi kuendeleza sekta ya uvuvi bila hasa kujua mambo ya msingi nayo ni kufahamu au kutambua aina ya jamii ya samaki iliyopo katika nchi yetu na vile vile ni kiasi gani tunao, watakubaliana nami kwamba, hili ni tatizo. Hili ndio suala la msingi litakaloweza kutuhakikishia kwamba, tunazungumzia kitu ambacho tunakielewa. Sasa hivi kuna aina ya samaki ambaao wanapotea bila kuwa kwenye kumbukumbu yoyote ya wataalam. Nadhani itakuwa ni hatari kama tutadhani kwamba, tunaweza tu tukafanya mambo ya kuvuna na nini bila Serikali kuweka mambo ya msingi nayo ni *species identification and how much can be harvested*. Haya ni mambo ya msingi kabisa, ambayo najua yanaghanimu fedha katika kuhakikisha kwamba, hii raslimali yetu ya uvuvi tunaivuna kwa njia za uendelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi kwa kweli kutokana na uharibifu wa mazingira kwa sababu mbalimbali ikiwemo hii ya matumizi ya baruti na kadhalika, lakini vile vile kuna matumizi tu ya madawa ya kuua wadudu, kilimo kisichokuwa kwenye *level* kwa mfano, katika eneo la Ziwa Nyasa, miaka ya nyuma palikuwa na samaki wengi sana aina ya mbufu, mbasa na kadhalika, sasa hivi samaki hawa hawaonekani, wamekwenda wapi? Je, kuna taarifa yoyote kutoka Serikalini? Haya mambo hayajulikani. Lakini ukienda upande wa mwambao maeneo ya kuzalia samaki yanakwisha siku hadi siku matokeo yake tutafika mahali ambapo tutaona kwamba, tuna mipango mizuri sana katika sheria lakini utekelezaji wake sio mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile yako matatizo ya mpaka kwa mfano, katika sheria hii tunayozungumzia sasa hivi, inazingatia masuala ya Tanzania Bara haisemi mambo ya Tanzania Zanzibar, lakini ni lazima tukubali kwamba, hapa tunashughulika na raslimali ambayo haitambui mipaka ya binadamu. Kwa namna moja pengine sikubaliani na ushauri wa Kamati katika hoja ya kusema kwamba, mpaka kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ufahamike. Hii ni sawa kiutawala lakini linapofika suala la samaki ambaao wanataga Tanga wanakwenda Zanzibar na mpaka kule kwenye *Exclusive Economic Zone*, sasa huu mpaka wewe utakusaidia nini?

Haya ni mambo ya msingi kabisa katika kuhakikisha kwamba, tunaposhughulikia raslimali ambayo ni *trans-boundary*, haitambui mipaka ya kiutawala, lazima sheria zetu zioanishwe. Sio vizuri sisi kuzungumzia kwamba tunataka kuwa na ushirikiano na nchi za SADC, ushirikiano na nchi za Afrika Mashariki, lakini tunashindwa kuoanisha sheria zetu kati ya Tanzania Bara, pamoja na Zanzibar. Nadhani sheria hii ndio ingekuwa msingi namba moja wa kuhakikisha kwamba tunadumisha muungano wetu. Hivi ndio vitu hasa vinavyoweza kutuunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda niseme neno la jumla tu kwamba, kazi ya uvuvi ni ya kitaalam, hawa wataalam kwa kweli wanafanya kazi katika mazingira magumu na wanahitaji vifaa vyia kisasa. Kama wenzangu walivyosema

kwamba, wavuvi haramu wanakuja, wanatuibia na wanaondoka, kama hatutatumia raslimali yetu kuwafanya hawa walinzi wetu waweze kufanya kazi zao vizuri, maisha yao yawe mazuri, waweze kupata mishahara mizuri, nadhani tutakuwa tunazungumza kitu ambacho hakitatusaidia tutakapoamka tutakuta raslimali yote imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, napenda nikubaliane na Kamati iliyopitia Muswada huu kwamba, Muswada huu pamoja na kwamba unawalenga watu lakini ni vizuri ukatafsiriwa kwa Kiswahili ili watu wausome na waelewewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile moja ya matatizo ambayo Wilaya zetu zinayapata ni kuwa hakuna wataalam, wote walipunguzwa kazi. Napenda Serikali iangalie sasa baada ya kuwapunguza hao wataalam tutafanya nini; je, tunaweza kuanza sasa kuwafundisha wavuvi wenyewe ili wakafanye kazi hiyo? Je, tunaweza kuanzisha shule angalau hata watu wakahuduria kwa siku mbili au kwa siku tatu hata wiki ili waweze kuendesha uvuvi bora? Nadhani suala la elimu hasa kwa walengwa ni la msingi zaidi katika kufanikisha utekelezaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo kama nilivyosema hapo awali, naunga mkono Muswada huu asilimia mia kwa mia na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono Muswada huu. (*Makofi*)

MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie Muswada huu ambaa ni muhimu. Kwanza, naomba kusema kwamba, naunga mkono hoja na yapo nitakayoyazungumza kwa matumaini kwamba, yatazingatiwa katika kuboresha utekelezaji wa Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kusema Muswada huu unahitaji kuwa na mtazamo ambaa kidogo unamwangalia mvuvi kwa mazingira tuliyomo sisi. Ukiutazama Muswada huu unaelekea zaidi kwa wavuvi wakubwa, pamoja na kwamba hapa na pale umetaja wavuvi wadogo wadogo lakini ukija kwenye utekelezaji sikuona mahali ambapo hawa wavuvi wadogo wadogo wamewekewa umuhimu wa kuwaendeleza ili waweze kufikia mahali ambapo tunapatazama kama tunavyotazama wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida wavuvi ni watu wanaoishi karibu na maji na maisha yao, utamaduni wao, uchumi wao, umeambatana sana na muunganiko wa maji, ardhi na vilivyomo ndani ya maji na wana ujuzi wa hali ya juu kwa mazingira haya. Moja ambalo halijafahamika vizuri katika Serikali ni kwamba, huu ujuzi haujatiliwa maanani hata kuandikwa tu kwamba, je, watu hawa wanaoishi kama Mafia ni kwa kiasi gani wanaifahamu Bahari, watu wa Kojani, watu wa Ukerewe, watu wa Izinga wote hawa wanafahamuje mazingira haya ili yaweze kuwa *documented* na ndio kiwe chanzo cha kuweza kutumia maarifa haya ambapo wao wamezaliwa na wanaishi humo wanayaifahamu vizuri sana?

Kwa hiyo na wao wachukuliwe kama wadau wa kweli kweli kwa sababu wakati mwingine kwa sababu uvuvi wa biashara umewekewa mkazo zaidi kwa kuwaletea watu kwenye mazingira yao, wamevunja hata miiko na utamaduni wa uvuvi na sheria zinapotungwa haziainishi kati ya mtu ambaye uvuvi ni utamaduni wake na mtu ambaye ni mchumaji tu. Nafikiri tutakapokuja kutekeleza sheria hii tutakuja kuiangalia kwa makini zaidi isije ikafikia mahali utamaduni wa uvuvi ukavurugwa ama maisha yao yakawa ya dhiki sana kwa sababu tu ya kutaka kutekeleza sheria hii ambayo tumeipitisha, ambayo tunafikiria kwamba itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wamekuwa na mchango mkubwa sana katika Pato la Taifa. Ukiangalia kiasi cha samaki wanaotolewa *Lake Victoria* kupelekwa nje ya nchi ni kikubwa sana, lakini ukiangalia uzito huo huo na kiasi gani kinachotolewa ndani ya Mfuko wa Taifa kuelekea kwa wavuvi hawa ni kidogo sana. Mara nyingi wameachiwa wenyewe wahangaike kutafuta nyavu, vifaa vyta kuvulia bila kuwekewa mkazo na bila kupewa gawio linalostahili katika kuendeleza sekta hii ya uvuvi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni kubwa zaidi na ambalo lazima tulizingatie sisi tuliozaliwa na kukulia kwenye visiwa kula samaki ilikuwa sio tatizo, unakula samaki tangu asubuhi mpaka unapokwenda kulala wakati wote unaweza kula samaki, ndio maana wengi ukituona afya zetu kwa kweli zinaridhisha, hatukuwa tunafahamu mambo ya utapiamlo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi kwa sababu ya kutoangalia sekta hii na imekuwa ni biashara tu watu wameanza hata wanaotoka sehemu za Visiwanî kukosa lishe ya samaki kwa sababu samaki wote wanachukuliwa lakini mvuvi huyu hanufaiki kwa kiasi kikubwa na wale samaki amba yoeye anawavua kwa sababu ya soko lilivyoandaliwa ni soko la unyonyaji huyu atavua atauza kwa bei ya kutupa na hawezitena kukidhi mahitaji yake na hivyo mzunguko huo wa umaskini unaendelea. Kwa hiyo, hilo nalo baadaye lazima tulitazame na tuweze kulidhibiti ili watu hawa nao wasije wakaingia kwenye mzunguko wa kupata utapiamlo, suala ambalo halikuwepo hata mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu kuna sehemu inayozungumzia uhusiano wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, suala hili nalipongeza sana. Kwa sisi tunaotoka maeneo ya majini tumekuwa na tatizo kubwa la kushtukia mnaambiwa kuna *over fishing* lakini *over fishing* hii ni sababu ya kutoelewa mazingira. Watu wamepata leseni kwa mfano, Wilaya ya Ukerewe ina ardhi ambayo ni *square kilometer* 640, maji ni *square kilometer* 6,000 kwa maana hiyo ile Wilaya sehemu kubwa ni maji na kwa maana hiyo uchumi wa Wilaya ile ungetegemea eneo kubwa ambalo ni maji lakini linaachwa bila kuuliza *Local Government*, vijiji unashuklia watu wanapuyanga tu wanakuja kuvua, wanafanya kila ghasia, wanaleta ujambazi na nadhani hili ni sawasawa na wenzetu amba wako kwenye Visiwa vya Zanzibar, Mafia na kwingine. Kwa hiyo, hili napenda lisitisizwe ya kwamba, mvuvi yejote ambaye ni mfanyakishara, anapoingia katika Wilaya ya uvuvi, basi kuwepo na kuheshimu ya kwamba, eneo hilo sio *free land* ama *free water*, maji yale ni sehemu ya Wilaya na wakiingia waingie kwa utaratibu amba unajulikana katika Wilaya hiyo. Hilo ni moja ambalo napenda kulizungumzia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Lake Victoria* tumepata matatizo, kuna wavuvi wa biashara ambao wakifika katika eneo fulani wanalifanya ni himaya yao, wavuvi wengine wadogo wadogo hawawezi kwenda kuvua kwenye eneo hilo na wanalilinda kwa bunduki. Kwa hiyo, huu ni unyanyasaji wa watu ambao utamaduni wao, uchumi wao kwa karne na karne umetegemea uvuvi. Wengine wanategemea kilimo cha pamba, wengine mazao ya mifugo, hawa wanategemea uvuvi kwa hiyo, wanayo haki ya kuwa na kauli katika utoaji wa leseni katika eneo lao. Sisi kwa mfano, Wilaya ya Ukerewe tungakuwa hatuna *over fishing*, kama watu wangejipanga na ndio namna pekee ambayo inaleta ajira kwa watu, mtu akipata leseni kutoka Wizarani wote wakajazana katika eneo letu kwa sababu tu amepata leseni, hawa vijana wetu ambao ardhi yao ni ndogo na badala ya kuajiriwa kwa ajili ya kilimo cha ardhi wanajari majini, wanakosa fursa hiyo na wanakuwa ni watangaji na wahamaji kwa sababu wamekuwa *displaced*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu Mfuko wa Uvuvi. Nilipoona Mfuko wa Uvuvi nilifurahi sana lakini niliposoma ndani haujakidhi mategememo yangu kwa sababu katika Ilani ya Uchaguzi tumesema kwamba, tutasaidia vikundi vya ushirika katika kuvua, kufuga na kulima. Lakini Mfuko huo umelenga zaidi katika kuboresha *bureaucracy* ya Wizara, *research*, lakini mahali ambapo mvuvi anayetoka Mafia anaweza kusema naenda kwenye Mfuko wangu kukopa sikuiona, haipo. Ni kasoro kubwa ambayo Wizara lazima iangalie kama imekuwa ni bahati mbaya, Mfuko huo uundwe kwa sababu sasa hivi ukienda Benki mvuvi hana nafasi. Watu wengi wanafahamu Benki anakopa mkulima na mfugaji, mvuvi hana nafasi na Bahati mbaya sana sekta ya uvuvi watu wengi hawailewi. Kwa mfano, *Micro Finance* mara nyingi utakuta wanakopesha Sh. 50,000/=, hizi kwa mvuvi hazimfai hata kidogo kwa sababu katika uvuvi wa kawaida kwa mfano wavuvi wale wanaotega dagaa katika Ziwa Victoria ule mtumbwi akitaka avue bila kuharibu mazingira ni Sh.400,000/=, *engine* ambayo itamwezesha kutoka Pwani ili asogee ndani ya maji asije akavua kwenye mazalio ya samaki ya chini kabisa ni Sh.1.6 milioni, ukiweka nyavyu, karabai na vitu vingine, lazima mtu awe na mtaji usiopungua Sh.3.3 milioni ndio anaingia majini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea basi kwa sababu ya ukosefu wa mitaji badala ya kuwabdalisha hawa wavuvi ambao ndio kazi yao kwa asili waendelee kuvua, tumewafanya wawe manamba katika vyombo vya watu wenyepesa ambao asili yao sio kuvua na kwetu kabisa wanasa namba, kwa sababu mtu ana mitumbwi yake 10, 20 anamwita hawezi huyu kupata milioni 3 kwa utaratibu tulionao. Kwa hiyo, Mfuko huu nilifikiri utasaidia sana kuwakomboa hawa wasiendelee kuwa manamba waweze kuondoka kwenye umaskini na hawawezi kuondoka kwenye umaskini kwa sababu anakuwa ni kibarua kwenye mtumbwi wa mwenzake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabla sijapigiwa kengele ya pili, nadhani lipo tatizo lingine, *industrial development* sioni sababu yoyote kwa nini Serikali isisaidie Visiwa hivi kuwa na viwanda vya kusindika samaki. Nashangaa mtu anatoa samaki mahali ambapo wanavulia anapeleka mahali wasikovulia kwanza, *quality* ya samaki inapungua sana kwa sababu samaki anapaswa *immediately* akitolewa majini aingizwe kwenye barafu na katika uvuvi ulioendelea meli zinakuwa zime-park wana-process pale

pale. Lakini sisi kwa sababu ya kujenga msururu wa unyonyaji, unakuta mtu anakimbizana na samaki kutoka kwenye Visiwa kwa mfano, kule kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Ruth Msafiri mpaka Mwanza kuja kuuza kwenye viwanda badala ya labda Pwani iliyoko karibu na Muleba kule ndio ingekuwa na kiwanda ili samaki waweze kuwa-*processed* haraka iwezekanavyo. Nafikiri Ukerewe ingeweza kuwa *donor country* kama tungepewa uwezo wa kusindika mazao haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu haya mambo ya kusema watu wajitegemee jamani tunapoteza muda. Hivi kweli unategemea Wilaya kama ya Muleba, Wilaya ya Ukerewe na kipato chetu kama mnataka kuondoa umaskini muwaachie eti wenyewe ndio wajenge kiwanda ambacho ni *standard*, lazima tusaidiwe. Kwa hiyo, lazima tusaidiwe kujenga viwanda ambavyo ni *standard*, lazima tusaidiwe kupata masoko ya kuuza, unakuta *made in Ukerewe, made in Muleba* kwenye soko la New York, lakini sio mtungoje tuhangaikehangaike mwisho tuanguke katika mikono ya walangazi amba wanatulangua na hatuwezi kuondoa umaskini.

Umaskini mwingine ni umaskini batili, sisi amba tuko kwenye sekta ya uvuvi tusingepaswa kuwa maskini hata kidogo kwa sababu tungekula vizuri, tungezalisha vizuri na pesa nyingi tungeweza kutoa gawio katika maeneo ambayo hayana uwezo. Sasa nataka kuuliza swali hivi ni kweli katika Ziwa Victoria hatuwezi kuvua kwa meli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo lakini naunga mkono hoja kama mtanahakikishia kwamba, kutakuwa na Mfuko wa kuwakopesha wavuvi wadogo wadogo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mongella, naona Wabunge wa Muleba wote wanapiga makofi kwa bidii, pamoja na Mheshimiwa Masilingi. (*Kicheko*)

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumshukuru Waziri na watendaji wake, Katibu Mkuu na wengine katika Ofisi kwa kuleta Muswada huu Bungeni ili tuweze kuutolea maamuzi na kuujadili kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimefurahishwa na utaratibu huu, sina ugomvi na kufuta ule Mkataba wa 1970 kwa sababu una mapungufu mengi, huu unaonekana una utaratibu mzuri, una uvuvi endelevu, una mipango ya kisasa na una utaratibu amba unaweka wazi mambo ambayo sasa tunataka kuyafanya katika shughuli zetu za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo napenda kuanza nalo ni suala la usimamizi wa maliasili. Katika Muswada imeelezwa wazi kwamba uko endelevu, tutasimamia, tutavua kwa utaratibu, samaki wabaki kama maliasili nyingine tuliyonayo hapa nchini. Katika hili, ukiangalia sehemu hii ya ubora, matatizo ambayo tuliyapata juzi juzi na watu wa *European Union*, mazao yetu ya samaki yakakataliwa kununuliwa kule

Ulaya ni kweli kwamba, mpango na yote yaliyoainishwa kwenye Muswada, naomba yaelezwe vizuri na kwa wengine hasa kwa wavuvi wanaohusika na kazi hii. Elimu kwa wavuvi mpaka sasa hivi bado haijafika, wavuvi wanajifanyia mambo yao wenyewe tu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hali halisi ya uvuvi tulionao na Muswada unatulenga sisi wote kwa sababu wavuvi tulionao ni wavuvi wadogo wadogo karibu nzima. Wanaoleta samaki kwenye viwanda vya Mwanza kwa ajili ya kusafirisha Ulaya ni wavuvi wadogo wadogo, wanaopeleka Musoma ni wavuvi wadogo wadogo na vingine kote ambako vimejengwa ni wavuvi wadogo wadogo. Kwa hiyo, suala hili la kuboresha na utaratibu mzima wa kuelewa kazi hii vizuri, naomba Wizara iweke utaratibu wa namna gani iwasaidie kwa kuwaelimisha, kuwasaidia, kuwapa mwanga ili washiriki vizuri na wasifanye vibaya kama wanavyofanya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala moja ambalo napenda kuliuliza hapa ni katika Sehemu ya Tano, kifungu cha 3 na 4, kuhusiana na usimamizi hasa madaraka ya Mkurugenzi. Tuna maeneo mengi ambapo tunavua, huyu ndiye anayepaswa kusimamia, kutoa leseni, kuandikisha vyombo vyote labda wanashahau kwamba kuna mitumbwi maana hapa anazungumzia *vessels*, sijui ana maana ya meli? Kuna mitumbwi mingi ambayo inavua *Lake Tanganyika* ipo, *Lake Victoria* ipo, sasa huyu yuko mbali, naona hapa kuna *bureaucracy*. Naomba Wizara iangalie jinsi ya kuwasaidia hawa watu ili huyu Bwana aweze kuwafikia kwa sababu wao itakuwa ni vigumu kumfuata Dar es Salaam. Naomba vifungu hivi viangaliwe kwa makusudi kabisa kama nilivyosema ili tupunguze huu urefu na umbali wa Mkurugenzi ili hawa watu wa maeneo haya waweze kumfikia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ninataka nikisemee kwa karibu ni hii Sehemu ya 18, ambayo inahusiana na usimamizi kwenye mialo kuhusisha jamii. Kwa kweli wazo hili ni zuri na nampongeza Waziri kwa wazo hili na naomba likomazwe zaidi kwa sababu hawa watu ndio watakaoleta taarifa zote muhimu, ndio watakaowaona wanaotumia sumu, wanaoendesha makokoro kule, wanaochoma mialo. Hawa watu kwa kweli kama inavyoelezwa katika kifungu na sehemu nzima ya Muswada, ningeomba pale ingeongezwa sehemu moja kwamba, wapewe nini kwa sababu kazi watakayokuwa wanafanya ni kubwa na hawa kama wataelewa na watakuwa na mwamko wa kutosha kuhusiana na uvuvi huu, watasaidia sana kusimamia na kuhakikisha kwamba, mazao yetu ya samaki yanabaki sawasawa. Kwa mfano, namna ya kulipata na kulikamata kokoro sio rahisi, huyu mtu anapanga mipango yake usiku na anavua usiku. Sasa usiku kama huo mialo yote hii nani atafika kule na kumsimamia, watakaoweza ni hawa watu walio katika maeneo hayo na ili waweze kufanya kazi yao vizuri, wapate elimu nzuri lakini pia paelezwe kwamba watapewa nini pale. Kwa mfano, katika shule zao wakiongezewa madarasa itakuwa vizuri, wakijengewa *dispensary* itakuwa vizuri, hata kama kuna malipo kidogo walipwe ili waweze kushiriki kwa karibu na kwa moyo wa wazi katika kusimamia suala hili na kuhakikisha kwamba, samaki na mali yetu ndani ya maji inabaki salama.

Jambo lingine hapa ambalo napenda niulize na nipate maelezo yake ni kuhusiana na sehemu hii ya Mfuko. Kwa kweli kama alivyomaliza kuzungumza msemaji aliyejita, hata mimi niliposikia Mfuko nilipata mawazo kwamba, sasa labda hali ya uvuvi itasaidiwa zaidi. Pamoja na kukomaza utawala pale lakini katika maeneo mengine kwa mfano, kwenye pamba, kahawa, wana taratibu nzima hizi za ruzuku na ruzuku hii inatokana na Mifuko yao humo ndani, sasa kwa nini katika samaki pasiwe na ruzuku?

Vifaa vya uvuvi ni ghali sana, hizo *engine* ni ghali, mitego ni ghali, mitumbwi ni ghali, kama unanunua meli nayo ni ghali lakini mvuvi ameachwa mwenyewe afanye hayo. Lakini kila siku tunasema uvuvi umetuletea faida kubwa sasa, hizo hela zote zinakwenda wapi kama haziwezi kurudi kidogo kwa hawa ili ziwasaidie waweze kufanya kazi nzuri na wafanye katika mazingira ambayo ni rahisi kwao, sio hali ilivyo sasa hivi? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unatoka Mbeya, ukifikishwa maeneo ya Ukerewe na Mwanza pale ukiambiwa uingie kwenye ule mtumbwi unaweza ukaogopa na ukakimbia kutokana na hali halisi mpaka uwe na mazoea na utamaduni wa jambo lile ndiyo unaweza kutulia na kufanya kazi. Sasa katika huu Mfuko mimi ningeomba sana waangaliwe kwa makini, kama ni vigumu kukopeshwa waachwe wakope kwenye mabenki, kwenye viwanda vya samaki lakini angalau ruzuku kwenye hivi vifaa vyao iingie ili iweze kuwasaidia hao.

Kingine ambacho nakiona ni cha msingi hapa, ambacho kimejadiliwa kwenye Muswada, pamoja na uboreshaji lakini kuna vyombo ambavyo vinaendana na hali halisi ya kuboresha mazao haya ya samaki. Kuna hizi taasisi ambazo zinahusiana na shughuli hii hazikuonyeshwa huku ndani ya Muswada kama *Research Institutes*, zile zinapaswa ziingie kwenye Muswada huu. Pia Vyuo vya Uvuvi vinapaswa vizungumzwe angalau vitamkwe kwamba vina *role* gani katika kuboresha mazao ya samaki. Kwa hiyo, katika hilo ningeomba Wizara iangalie, ione kwamba inapotekeleza Muswada huu kama kuna mapungufu katika *Research Institutes*, basi itafute namna ya kuyaboresha kwa sababu huko ndiko tunapata viwango, vipimo na tunapata picha ya hali halisi ya samaki wetu na hasa katika biashara hizi kubwa, tunazofanya na *European Union* na sasa mpaka Japan, wanategemea maabara na taarifa kamili kutoka kwenye Idara hizi za Utafiti na Vyuo vya Samaki. Sasa kama hivi havikuwekwa sawasawa na kutamkwa kwenye Muswada kwamba, hali halisi pamoja na haya tunavyo hivi, Wizara itavisimamia ili waungane kwa sababu jambo hili linatakiwa liende pamoja, tuonyeshe uzito wake ili hali hii iwe ya kuridhisha.

Ningependa tu kumalizia kwa kulikazia suala la utaratibu wa usimamizi hasa kuhusiana na kusimamia kazi nzima ya uvuvi. Katika vifungu kwa mfano cha 17, 18 na pia sehemu ya 19, ningeshauri na ningeomba Wizara, kwa vile kuna watu wengine wanaohusika kama Halmashauri, watu wanaokaa kwenye mialo, ambao hii *beach management* taarifa zake, utaratibu wake wa kuzipokea kwenye Wizara ungeandaliwa ili uwe mzuri na wa haraka. Kama kuna uwezekano hata wa kuweka *radio call* kwenye maeneo ambayo ni makubwa, basi iwekwe pale ili linapotokea tatizo liweze kufika kwenye Wizara mara moja na Wizara iweze kuchukua hatua na kulisahihisha mara moja.

Kwa sababu haya yametokea huko nyuma, watu wamekuwa na matatizo kwa mfano, wavuvi wamekuwa na matatizo kwenye eneo lao, yanafanywa labda na wavuvi wa kutumia sumu, wamewaona na wapo tayari kuwatolea taarifa, lakini inakuwa ni vigumu sana sana kuffikisha taarifa. Haya mambo yanachelewesha na kuharibu mali yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningeomba Wizara kwa ukaribu kama ilivyoeleza suala la usimamizi, kwa kweli hao wavuvi hasa katika visiwa vidogo vidogo kwenye maeneo ya *Lake Victoria* kule, usalama wao ni mdogo sana. Wapo watu ambao wana tamaa na hamu ya kupata zaidi, wanakwenda kuwaonea na kuwanyang'anya mali zao, wanakwenda kuwavamia na kuwfanyia fujo. Sasa usimamizi uwe wa namna ya kuhakikisha kwamba, usalama wao unabaki sawasawa kama wengine, utaratibu wa kusimamia na kukagua maeneo haya upangwe vizuri. Nashukuru kwamba, Wizara hii ina *boat* katika maeneo ya Mwanza pale, lakini naona matumizi yake yangepangwa na yakapanuliwa ili ifahamike na iweze kufanya doria kamili kama walivyoeleza hapa. Wakichukua na kuwa pamoja na maofisa wa Polisi kwa nia ya kwamba wakaweke usalama kule kwenye maji, watu wakishaona sasa hali imekuwa ya kawaida, nao wavue katika hali ya usalama na kuridhisha, wawe na starehe siyo kufanya kazi kwenye mazingira ya kupigwa risasi na kutishwa tishwa. Hilo ni jambo ambalo nisingependa lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo nasema tu kwamba, Muswada nimeukubali, mazingira yake ni mazuri na ni wa kisasa kwa kweli, unaangalia hali na unatuweka katika hali endelevu ya shughuli zote za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi nikushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ili nami nichangie angalau machache. Aidha, namshukuru Waziri kwa kututayarishia Muswada huu ambao una nia ya kutukomboa katika uchumi kwa upande wa baharini. Nampongeza Waziri na kumshukuru yeye na watendaji wake wote, nilivyouona ni Muswada mzuri na kama una kasoro ndogo ndogo za hapa na pale ni mambo ya kawaida kwani wanaotengeneza ni binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nianzie katika hali ya uvuvi ambao ndiyo tumetia nia kwamba uwe mkombozi wetu wa pili tukiondoka kwenye kilimo. Bado hatujatulia hasa tukaitazama hali ya bahari yetu na kuitumia ipasavyo. Wavuvi wetu wanavua kwa vyombo dhaifu sana, vyombo vyenyewe si vyombo hasa vya kwenda navyo baharini, lakini inabidi waende kwa sababu maisha yao yote yapo katika bahari hasa ukichukua kama zile sehemu zetu za Visiwani kama Unguja na Pemba, Mafia na kwagineko kama Ukerewe, kama alivyo sema Mheshimiwa Mongella. Sasa utegemezi wetu wa kule ni kutumia bahari ambayo ndiyo ardhi yetu. Sasa kama hatujawa *serious* tukaanza kuitumia bahari, tutabaki hapa hapa na ule uchumi tunaozungumza kwamba unachangia *ten percent* wakati ingewezekana ukachangia hata *fifty percent* kama tutautazama na tutau shughulikia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tumeelekeza nguvu zetu kwenye ardhi, juzi tulikuwa tuna semina hapa ya wachimbaji wa almasi na dhahabu lakini kazi kubwa ni kuichimba ardhi tu, wanasema si chini ya kilomita moja na nusu, jamani siku moja hii ikija kukasirika tutatafuta pa kwenda. Siku moja hapa ilijaribu tu kidogo kujitikisa tukashindana hapa tena kiongozi wetu akawa ndiyo anaongoza msafara wa kutoka nje. Iljaribu kidogo tu, kwamba nayo inasema jamani enhee, mbona hamuikamatii bahari mmeshika huku tu kwangu mimi. Kwa hiyo, jinsi Waziri alivyotayarisha Muswada huu maana yake ni kwamba, sasa tuelekeze macho yetu baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokwishazungumzwa na walionitangulia kwamba, bahari yetu kubwa na tunaweza kuitumia na kunyanya uchumi wetu kwa hali ya juu, lakini pia kutakuwa kuna labda niseme udhaifu kidogo ikiwa kama tutaanza kuweka mipaka na kuanza kugawa baina ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huku Bara. Mimi naona hii hata siku moja haielekei na haielekei kwa sababu si historia yetu wala jiografia yetu haikubaliani, maana hizi zimeungana kama mapacha wawili wa Iran. Bahari yetu imeungana na ndiyo ilioleta Muungano kwa sababu ni moja na watu ni wamoja. Sasa leo kama Sheria hii itakuwa *very strict*, ikawa inamzuia mtu wa Zanzibar asivuke zaidi ya *zone* ile, nasema yatayarishwe Magereza zaidi kwa sababu ndiyo bahari yao na ndiyo sehemu zao, sasa waende wapi? Sasa haya Magereza yatakuwa hayatoshi maana kila siku watu watakuwa wanawekwa ndani kutokana na sheria ilivyokuwa imewabana.

Ninavyojuu wavuvi wa Zanzibar, nakusudia wavuvi wa Unguja na Pemba, mwambao wao ni hapa Kunduchi, sehemu hizi za Pangani, Kipumbwi mpaka Tanga na Bagamoyo, ndiyo mahali pao tena wanakwenda dago, wanalala dago kule, wapo nyumbani wanavua na ndiyo hivyo hivyo watu wanaotoka huku bara kuanzia sehemu za Dar es Salaam, Mafia, wote utawakuta Fungu Mbaraka pale, Fungu Mbaraka ni sehemu ya Zanzibar lakini ipo karibu na Visiwa vya Mafia kule, nadhani Mafia wakikaa vizuri wanaweza kuiona, ipo jirani sana kule na huko ndiko kwenye samaki hasa wa *deep sea* na vyombo vyote utavikuta vya Mafia viro kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba sana Waziri bado akae na ndugu zake ili waweze kuitengeneza hii sheria iende pamoja na ndivyo inavyotakiwa kuwa kwa sababu sasa hivi tupo *strict* katika kuinyanya nchi yetu kiuchumi. Lakini haishii hapo tu lazima tuangalie vile vile kwamba umefika wakati tutafute vyombo vikubwa hasa, leo tunabinafsisha vitu vyote huku, kwa nini basi hatubinafsishi bahari, tukaweza kupata meli za kweli na tukapata kuungana kikweli kweli hasa, tukavua samaki ambaa pale pale wanapelekwa kwenye viwanda vya samaki basi tunatoa samaki, peleka. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie sana upande wa bahari, kwani sasa hivi ndiyo mkombozi wetu aliyebakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuangalie suala la hawa wavuvi haramu hasa wale wanaopiga mabomu chini ya bahari yaani ndani ya maji ya bahari. Unapolipiga lile na ikiwa bahati mbaya si kwa kuvunja matumbawe tu au kuvunja zile nyumba ambazo wanazalia samaki pamoja na maeneo yaliyo karibu penye madimbwi yale, lakini kama kutakuwa kwa bahati mbaya kuna *diver* chini pale, ambaye atakuwa katika *sports diving*,

basi tuhakikishe na yule *diver* naye sasa kawa sehemu ya samaki, litam-*affect* naye atakufa. Ubaya wa bomu kwa sababu lile kwa masafa ya robo kilomita aliye karibu naye anakwenda, kwa sababu linakimbilia kupasua *lungs* na kupasua *ear drums*, moja kwa moja inapasua masikio na mapafu na ndiyo samaki unapompiga maana yake unampasua mapafu hawezo tena ku-*breath* mwenyewe kama anavyo-*breath*, matokeo yake analala na unamkamata. Sasa nashauri sana sana katika haya, lazima tuwe wakali katika kuhakikisha kwamba, bahari yetu haitatumiwa kiharamu mbali ya sumu ambayo inaweza kutembea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sasa umefika wakati wa kuishauri Serikali kuunda *Coast Guard*. Kwa nini nasema hivyo, kwa sababu *Coast Guard* maana yake hasa watashughulikia ulinzi wa mwambao kwa upande wa bahari, magendo na kadhalika. Sasa sisi tunasikitika kila siku kwamba, kuna hawa wanaoteka nyara meli na kadhalika. Sasa kama tusipojiandaa na leo tumeingia katika hali ya Kimataifa tutakuwa sisi tupo, wenzetu wanakimbia na sisi tunatembea. Lazima na sisi tufuate ulimwengu unavyokwenda, lazima tukubali kwamba sasa umefika wakati wa kugeuza. Kama alivyoileta Waziri sheria hii kuigeuza kwa kuona kwamba mna kasoro nyingi za sheria ya mwaka 1970, basi sasa umefika wakati tuikebishe ili kujenga vile vile hali bora ya uchumi wetu katika upande wa baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakizungumzia chuo chetu cha Uvubi Mbegani. Chuo hiki bado hatujakisimamia vizuri, Chuo hiki ndicho kinachoweza kabisa kusaidia katika kutoa wavuvi wazuri na ndiyo hao watakaoweza kusaidia katika kuimarisha uchumi. Chuo cha Mbegani maana yake hasa ni kuimarisha uchumi katika upande wa uvubi. Sasa Chuo hiki tumekiacha katika hali kilivyo ingawa nasikia kwamba kuna nia ya kukiimarisha, lakini sasa tusiwe na nia tu bali tukiimarishe na tena tuimarishe hata wale wavuvi wetu waliokuwa wadogo. Kwani wale ndiyo watajisaidia kuondoka katika umaskini, tuwasomeshe vizuri, tuwape misada inayostahili ili waweze kuvua samaki na wao waweze kupata maisha mazuri, matokeo yake uchumi wa Taifa utakuja juu kidogo kidogo kwa upande wa uvubi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba sheria hii ni nzuri na nasema kwamba, nitaiunga mkono huko mwishoni ninakokwenda, lakini naomba tena Mheshimiwa Waziri, mtazamo wake aangalie zaidi katika suala la kuunganisha uvubi wetu huu, hatuwezi kubaki Zanzibar kwake, Bara kwake au kwingineko, kwani tunaanza kujigawa na hii kidogo inaleta athari katika hii miani yetu. Kwa hiyo, lazima tuione hiyo na ni lazima tuimarishe Muungano wetu, tusiache mwanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili nichangie kidogo katika Muswada ulioko mbele yetu kulingana na masuala ya uvubi. Kwa kweli nafikiri wachangiaji waliopita kwa kiasi fulani wamechangia mengi na kwa mujibu wa kanuni, si jambo zuri kurudia yale yale ambayo tayari mtu ameshayasema. Lakini kwa ruhusa yako ningependa nirudie tu suala moja

kwa kutilia mkazo kufuatana na sheria hii kama alivyozungumza msemaji aliyepita, Mheshimiwa *Colonel*, ambaye kwa bahati yeze ni *Colonel* wa baharini, kwa hiyo, ni mtaalam zaidi wa mambo ya bahari kuliko nitakavyokuwa mimi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri suala la bahari tunesema tunaweka mipaka lakini samaki hana mpaka, kwa hiyo, halitakuwa jambo la busara kuanza kukaa hapa na kujadili kuwekeana mipaka ya samaki huyu atapita wapi, samaki huyu atapita wapi. Uzoefu uliokuwepo kwa Zanzibar, kwa bahati mimi natoka Kusini Mashariki ya Kisiwa cha Zanzibar, karibu sawa sawa na wenzetu wa Seychelles, kama utaweka mstari unaweza kutokeza pale pale na uzoefu uliokuwepo wakati unapokwenda baharini tunapishana pishana sana na vyombo vya uvuvi wa bahari kuu, hatuvijui vinapotoka na hatujui leseni hizi wamekuwa wanazipata wapi, kama wamepata Zanzibar au Tanzania Bara? Kwa hiyo, kuja kwa sheria hii ningeshauri sana Serikali iwe makini katika kutambua na kuamua ni chombo gani kinapewa leseni katika uvuvi na leseni hizi ziweze kutambulika zinatolewa wapi. Ikiwa kama zitatolewa Zanzibar au Tanzania Bara, ziwe na hadhi sawasawa kwamba sote ni Watanzania. Nafikiri hiyo ni sehemu yangu ya kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, katika Muswada huu imezungumzia masuala ya *aquaculture* na kutokana na maendeleo ya dunia sasa hivi suala la *aquaculture* linaambatana sana na shughuli za kiutalii na kwa uzoefu uliokuwepo tunapogawa hizi sehemu kwa ajili ya shughuli za *aquaculture* na kuwapa leseni watu wazitumie sehemu hizi kwa shughuli za utalii, kunakuwa na vitendo ambavyo kwa njia moja au njia nyingine, huwa vinawanyima fursa wavuvi wadogo wadogo kuendelea na shughuli zao. Kwa hiyo, ningeshauri katika suala hili wakati inapokuja kutekelezwa sheria hii, baada ya kupitishwa Muswada huu, kuwe na vipengele maalum ambavyo vitawekwa kuwalinda wananchi ambaeo ni wakulima wadogo wadogo wa baharini na vile vile kuweza kuamini kwa udhati na kuwa na fursa ya kutumia hii taaluma au hali halisi ya *aquaculture* wakati inapohusiana na shughuli za utalii.

Zaidi ya hayo kutokana na suala la *aquaculture* kuna masuala ya kilimo kidogo kidogo kama cha miti ya baharini kwa Kiswahili au kwa Kiingereza tunasema "seaweeds". Hivi karibuni kiasi cha miaka minne au mitano, kumejitokeza masuala yanayohusiana na uvuvi kama wa mwani na hili limekuwa ni zao kubwa sana sasa hivi kwa hapa Tanzania. Zao hili linapatikana kutokana na kutengeneza mashamba katika bahari, mashamba ambayo kwa kweli baada ya mavuno huwa tunategemea kupata kitu kutokana na zao hili. Kwa hiyo, ningeshauri wakati tunapopanga mikakati ya kuweza kuweka mashamba kama haya ya baharini kwa hifadhi, hatuna budi tuwe na utafiti wa kufaa wa kuweza kuona ni sehemu gani ambazo zinaweza kufaa vizuri katika kuendeleza vipato hivi. Wakati ule ule tuweze kujua masoko ya kuweza kuyatumia katika kuuza bidhaa zinazotokana na mazao haya, kwa sababu hivi sasa kupata masoko imekuwa ni tatizo kubwa sana. Ni wiki iliyopita tu wataalam walikutana Zanzibar kuhusiana na zao la mwani na kuweza kutafuta mbegu ambapo yote haya yanatokana na masuala ya *fisheries* kwa ujumla. Kwa hiyo, wakati tunafanya hii hatuna budi kuweza kulizingatia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuliongelea ni suala la utafiti kwamba, wakati tunapotoa leseni, wakati tunaporuhusu na kuendelea na sheria yetu hii, hatuna budi kuwa na utafiti wa kutosha. Wakati tunapofanya utafiti wetu lazima tuwajumuishe wananchi ambao kwa njia moja au nyingine, wanayo taaluma ya kutosha kuhusiana na mambo ya bahari na inapotokea kwamba tumeshapata matokeo ya utafiti ni lazima turudi kwa wananchi tuwaelimishe ipasavyo na hatua yoyote ambayo tutakuwa tayari kuichukua katika kuendeleza masuala yetu haya yanayohusiana na *fisheries* kwa sababu hivi karibuni, si karibuni sana, tulikuwa na masuala ya utafiti kwa Zanzibar na kwa bahati mbaya kuna hii *Institute of Marine Sciences*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba, katika Bunge lako hili tumekuwa tukizungumza mara nyingi kuhusiana na *Institute of Marine Sciences*. Kwa bahati mbaya hapa katika Muswada huu kimetajwa Chuo cha Mbegani lakini kile Chuo cha *Zanzibar Marine Institute* kimesahauliwa. Kwa hiyo, ningeshauri sana kwamba, juhudzi zifanywe kwa kila hali kuweza kuona *Institute* ile inafufuliwa na ninachoshukuru ni kwamba, *Universty of Dar es Salaam* sasa hivi inatia moyo kwamba imevalia njuga na kuweza kukiokoa Chuo kile. Ninashukuru na ninaamini kwamba, kila juhudzi itachukuliwa ili kuweza kuboresha zaidi shughuli za kiuvuvi kutokana na hili na hasa ukizingatia kwamba, katika historia Chuo kile kwa Afrika Mashariki kilikuwa ni Chuo ambacho kinategemewa, kulikuwa kuna *aquarium* pale ambayo haijapata kutokea, haijawahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba, imekufa kabisa, hakuna chochote kilichokuwepo. Kwa hiyo, wakati tunapokuwa na utafiti wetu, tuyazingatie mambo kama haya ili yaweze kuboreshwa zaidi katika Muswada wetu huu na kuweza kuona ni jinsi gani tunavyotekeleza kwa mashirikiano kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Si jambo la busara kuweza kuzungumza kama mwenzetu hapa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, wakati alipokuwa anawasilisha taarifa ya Kamati, labda alipozungumza akasema kwamba Muswada huu utatumika Tanzania Bara na siyo Tanzania Visiwani.

Hili nafikiri inabidi tulizingatie tena au pengine labda katika mazungumzo yake zaidi Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akizungumza kwamba wamefurahi kuona kwamba wenzetu waliishirikisha Zanzibar katika kutekeleza sheria hii. Lakini wamesema Visiwani, kwa hiyo ningefurahi sana kama angesema Zanzibar, asingesema kwamba Tanzania Visiwani, maana pengine visiwa vyenyewe alikusudia vya Mafia au Ukerewe, lakini kama ni Visiwa vya Zanzibar ni jambo la kupongeza na kwamba ni lazima tuwe na mwelekeo na mwenendo kama huu katika kuboresha Muungano wetu huu tuliokuwa nao wa Jamhuri yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina kawaida ya kupigiwa kengele ya pili, kwa hiyo kutokana na hayo napenda niunge mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofifi*)

MHE. ABDILAH O. NAMKULALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada ulioko mbele yetu.

Mimi nina mambo matatu: La kwanza, wavuvi wa Mtwara Vijijini wanasema wameelewa na wanakubali kwamba kuna uvuvi haramu, pamoja na nyavu zenyenye matundu madogo. Wanakubali kuanza kutumia nyavu zenyenye matundu kuanzia inchi tatu.

Lakini wamenituma nimwulize Mheshimiwa Waziri na nimwombe Mheshimiwa Waziri aende akawape utaalamu wa jinsi ya kutumia nyavu zenyenye matundu ya inchi tatu jinsi watakavyoweza kuvua dagaa, watakavyoweza kuvua lupapa, kuna aina ya dagaa wanaitwa lupapa, kuna samaki aina ya vibua ni wadogo mno hawakui hawa hata kwa miaka mia moja, watawauvavua vipi katika nyavu za inchi tatu? Wao hawana matatizo ila wanaomba utaalamu wa jinsi ya kuvua dagaa kwa kutumia nyavu za inchi tatu. Lakini lingine wamenituma nije nimueleze Mheshimiwa Waziri, tafadhali aunde Mfuko wa kuwakopesha wavuvi ili wapate mahali pa kukopa ili wanunue zana za kisasa kwa ajili ya kuvua samaki.

Mwisho, wanaomba sheria hizi za uvuvi ziwafikie mapema na kwa ufanuzi zaidi, maana inaweza wakawa wanapinga jambo bila kujua. Kwa mfano, wavuvi wa Naringu wameniita na kuniambia nenda kamwambie Mheshimiwa Waziri, *hatutaki marine park*, nikawauliza kwa nini hamtaki *marine park*, wakasema hatuelewi sisi tunaona wanachukua bahari yetu eti wanatupa mipaka tusivue samaki, sasa tufanyeje na sisi hatuelewi, hakuna aliyejukua kutuelewesha. Kwa hiyo, kamwambie Mheshimiwa Waziri hatutaki. Kwa hiyo, nikagunduka kwamba, wanahitaji utaalamu, yaani taaluma hawakuipata vizuri. Kwa hiyo, kuhusu sheria hii tafadhali wekeni vipindi katika redio au fanyeni mikutano mtuwezeshe sisi Waheshimiwa Wabunge, tutakwenda kule kuwapa utaalamu zaidi. Ahsante sana. (*Makofsi*)

MHE. STANLEY H. KOLIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Muswada huu muhimu wa uvuvi. Vilevile napenda kuipongeza sana Wizara inayohusika kwa kuleta Muswada ambao mimi binafsi nauona kwamba ni wenye manufaa sana kwa nchi yetu na hasa kwa wavuvi wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuusoma Muswada huu, nimegundua kwamba, Muswada huu unalenga katika kuhamasisha, kuendeleza na kusaidia juhudhi za wavuvi ili kuwa na uvuvi endelevu. Lakini wasiwasidhi wangu wa kwanza unatokana na neno *Fisher* yaani mvuvi lilivyotafsiriwa hapo. Katika Wilaya ya Ludewa kwa mfano, tuna Tarafa mbili nzima zipo katika Ziwa Nyasa, zenyenye wavuvi na hawa kwa tafsiri hii watawaingizwa kwenye matatizo. La kwanza ni tatizo gani? Kwanza, ipo *section* inayosema kwamba, hakuna mvuvi atakayevua samaki bila kuwa na leseni. Kwa hiyo, tafsiri ya mvuvi ni mvuvi ye yeyote anayeshika ndoana anakwenda kuvua samaki mmoja au wawili. Kwa hiyo, lazima atawajibika kuwa na leseni, sasa hili ni tatizo. Kwa hiyo tukiichukulia tafsiri ya sheria hiyo ndugu zangu Wakisi na Wamanda itakuwa matatizo. Wao hawana kitoweo kingine, ni kukimbilia kwenye samaki pale anachukua wawili, watatu anaondoka. Sasa leo huyu anaambiwa kwamba lazima awe na leseni, ni ngumu hiyo. (*Makofsi*)

Kwa hiyo nafikiri kwamba, hapa pange -*qualify* kidogo kwamba, huyu mvuvi tunayezungumzia hapa wa leseni ni *commercial* siyo huyu mvuvi anakwenda pale na dema la samaki anakwenda kuweka pale gona, anaweka pale watu watatu tu na familia yake halafu awe na leseni ya shilingi 2,000 ataweba wapi itakuwa kero vilevile. Kwa hiyo, nafikiri pawepo na *ku-qualify* huyo mtu, *who is a fisherman* katika maana hiyo? Vinginevyo anakwenda kuna mto mmoja unaoitwa Mchuchuma ambao tumezungumzia sana kuhusu makaa ya mawe, lakini Mchuchuma ni mto huo, anakwenda kuvua samaki mle, unasema huyo awe na leseni, ni haki gani hiyo na atapata wapi hiyo fedha kwa ajili ya kulipia leseni? Lazima kuwe na tafsiri inayoelewaka vizuri hapo. (*Makofî*)

La pili, nimefurahi sana kusikia mnazungumzia habari ya mvuvi kulinda yale maeneo ambayo kwa kweli mengine ni mazalio ya samaki. Kwa mfano, tuna maeneo katika Ziwa Nyasa hasa Mto Luhulu unaokata kati ya Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Iringa, pana samaki wazuri pale aina ya mbasa, kuna ningi, mbelele na matuga, hawa samaki wote wanapotea kwa sababu wanavua wameharibu maeneo yale. Hivyo, nakubaliana kwa kweli kuwe na utunzaji wa mazingira pale na hiyo kwa kweli mimi naifurahia kwa sababu yale mazalio yote yanachukuliwa hiyo nakubali.

La tatu ni kwamba, Muswada huu unatoa nafasi kwa mvuvi na ninaona sasa mvuvi anaanza kukumbukwa kumbukwa hivi, kwa kuanzisha Mfuko ambao manautwa Mfuko wa Maendeleo, nadhani ni *the Fisheries Development Fund*, nafikiri hivyo, kwa hiyo hapa naona kidogo kuna *right*.

Halafu lingine ambalo nalionna walitazame vilevile kwenye sheria wamezungumzia sana habari ya kwamba kila chombo cha mvuvi lazima kiwe *registered*, kwa maana kwamba kiwe na leseni. Sasa kuna vyombo vingine katika maeneo ya kwetu havitumiki kwa ajili ya kuvua ni kama baiskeli tu. Mtu anatoka hapa anakwenda sehemu nyingine *like a bicycle* ambayo hata juzi Serikali iliondoa ushuru wa baiskeli. Nadhani hata mitumbwi ya kwetu ile ingeondolewa ushuru haina chochote, mtu anatoka tu anasafiri kupeleka mtoto wake shulenii, maana kuna Kata nyingine kama za Lumbira, Makonde, Kirondo na sehemu za Lupingu ni sehemu ambazo watu wanatembea hakuna usafiri mwininge isipokuwa kwa kutumia mitumbwi tu. Sasa hiyo mitumbwi haitumiki ni midogo sana, lakini sasa sheria hii ime-*generalize* kwamba nao wapate leseni, sasa mbona ushuru wa baiskeli mmeondona! Kama mmeondona ushuru wa baiskeli je, mtumbwi mtu anaotumia kwa ajili ya kupeleka mtoto shulenii au hospitali, kwa hiyo kuwepo na tafsiri nzuri.

Lingine bado naona vilevile kuna matatizo kama wenzangu walivyozungumzia, Kituo cha Utafiti wa Uvuvi (*Research Centre*). Katika Ziwa Nyasa kulikuwa na *Research Centre* zamani kituo kidogo pale Kyela kwa kweli kimepitwa na wakati sasa hivi. Nadhani Wizara ifanye kila juhudii kuhakikisha kwamba, Ziwa Nyasa linakuwa-*covered* na *Research Centre* inayoelewaka. Hakuna hapa *Research Centre* na matokea yake ni kwamba, watu wengi sana wa maeneo haya wamehama kutoka maeneo yale wamekimbia mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu sasa ni tatizo, limejaa watu wa kutoka Ziwa Nyasa, kwa sababu hakuna *proper research* iliyo fanyika ya kuwasaidia hao

kujua maeneo yenyne samaki wengi. Kwa hiyo, ile *Research Centre* ya Kyela iimarishwe ili iweze kuwa ya manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimefurahi kwamba mnazungumzia habari ya *ku-strengthen Regional International Cooperation* ili kuwepo na *sustainable utilization of management* kwa ajili ya *conservation* na *resources* katika *shared waters*. Nakumbuka Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, wakati akiwasilisha Bajeti ya Wizara yake, alizungumzia hoja ya kwamba sasa hivi watatazama namna wanavyoweza kutunza mazingira ya Ziwa Nyasa. Sasa naona hata *fisheries* nao wanazungumzia jambo hilo na tutumie nafasi hii ya mahusiano kati yetu sisi na Malawi kuimarisha mahusiano haya, kwa sababu haya mazalio ya samaki mengine yapo Tanzania na mengine yapo kule Malawi. Kwa hiyo, hii nimeipanda hii. Sisi tuna historia kwamba, wakati mmoja wazee wetu walikuwa hawajui kama samaki wanatembea kwa safari ndefu sana. Ikatokea samaki mmoja akavuliwa upande wa kwetu ana mhuri pale, watu wakafikiri huyo samaki katoka mbinguni, kumbe yule samaki alitokea Malawi, watu wakakataa kumla, kila mmoja akipewa anakimbia. Kumbe wenzetu kule walianza kutafuta namna samaki wanavyotembea katika Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, tukifanya mahusiano mazuri na nchi ya Malawi, nadhani tunaweza kufanikisha kuwasaidia wavuvi wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hapa tunazungumzia habari ya sheria hii, labda Wizara sasa itajizatiti vizuri kwani katika kuanzia, Wilaya yangu hadi kufika Kyela hakuna chombo cha kusimamia hayo yote ambayo yatakekelezwa, *Fisheries* hawana boti na Maliasili hawana chombo, kwa hiyo, utasimamiae haya mambo. Nafikiri Wizara sasa ifanye utaratibu wa kuhakikisha kwamba, maeneo haya yanapata chombo cha kusimamia kwa sababu hakuna boti, hata mtumbwi hawana.

Halafu lingine nafikiri *section* ya 22, ambayo nimeikazia sana hapa kwamba, kwa kweli kusema kwamba, mtu hawezi kuvua ana *apply, he is granted, authorised* kuwa na leseni hizi kubwa zaidi. Kwa sababu kwa kweli maisha ya wavuvi wetu pale hawana uwezo huo. Afadhali hata umwambie kwamba alipie ada ya mtoto wa shule kuliko kumwambia akienda kuoposha kule, kuoposha ni kishwahili cha kwetu kule, maana yake ni kuvua samaki kwa kutumia ndoana, akate leseni ya mwaka mzima.

Halafu tafsiri nyingine mimi nilikuwa nafikiri kwa mfano, mtu mmoja ana nyavu lakini anashirikiana na watu labda watano au sita. Sasa mvuvi pale ambaye nafikiri awe na leseni ni yule ambaye ana nyavu pale na wale wengine ni wafanyakazi wake tu siyo wavuvi wale. Lakini kama tutawatafsiri wote kumbe mwenye nyavu ni mmoja halafu wale wengine wamekwenda kumsaidia tu pale kusudi wapate kibarua cha siku na wao ni *fishermen* wawe na leseni, kwa kweli hilo naona pengine Wizara ingejaribu kulifanyia marekebisho. Kwa sababu mwenye nyavu ni mmoja, anakwenda na vyombo viwili na wasaidizi wanamsaidia, sasa na wale nao sijui tafsiri yao nao ni *fishermen* wanapaswa kupata leseni au ni yule tu ambaye amewakusanya wale kwenda kuvua samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa sababu nimesema Muswada huu ni wa kihistoria, kwa kweli kwa kumkumbuka mvuvi, naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ALI MACHANO MUSSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi karibu ya mwisho ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, kabla sijaanza kuchangia katika Muswada huu, nisingependa kusahau kwa sababu ni mara yangu ya kwanza katika kikao hiki kupata nafasi ya kuchangia, kuwapa pole ndugu zetu wa Arusha na Moshi, ambao nina imani katika ajali iliyotokea kule Mkoani Arusha, wasafiri wengi walikuwa ni watu kutoka Moshi na Arusha. Kwa hiyo, nawapa pole kutokana na msiba ambao umewapata na Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nafikiri niipongeze Waziri wa Maliasili na Utalii, lakini pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii na Maafisa wote ambao wameshiriki katika kutayarisha Muswada huu ambao umetufikia leo tunaujadili. Lakini pia niipongeze Kamati yetu ya Bunge, ambayo ilipata muda ikaupitia Muswada huu na ikaona unafaa kufika mbele ya Bunge hili na ikatoa mchango wake. Kwa hiyo, naipongeza Kamati iliyohusika katika kuchambua Muswada huu, niseme kwamba, kazi yao ni nzuri na waendelee kufanya hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasema: “mwenye pupa hadiriki kula tamu.” Sasa na mimi kwa sababu waajiri wangu walionifikisha hapa ni wavuvi, nafikiri sitokuwa na mchango mkubwa kwa sababu ninafurahi kubwa sana kwa kuletwa Muswada huu. Kwa hiyo, nasema kwamba, naunga mkono Muswada huu na ninasema ni wakati muafaka kwa wavuvi wote wa Tanzania kufaidika na Muswada huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, ametupigia debe vizuri sana kwa Muswada huu, ninategemea utatusaidia kwa mwaka 2005. Lakini pia niseme kwamba, mchango wangu nitakaouchangia sitatoa makosa katika Muswada huu. Nitazungumzia suala la namna gani tuwasaidie wavuvi wadogo wadogo. Kwa sababu kuna watu ambao wamenitangulia na naamini wamenitangulia mara mbili kwa sababu wamenitangulia kwa elimu na wamenitangulia kwa kusema na pia wamenitangulia kwa sababu ni watu wa Visiwani vilevile. Kwa hiyo, wanajua maana ya uvuvi, mama yangu kule mwisho, Mama Getrude Mongella amenifilisi. Kwa sababu nilikuwa tayari nimeshaomba nikaona nisimame tu niseme kidogo ili waajiri wangu wajue kwamba nimewajibika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ulivyo ni kwamba, kuna baadhi ya mambo yatasemwa kwa siku ambazo itabidi kusemwa. Sasa wakati huu ni wakati muafaka wa kuzungumzia masuala ya uvuvi kwa sababu ni kitu kimoja ambacho tunasema kwamba tunataka kuondoa umaskini na Watanzania wengi tuna uhakika ni maskini. Lakini pia niseme kwa furaha kuwa wengi wetu hapa tunakula samaki na kama kuna wengine ambao hawali samaki basi sijui kuna nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwenzangu mmoja ametoa mfano amba o na mimi nataka nisiwe mbali naye, amesema maneno mawili, matatu na akawa amemaliza lakini yanayoeleweka. Mimi ninachosema ni kwamba, katika suala la wavuvi tuangalie Watanzania wetu, wengi wanaoonekana maskini ni wale wanaofanya kazi ya uvuvi.

Tukiangalia kuanzia Tanga mpaka kufika Bagamoyo, tukija Dar es Salaam pale *Ferry*, wale unaowaona wote ni wavuvi, tunaenda mpaka Lindi na Mtwara, lakini hatuishii hapo tukienda kwenye Visiwa vya Ukerewe kwenye Ziwa Victoria, tukienda kwenye Ziwa Nyasa na maziwa mengine, kuna wavuvi, hata tukienda Moshi kule kuna wavuvi, Kigoma kuna wavuvi. Sasa tunapozungumzia suala la wavuvi tunazungumzia karibu robo tatu ya Watanzania.

Kwa hiyo, kwa sababu wenzangu wamenifilisi, nafikiri niseme kwamban itakapopita sheria hii, kuna uwezekano mkubwa tukawapa faida Watanzania wengi.

Kwa hiyo, mimi nasema kwamba naunga mkono Muswada huu na Mwenyezi Mungu, ajalie tuupitishe bila vikwazo ili Watanzania waweze kufaidika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu napendekeza utakapopita Muswada huu tu basi tuwatazame kwa jicho la huruma wavuvi wadogo wadogo amba o ndiyo wenzetu. Wavuvi gani hao, wavuvi hawa ni wale amba o wanavua samaki katika bahari zetu amba o hawana mipaka, kwa sababu wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu wanavua samaki wengi sana, lakini kwa umaskini wao samaki wanaowavua wanakula kidogo kuliko amba o wanataka kuharibika. Sasa wanachukua bidii ya kutoa samaki karibu na Nungwi, Bumbwini au Kizimkazi na wanawaleta feri Jijini Dar es Salaam. Sasa kama tutasema tunaweka mipaka tuelewe kwamba wavuvi wa Zanzibar wanaauza samaki feri Jijini Dar es Salaam. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na wakati huo huo kuna samaki amba o wanavuliwa Mwanza tunawanunua pale Kariakoo, kuna aina ya samaki wa kamba wanaovuliwa Lindi na Mtwara nao wanakuja kuliwa Dar es Salaam, sasa mipaka yetu nafikiri tuangalie tusiwe na mipaka katika masuala ya uvuvi. Sasa ninachosema ni kwamba, tutafute mbinu za kuwawezesha wavuvi wavue samaki kwa wingi ili wale nao wafanane na Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyotuona. Sasa baada ya kuvua samaki hao isiishie hapo kwamba wavuvi wavue samaki waje wawauze kwa bei rahisi na yawe yamemalizika.

Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri kuna hizi faini ambazo zinajitokeza kwa wale amba o watafanya makosa au leseni zinazolipiwa na wavuvi amba o labda wanavua bahari kuu. Mimi ningependekeza fedha zile zinazopatikana basi wajengewe viwanda kiasi ambacho samaki hata wanapokuwa wengi wauze kwenye viwanda vya kusindika samaki ili wasafirishwe wakati mwingine kupelekwa nje ya nchi yetu.

Lakini si kujengewa viwanda tu, wangewezeshwa wavuvi hawa kwa kupatiwa mafriza au hifadhi nyingine ambapo watakapokwenda kuvua samaki waweze

kuwahifadhi samaki hao, wasiwe wanasema kwamba samaki wamekuwa wengi wawahifadhi ili wawauze kipindi kingine ambacho samaki huwa hawapatikani . (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sheria itakubalika na wavuvi wakapewa msaada huu, tunaweza kufaidika kwa sababu samaki wanapovuliwa wakiwa wengi, kuna wakati ambao hawapatikani basi tutakuwa tunaondoa umaskini kiasi ambacho wananchi wetu watakuwa wamefaidika na wale wengine ambao si wavuvi, matokeo yake biashara zao zitakuwa nzuri zaidi. Kwa hiyo, naomba sheria hii ipite na itakapokuwa imepitishwa basi Mheshimiwa Waziri, atilie maanani namna ya kuwawezesha wavuvi kuweza kupata maslahi katika shughuli zao za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nisingeishia hapo, kuna hili zao la mwani sijatembea sana katika Pwani za huku Tanzania Bara, kwa mfano kutoka Mtwara mpaka kufika Tanga. Lakini kwa kule Zanzibar inaonekana kwamba, mwani unavunwa kwa wingi.

Kwa hiyo, nina hakika hata Mafia mwani utakuwepo. Sasa kama mwani ni zao la baharini, hebu tuchukue nafasi kama tunavyotafuta masoko ya pamba, tunavyotafuta masoko ya tumbaku, tunavyotafuta masoko ya alizeti, tunavyotafuta masoko ya korosho, basi na zao la mwani vilevile tulitafutie soko kiasi ambacho wananchi wetu waweze kufaidika.

Kwa uchunguzi nilioufanya ni kwamba, kuna watu wanawenza kwenda kuvua bahari kuu, lakini ulimaji wa mwani unalimwa katika bahari ndogo ndogo kiasi ambacho unakwenda kwa miguu na unarudi kwa miguu. Hata akinamama wa kawaida wanalima zao la mwani.

Kwa hiyo, kama tutawatafutia soko la mwani wanawenza wakafaidika kwa kiasi ambacho kama mnayojuja, akinamama wanapokuwa na bidii mnajua wanatusaidia sana akinababa na bila akinamama mambo yetu hayaendi vizuri, lazima tukubali hilo suala.

Sasa kama tunalifikiri suala la kuwapa kipaumbele akinamama katika zao hili, tunaweza tukapata matunda fulani kiasi ambacho baada ya kujisikia tutaendelea na kujisikia na kujisikia na tena. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya kupitishwa sheria hii, atilie maanani suala la zao la mwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa sababu muda hauturuhusu na sitaki nionekane kwamba ni msemaji sana, Waswahili wanasema “sema ubakishe na ya kesho upate kuyasema.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sina budi kusema naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja na ninauombea mafanikio mema. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wabunge, huyo ndiye aliyekuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo. Kesho tutaendelea na mjadala kuhusu hoja hii. Watakaochangia kesho ni Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa John Singo na

Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, hawa ndiyo watakaochangia kesho asubuhi na hoja kuhitimishwa na Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa muda uliobakia ni dakika tatu tu, basi naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 11.57 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi
Tarehe 13 Novemba, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*

